

**UTU WA WAHUSIKA WA KIUHALISIAJABU KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID
AHMED MOHAMED**

PERES AKELLO OBONDO

Z551/4134/2016A

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KAMA SEHEMU YA KUTIMIZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

IDARA YA LUGHA, TAALUMA ZA FASIHI NA MAWASILIANO

**CHUO KIKUU CHA JARAMOGI OGINGA ODINGA CHA SAYANSI NA
TEKNOLOJIA**

JANUARI, 2023

UNGAMO LA MTAHINIWA NA IDHINI

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote.

SAHIHI

TAREHE

Peres Akello Obondo

.....

.....

Z551/4134/2016A

IDHINI YA WASIMAMIZI

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia.

Dkt. Juliet Akinyi Jagero

Idara ya Lugha, Taaluma za Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia.

Sahihi _____

Tarehe _____

Dkt. Naomi Nzilani Musembi

Idara ya Lugha, Taaluma za Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia.

Sahihi _____

Tarehe _____

HAKILINZI

© 2023 PERES AKELLO OBONDO

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kunakiliwa, kupigishwa chapa, kutafsiriwa au kutoa tasnifu hii kwa jinsi yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia.

SHUKRANI

Kwanza kabisa, ningependa kutoa shukrani kwa Maulana kwa afya njema katiki kipindi cha kuandika tasnifu.

Pili, ningependa kushukuru Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga kwa kunipa fursa ya kusomea shahada ya uzamili. Wasimamizi wangu: Dkt. Jagero Juliet na Dkt. Naomi Musembi, asanteni kwa kuvumilia udhaifu wangu. Mlisimama nami tangu mwanzo, hamkunikemea japo nilikuwa mwanafunzi ‘hafifu’ mwenye wingi wa makosa. Kwa hakika, nawaombea dua njema. Aidha, jopo lililoshughulikia kazi yangu kwenye idara na shule kuu, wote ninawashukuru.

Shukrani zangu vilevile, ni kwa familia yangu: Mume wangu Calvince Omondi, asante kwa kuwa mfadhili wa kweli, ulinifadhili katika harakati za kukosa peni za kuendeleza utafiti, wakati wa kutikisika, ulinisimamisha imara. Langu ni kukurejesha kwa Mola, akubariki. Watoto wangu wapendwa Nathaniel Obondo na Kelly Calvince ninawaenzi sana. Mola awalinde.

Kwa wazazi wangu wapendwa, Bi. Isabell Obondo na marehemu Bw. Nathaniel Obondo aliyenitia moyo ili niendeleze masomo yangu, nimepiga magoti, mikono yangu i juu, uso wangu u juu. Lengo ni kuwashukuru na kukuombea zaidi mama, ili uone jinsi Mungu atazidi kubariki vizazi vyenu. Mlikuwa jiwe la msingi, maombi yenu, ufadhili wenu na hata mapenzi yenu yaliweka nuru katika kiza. Nimefikia kiwango hiki leo kwa sababu ya maneno yenu ya busara.

Sitamsahau rafiki zangu Steve Odinga na Seth Alomo, asante kwa ukarimu wenu. Mlijitokeza, mkanisaili, mkanikosoa, mkanifunza na hata kunipa moyo, nakushukuru.

IKISIRI

Utu huhusisha wema. Utu ni sifa mojawapo muhimu katika mahusiano mazuri maishani mwa binadamu. Utu ni sifa ambayo huhusishwa na wahusika mbalimbali katika dunia halisi na hata kwenye dunia ya fasihi. Wahusika ni muhimu katika fasihi kwa vile kupitia kwao, mwandishi huweza kupitisha ujumbe aliokusudia kwa wasomaji. Wahusika huwa wa aina mbalimbali wakiwemo wahusika wa kiuhalisiajabu ambao pia huchangia katika kupitisha ujumbe wa mwandishi sawia na wahusika wa kihalisia. Tafiti za awali zimewasawiri wahusika binadamu wakionyesha utu kwa sababu ni sifa muhimu anayopaswa kuwa nayo binadamu. Hata hivyo, waandishi wa Kiswahili akiwemo Said A. Mohamed wamesawiri wahusika wa kiuhalisiajabu wakionyesha utu kwa viumbe wengine. Huu ni mtindo ambao umeanza kutumiwa katika riwaya mpya na waandishi wa fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu ulichanganua kiuhakikifu wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed ili kudhihirisha kwamba hata viumbe wasio binadamu huwa na sifa ya kibinadamu ya utu. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Malengo yaliyoongoza utafiti huu ni: Kubainisha umbo linalochukuliwa na viumbe wa kiuhalisiajabu wanapoonyesha utu katika riwaya teule za Said A. Mohamed, kufafanua udhihirishaji wa utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed na kutathmini athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa wahusika binadamu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kiuhalisiajabu kama inavyofafanuliwa na Zamora & Wendy (1995). Nadharia hii hueleza matukio katika hali ya kutisha, kushangaza na kuogofya kwa kuziwasilisha kana kwamba ni hali ya kawaida. Muundo wa kimaelezo ulitumika huku eneo la utafiti likiwa fasihi ya Kiswahili, utanzu wa Riwaya. Mwango wa utafiti umehusisha riwaya zote tatu za kiuhalisiajabu za Said A. Mohamed. Sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteua riwaya tatu za Said A. Mohamed hususan: *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)*. Data ilikusanywa kutokana na kusoma riwaya hizo tatu zilizoteuliwa na kudondoa sehemu zilizolingana na malengo ya utafiti. Data ilidondolewa, ikanukuliwa, ikapangwa kasha kuchanganuliwa. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa kwa kweli viumbe wa kiuhalisiajabu wana sifa za utu kama upendo, ukarimu, kusamehe miongoni mwa mengine. Aidha walidhihirisha umbo mbalimbali kama kuwa kivuli, mizuka na mengineyo. Vile vile binadamu waliathirika kwa kufurahi na hata kukasirika. Utafiti huu unatoa mchango kwa walimu na wataalamu wa fasihi katika taaluma ya fasihi simulizi.

ABSTRACT

Humanness involves any act related to wellness of a being. Being humane is an important aspect of life for healthy human relations. Humanness is related to various characters in the real world and in the literature world too. Characters are very important aspect of Literature. It is through characters that the writer conveys his intended message to the readers. There are many types of characters including magical realism characters through whom the writer, like the normal characters, conveys his message. Previous research have it that the humane character is only found in human beings. In as much as it is only found in human beings, some Kiswahili authors, among them Said A. Mohamed, have used non-human characters through magical realism to portray humanness. The art of writing using magical realism is a new style being used in literature by Kiswahili authors. This research therefore critically analyzes the humanness of non-human characters in magical realism to show that even non-human characters have humanness. The objectives of this study are to: identify and explain forms in which non-human characters in magical realism appear as they perform acts of humanity in Said A. Mohamed's novels, describe ways in which they perform acts of humanness in Said A. Mohamed's novels and the effect of humanness of these characters on human beings in Said A. Mohamed's novels. This study uses Magical Realism theory as expounded by Zamora & Wendy (1995). This theory explains horrifying and fantastical scenes as if they are occurring in normal situations. This study employed descriptive research design while its area of study was the genre of novel in Kiswahili literature. The population of the study are all the 3 books of Said A. Mohamed that involve magical realism. Purposive sampling was used in selecting the three novels written by Said A. Mohamed; *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010), because the writer has extensively expressed humanity through the non-human characters. Data was collected by reading the three selected texts. Excerpts were recorded, arranged as required and analyzed. The findings of the study show that non-human being characters are humane as they show traits like love, generosity and even forgiveness. When showing these traits, they changed into different forms like shadows and even ghosts. The human beings reacted differently by being happy and some by being sad, after receiving these humane acts. This research will be beneficial to students, teachers and researchers of literature.

YALIYOMO

<u>UNGAMO LA MTAHINIWA NA IDHINI</u>	II
<u>HAKILINZI</u>	III
<u>SHUKRANI</u>	IV
<u>IKISIRI</u>	V
<u>ABSTRACT</u>	VI
<u>YALIYOMO</u>	VII
<u>UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU</u>	X
<u>SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI</u>	1
<u>1.0 Utangulizi</u>	1
<u>1.1 Usuli wa Utafiti</u>	1
<u>1.2 Suala la Utafiti</u>	5
<u>1.3 Malengo ya Utafiti</u>	5
<u>1.4 Maswali ya Utafiti</u>	5
<u>1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada</u>	6
<u>1.6 Umuhimu wa Utafiti</u>	6
<u>1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti</u>	7
<u>1.8 Hitimisho</u>	7
<u>SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA</u>	9
<u>2.0 Utangulizi</u>	9
<u>2.1 Misingi ya Kinadharia</u>	9
<u>2.2 Dhana ya Uhalisiajabu</u>	12
<u>2.3 Utu wa Viumbe na athari ya utu kwa binadamu</u>	15
<u>2.4 Umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu</u>	22
<u>2.5 Hitimisho</u>	29
<u>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI</u>	30

3.0 Utangulizi	30
3.1 Muundo wa Utafiti	30
3.2 Wango la Utafiti	30
3.3 Sampuli na Usampulishaji	31
3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data	31
3.5 Uchanganuzi na Uwasilishaji Data	32
3.6 Utegemezi na Uaminifu katika Data	32
3.7 Maadili ya Utafiti	33
3.8 Hitimisho	33
SURA YA NNE: UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI DATA	34
4.0 Utangulizi	34
4.1 Umbo La Viumbe wa Kiuhalisiajabu	34
4.1.1 Mzuka	35
4.1.2 Kivuli	38
4.1.3 Binadamu Halisi wenye Uwezo wa Kiungu-Utu	40
4.1.4 Kiumbe Bila Umbo Dhahiri	42
4.1.5 Sauti	44
4.1.6 Ishara	45
4.1.7 Kiumbe cha Kiajabuajabu	47
4.1.8 Jini	48
4.2 Udhihirishaji wa Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu	49
4.2.1 Upendo	50
4.2.2 Ushauri	57
4.2.3 Kupenda Amani	64
4.2.4 Heshima	67
4.2.5 Hekima	68
4.2.6 Msamaha	71
4.2.7 Utoaji Msaada	72
4.2.8 Uwajibikaji	76
4.2.9 Usemaji Ukweli	78
4.2.10 Ukarimu	79

4.2.11 Motisha	82
4.3 Athari ya Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu	85
4.3.1 Ushirikiano.....	85
4.3.2 Furaha	87
4.3.3 Shukurani.....	89
4.3.4 Nguvu.....	90
4.3.5. Hamaki.....	91
4.3.6. Mshangao.....	92
4.3.7 Ufarakano.....	93
4.4 Hitimisho.....	94
<u>SURA YA TANO: MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI</u>	95
5.0 Utangulizi.....	95
5.1 Muhtasari	95
5.1.1 Muhtasari wa Tasnifu	95
5.1.2. Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	96
5.1.1.1 Umbo la Viumbe wa Kiuhalisiajabu.....	96
5.1.1.2 Udhihirikaji waUtu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu.....	97
5.1.1.3 Athari ya Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu kwa Binadamu.....	98
5.2 Hitimisho.....	98
5.3 Mapendekezo ya Utafiti.....	99
5.4 Mapendekezo kwa ajili ya Tafiti Zaidi	99
5.5 Changamoto za Utafiti	100
5.6 Mchango wa Utafiti	100
<u>MAREJELEO</u>	101
<u>KIAMBATISHO 1: IDHINI YA CHUO YA KUFANYA UTAFITI</u>	106
<u>KIAMBATISHO 2: IDHINI YA ERC CHUO KIKUU CHA JOOUST</u>	107
<u>KIAMBATISHO 3: KIBALI CHA NACOSTI</u>	108

UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

Utu ni hali ya kuwa na uadilifu. Ni uzuri wenye nia ya kutia wengine mazuri na mema yaliyo na kifani. Utu ni kufanya mema unavyotarajiwa na wanajamii.

Uhalisiajabu Udhirihikaji wa matukio yanayosawiriwa kuwa yasiyo ya kawaida, ya kushangaza, kuogofya na kutisha.

Riwaya ya Riwaya ambazo zimepiku mtindo wa uandishi wa kimapokeo wenye kiuhalisiajabu mkabala wa fasihi kujikita tu katika msingi wa uhalisia.

Mhusika wa Huyu ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye kiuhalisiajabu anafanana na binadamu kwa kiasi fulani cha kuweza kutenda matendo ya kibinadamu. Mhusika anaweza kuwa kiumbe aliye hai hususan binadamu, mdudu au mnyama. Pia huwa kitu kisicho hai hususan mawe, miti, mizuka na mengineyo.

SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Katika sura hii, tasnifu ilishughulikia masuala ya kimsingi yanayofaa kuzingatiwa. Masuala haya ni pamoja na usuli, suala la utafiti, malengo na maswali yaliyoongoza utafiti pamoja na sababu za kuchagua mada. Aidha, sura hii ilishughulikia upeo wa utafiti na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu.

1.1 Usuli wa Utafiti

Utu ni dhana ambayo inatambulika ulimwenguni kote kwa sababu ya mahusiano ya binadamu kijamii. Utu hukinzana na vita, ukabila, siasa mbaya, uongozi mbaya, utabaka na chochote kile kinachohusisha unyanyasaji wa binadamu (Pietersen, 2005).

Utu hujumuisha upendo na huruma haswa kwa kiumbe na huwa ni muhimu katika maisha ya binadamu. Aidha, utu huendeleza upendo na utengamano baina ya watu. Bila utu, panaweza kuwepo na vita, watu kuteswa, uongozi mbaya na maovu mengine. Kwa mujibu wa Kimeu (2016), binadamu wana mahusiano kupitia kuishi kwao, baada ya kifo na kupitia kwa hisia zao. Kimeu, anaendelea kueleza kuwa, binadamu tu ndiye ana utu kwa sababu za tofauti za hisia zao na zile za wanyama. Watunzi mbalimbali wa kazi za kifasihi wakiwemo E. Kezilahabi kwenye vitabu vyake kama vile *Nagona (1990)* na *Mzingile (1991)*, K. Wamitila kwenye riwaya, *Bina- Adamu! (2002)* na *Musaleo! (2004)* na T.Olali katika riwaya zake za *Mafamba (2008)* na *Watu wa Gehenna (2012)* wameendeleza maudhui ya utu. Ijapokuwa yamehusisha utu na binadamu. Utu hudhihirika haswa kwa binadamu kwa vile ana hisia na hupenda kutoa usaidizi kwa viumbe wenzake. Ijapokuwa utu huonekana sana kwa binadamu, wanyama na viumbe wengine pia huwa na utu.

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajriba mbalimbali za maisha ya wanajamii, ambayo huwasilishwa kwa njia ya mdomo au kupitia maandishi. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999) fasihi inawasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikizano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi inawasilisha maudhui yenye mguso kwa wanajamii kupitia kwa lugha iliyojaa mvuto. Aidha, msanii ni zao la jamii na hujaribu kuwasilisha matukio ya jamii katika uhalisia wake. Msanii huwasilisha maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka

za kitamaduni, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kupitia kwa kazi za fasihi tunapata picha kamili ya jamii ya kisasa. Hakuna fasihi inayoibuka katika ombwe. Kila fasihi ni zao halisi la jamii na inaonyesha kuwepo kwa jamii hiyo kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Hivyo, kadiri wakati na jamii unavoendelea kubadilika ndivyo kazi za fasihi zinavyobadilika zikiwemo riwaya za Kiswahili. Utanzu wa riwaya ulichipuka baada ya ukoloni wa Kimagharibi na unaendelea kukua ili kukidhi mahitaji ya jamii inayopitia mabadiliko katika nyanja za kijamii, kisiasa, kielimu, kiuchumi na kiteknolojia.

Wahusika ni muhimu sana katika fasihi (Senkoro, 1982). Kupitia kwao mwandishi huweza kupitisha ujumbe aliokusudia kwa wasomaji. Wahusika huwa wa aina mbalimbali wakiwemo wahusika wa kiuhalisiajabu ambao pia wanatwikwa majukumu muhimu katika kazi za sanaa. Waandishi wengi ambao wameshughulikia masuala ya uhalisiajabu wameweza kutumia wahusika kufanikisha hali hii ya sanaa ya uandishi wa kiuhalisiajabu katika kazi zao za fasihi. Hivyo basi, Senkoro keshataja kuwa, suala kuu hapa ni kwamba wahusika ni nguzo muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Utafiti huu ulishughulikia wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule kwa lengo la kuonyesha kuwa, pia nao wanamiliki sifa muhimu za kibinadamu ikiwemo sifa ya utu.

Ubunifu humwezesha msanii kuwaumba au kuwasawiri wahusika kinafsia, kiakili, na kimwili. Usawiri wa wahusika unaofanywa na msanii hutegemea mbinu mbalimbali ambazo msanii huyo amezitumia. Madumulla (2009) anaeleza kuwa, mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi na ni kiini cha vitu vyote vipya, dhamira na mada katika fasihi. Madumulla anaendelea kueleza kuwa, katika mhusika kuna uwili: kwanza, kuna usawiri wa kisanaa wa mtu kwa upande mmoja; pili kuna sura ya mtu kwa upande mwingine. Hivyo basi, kupitia mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu, utafiti uliweza kuwachora viumbe wa kiuhalisiajabu.

Viumbe mbalimbali huhusishwa na uhalisiajabu ikiwemo mizimu, mizuka, miungu, vifaa, binadamu hai, wanyama miongoni mwa viumbe wengine. Mbiti (1980) anaeleza kuwa; Waafrika wanaamini kuna nguvu za ajabu ambazo hutoka kwa kiumbe wa ajabu mwenye nguvu na uwezo zaidi. Kiumbe huyu tena husambaza nguvu zake kwa viumbe wengine au kwa vifaa. Mbiti, anasisitiza kuwa, nguvu hizi za ajabu huweza kutumika kwa njia chanya au hasi. Aidha, anasema kuwa Wakristo huamini tu kuwa nguvu hizi zinazotumika na viumbe hawa, hutumika kutenda mambo maovu tu kwa kuwa hudhibitiwa na binadamu kama vile wachawi na waganga. Hivyo

kutokana na mtazamo huu; utafiti uliweza kudhihirisha kuwa viumbe wa kiajabu huweza kutumika kwa njia chanya.

Uhalisiajabu ni njia mojawapo ya kusawiri matukio ya kifasihi (Nyambunga, 2005). Kwa mujibu wa Nyambunga, matukio husawiriwa kwa njia ya kiajabuajabu, kuogofya na kutisha. Hata hivyo, ingawa matukio hayo huwa ya kiajabu, huashiria hali halisi ya maisha katika jamii. Wanadamu katika maisha yao huamini kuwa, mambo ya kiajabuajabu hutendeka. Mambo haya huhusishwa na viumbe mbalimbali ikiwemo mizimu, binadamu hai, wanyama miongoni mwa viumbe wengine. Ijapokuwa viumbe wengine huwa wa kuangamiza, huwa kuna viumbe ambao katika hali ya uhalisiaajabu hudhihirisha utu kwa viumbe wengine.

Suala la uhalisiajabu limeshughulikiwa na watafiti wengine katika viwango tofauti. Baadhi ya tafiti hizo ni zile zilizofanywa na Onchwati 2016, Vutagwa (2013), Mwangi (2013), Magaju (2004) na wengineo. Onchwati (2016) na Mwangi (2013) wamezungumzia suala moja la uhalisia na uhalisiamazingaombwe ila wamehakiki vitabu tofauti. Vutagwa (2013) na Magaju (2004) nao wamehakiki suala la uhalisiajabu ila katika tanzu tofauti za fasihi. Kazi hizi aghalabu, zimeangazia kwa ujumla suala la uhalisiajabu katika vitabu tofauti. Hivyo, utafiti huu ulitumia sifa za uhalisiajabu kudhihirisha uhusika wa viumbe wa kiuhalisiajabu na kuonyesha jinsi wanavyodhihirisha utu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Sifa ya utu ambayo kwayo huwa sifa inayohusishwa na binadamu.

Utunzi wa riwaya za kiuhalisiajabu ni mtindo mpya wa utunzi. Mtindo huu unapiku njia za kimapokeo za uandishi wa fasihi ambao riwaya inapaswa kujengeka katika msingi wa uhalisia. Hivyo, kimsingi, riwaya hizi za kiuhalisiajabu huitwa “riwaya mpya”. Riwaya mpya au riwaya za kimajaribio kulingana na Wamitila (2003) ni riwaya ambazo hukiuka kaida za kawaida za utungaji na muundo wa riwaya. Anasema kuwa, riwaya za aina hii zina msuko, hadithi na wahusika wenye sifa zisizokuwa za kawaida. Kwa mfano, msuko huenda ukachanganya lugha ya msimulizi na mhusika, wahusika hawana sifa zinazowabainisha waziwazi na hawana wasifu wa wahusika halisi. Wamitila anaendelea kuelezea kuwa, riwaya mpya pia huitwa riwaya za kimajaribio ambayo ni dhana inayotumiwa kuirejelea riwaya iliyozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na kuakisi uhalisia wa hali ya juu na matumizi ya mbinu za kiubunifu za uandishi wa riwaya. Anafafanua kuwa, waandishi wa mkondo huu huwa na nia za kuziasi kaida za kijadi za uandishi wa riwaya, pamoja

na kuyapinga baadhi ya mawazo waliyonayo wasomaji kuhusu fasihi na hasa ya neno riwaya. Akiendelea kufafanua kuhusu riwaya hizi, Wamitila anaeleza kwamba riwaya hizi mpya pia hushughulikiwa vilivyo na wasanii wa usasaleo wakiwa na lengo la kubuni wahusika wenye ujumbe unaobeba matendo ya kushtua na kutia hofu. Waandishi hawa huwa na nia ya kujitenga na mitindo ya kawaida ya uandishi wa riwaya.

Baadhi ya riwaya za kiuhalisiajabu za Kiswahili ni kama vile *Bina- Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) za K.Wamitila, *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za E. Kezilahabi, *Babu Alipofufuka* (2002), *Nyuso za Mwanamke* (2010) na *Dunia Yao* (2006) za S. A. Mohamed, *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* (2012) za T. Olali miongoni mwa zingine. Mtindo huu wa utunzi umewezesha hali ya kukabiliana na mabadiliko kadha yanayozikumba jamii zetu za kisasa. Jambo hili linawapa waandishi wa riwaya mpya fursa ya kuyaeleza mambo ambayo hayangeweza kuelezeka kwa uwazi kwa mitindo ya kawaida.

Riwaya za kiuhalisiajabu huwa na sifa mbalimbali. Njogu na Chimera (1999) wanataja sifa hizo; Kwanza, zinaibua uhalisia na taratibu za maisha kama vile dini na siasa zinatazamwa kwa jicho la ukali na udhaifu wake unafichuliwa bila woga. Pili, wahusika wanahusishwa zaidi na hisia zao na masuala ya utu wao; wanaingiliana na jamii pana kwa mahusiano mbalimbali kisosholojia, kiuchumi na hata kisiasa. Wahusika hawa huhusishwa na kila tendo katika jamii. Tatu, Muundo changamano unaokiuka baadhi ya taratibu na uzoefu wa uandishi wa riwaya, ambazo humtumbukiza msomaji katika njia taratibu ya kumkomaza msomaji ashiriki kikamilifu na kufuatilia usimulizi kwa kina. Nne, uhalisiajabu hutumika yaani uhalisia wa kiajabu. Tano, kuna matumizi mengi ya ndoto. Sita, wahusika halisi wanatumwiwa kinyume na wahusika wanyama waliotumiwa katika riwaya za awali. Hali ya kisaikolojia ambayo inamsukuma mhusika kutenda jambo fulani inatiliwa maanani.

Katika maisha halisi ya binadamu, vitu vya ajabu hutendeka. Mara nyingi binadamu katika uhalisia wake huwa hawezi kueleza chanzo cha matendo haya ya kiajabuajabu. Hivyo ni muhimu kuangazia suala hili kwa vile ni mambo yanayoambatana moja kwa moja na maisha ya binadamu. Ingawa dhana ya uhalisiajabu inahusishwa na waanzilishi wa Kimagharibi, dhana hii imekuwepo katika fasihi simulizi za jamii nyingi ulimwenguni. Waandishi wa riwaya hizi wamethibitisha masuala ya uhalisiajabu ambayo hayatokei tu katika jamii zao, bali katika jamii nzima ya

ulimwengu. Said A. Mohamed ni mmojawapo wa waandishi wanaotumia uhalisiajabu katika maandishi yake. Utafiti huu ulishughulikia suala la uhalisiajabu katika riwaya za Said A. Mohamed.

1.2 Suala la Utafiti

Ni kweli kuwa utu ni sifa mojawapo muhimu katika maisha ya binadamu. Suala la utu limeshughulikiwa Zaidi jinsi utu unavyodhihirishwa na binadamu. Licha ya kuwa utu ni sifa ambayo inahusishwa na binadamu, viumbe wengine pia hudhihirisha utu. Katika hali halisi viumbe kama wafu, vivuli, mawe hawawezi kudhihirisha utu. Kutokana na haya utafiti huu ulishughulikia suala la utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed ukiwa na lengo la kubainisha kuwa wana sifa ya utu kama binadamu halisi.

1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Ili kutimiza lengo hili utafiti uliongozwa na malengo mahususi yafuatayo:

- i. Kubainisha umbo linalochukuliwa na viumbe wa kiuhalisiajabu wanapoonyesha utu katika riwaya teule za Said A. Mohamed
- ii. Kufafanua udhihirishaji wa utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.
- iii. Kutathmini athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu wahusika binadamu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Je, viumbe wa kiuhalisiajabu wanachukua umbo lipi wanapoonyesha utu katika riwaya teule za Said A. Mohamed?
- ii. Viumbe wa kiuhalisiajabu wamedhihirishaje utu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.
- iii. Je, utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu una athari gani kwa wahusika binadamu katika riwaya teule za Said A. Mohamed?

1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada

Kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu uhalisiajabu. Watafiti wamezishughulikia katika viwango tofauti. Baadhi ya tafiti hizo ni ule uliofanywa na Onchwati (2016), Vutagwa (2013), Mwangi (2013), Magaju (2004) na wengineo. Kazi hizi aghalabu, zimeangazia kwa jumla suala la uhalisiajabu. Watafiti hawa wamezungumzia sifa za uhalisiajabu, tofauti ya uhalisiajabu na uhalisia na matukio yalivyodhihirika katika vitabu tofauti.

Utafiti pia umefanywa kuhusiana na utu ila tu ni suala ambalo limeshughulikwa tu kwa kifupi chini ya mada nyingine. Ndanu (2018) ameshughulikia suala la utu katika *Maudhui ya Ukombozi*. Ameangazia utu kama maudhui katika kazi yake. Chepkoech (2017) naye anazungumzia suala la utu katika *Usawiri wa maudhui yenye kufunza wanafunzi wa vyuo maadili mema: Tathmini ya Alidhani Kapata na Damu Nyeusi*. Tofauti na tafiti hizi, utafiti huu ulishughulikia suala la utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya za *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)* za Said A. Mohamed lengo likiwa ni kubainisha kuwa, wahusika hawa wanamiliki sifa ya utu inayohusishwa na binadamu pekee. Uhakiki hutegemea mabadiliko ya kijamii kulingana na wakati na katika maendeleo ya kihistoria ambayo kwa njia moja au nyingine huathiri maendeleo ya fasihi. Pia, hakuna uhakiki unaoweza kudaiwa kwamba umekamilika kwa sababu wahakiki labda hutofautiana kwa mitazamo na misimamo (Onchwati, 2016). Utafiti huu ulishughulikia suala la uhalisiajabu ili kudhihirisha mabadiliko ya mtazamo kuwa viumbe wa uhalisiajabu hudhihirisha uovu (Mbiti, 1980).

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Mtindo, uhusika na wahusika, maudhui, mandhari na mazingira katika riwaya mpya zinazoongozwa na nadharia ya uhalisiajabu huwa tatizi kwa wasomaji hususan wanafunzi, waalimu na wataalam mbalimbali. Hivyo basi, wanafunzi, walimu na wataalam mbalimbali watanufaika haswa wanapofuatilia jinsi suala la uhalisiajabu limebainisha maudhui mbalimbali ikiwemo utu.

Data iliyokusanywa itarejelewa na watafiti wengine, wanafunzi wa fasihi na hata wataalamu mbalimbali wa lugha ya Kiswahili na fasihi yake. Itaweza pia kusaidia katika idara ya Lugha,

Taaluma za Fasihi na Mawasiliano ya JOOUST kwa vile wanafunzi watafiti watapata marejeleo ya data itakayowasaidia katika tafiti zao zenye uhusiano na huu.

Wajibu wa Taasisi ya kuendeleza mitalaa wa kupendekeza vitabu vya fasihi katika viwango mbalimbali vya elimu utarahisishwa. Utafiti una mawazo mapana kuhusu maudhui, uhusika na wahusika. Hizi ni mojawapo za mbinu mbalimbali za kuangazia katika mapendekezo yao.

Utafiti huu ulichangia katika kuboresha Kiswahili katika asasi za elimu hasa tukirejelea fasihi ambayo hujengewa msingi hasa kuanzia shule za upili.

Aidha, ni mchango kwa waandishi, watafiti na wahakiki wa tafiti zitakazotumia nadharia ya uhalisiajabu na watakaoshughulikia maudhui ya utu katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa kuweza kubainisha kuwa katika dunia ya kiuhalisiajabu mema hutendeka.

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza riwaya teule za Said A. Mohamed ambazo ni; *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)*. Utafiti huu vilevile uliyafafanua masuala ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu, umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu wanapodhihirisha utu na jinsi utu wa viumbe ulivyoathiri wahusika binadamu. Utafiti huu umeangazia mwandishi Said A. Mohamed kwa kuwa kama mwandishi mkongwe wa Kiswahili, japo ameandika vitabu vingine vikiwemo riwaya, tamthilia na hata mashairi, kazi hii ilizingatia riwaya teule kwani zinaibua suala la utu wa viumbe ambalo watafiti wa awali walidai ni binadamu pekee ambaye anamiliki sifa hii.

Aidha, sifa za wahusika ni nyingi lakini kazi hii ilijifunga kwa sifa ya utu pekee, tofauti na waandishi wengine walioangazia utu ila kupitia wahusika binadamu. Kupitia uhakiki wa riwaya teule, data toshelevu ilipatikana kwa sababu kutokana na mapitio yaliyoyafanywa, riwaya hizi zimeonyesha mwelekeo wa utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu.

1.8 Hitimisho

Sura hii imejadili usuli wa kazi hii ambao umeweka msingi wa suala lililotafitiwa. Usuli huu umeshughulikia masuala kadhaa. Suala la utunzi wa kiuhalisiajabu kama mtindo mpya wa uandishi

limeshughulikiwa. Wahusika nao wameshughulikiwa kama sehemu muhimu ya fasihi. Vilevile, suala kuu la utu nayo limeelezwa katika sehemu hii. Malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, msingi wa uteuzi wa mada, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na misingi ya kinadharia imeshughulikiwa katika sehemu hii. Kwa hivyo, sura hii imejenga msingi ambao kwao mapitio na tahakiki ya maandishi zilifanywa. Sura inayofuata inawasilisha mapitio ya maandishi ili kubainisha haja ya kuchunguza utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura hii inahakiki maandishi yanayohusiana na uhalisiajabu. Mapitio mbalimbali hutoa mwongozo unaofaa kwa mtafiti. Maandishi haya yanaangazia dhana ya uhalisiajabu, utu wa viumbe, uhusika na mbinu za usawiri wa wahusika na mapitio kuhusu utu wa viumbe hawa unavyoathiri binadamu. Lengo hasa la kufanya mapitio ya maandishi ni kuchambua tafiti zilizofanyika ili kubaini pengo lililopo.

2.1 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisiajabu. Zamora & Wendy (1995) anatumia kwamba nadharia hii iliasisiwa mwaka wa 1925 na Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz Roh alitumia istilahi uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelezea na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya ujiza uliomo kwenye uhalisi uliozoelewa na unaotokana na ujarabati.

Zamora & Wendy (1995) wanatumia kwamba nadharia hii pia hujulikana kama nadharia ya uhalisia mazingaombwe na ni mojawapo ya nadharia za usasa-leo ambazo hushikilia kwamba kazi ya fasihi hujengwa kutokana na kuchanganya mambo ya kiuhalisia na mambo yasiyo ya kiuhalisia. Zamora na Wendy wanasema kuwa katika uhalisiajabu, uhalisia na ndoto havitofautishwi. Njogu & Chimerah (1999) wanaeleza kuwa, uhalisiajabu ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyo zoelewa na maandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa.

Kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabuajabu. Wamitila (2003) anatoa mifano ya wahusika wanaopatikana kwenye riwaya ya Marquez, *One Hundred Years of Solitude* ambao wanaishi chumba cha choo bila kutambua na pia kupaa angani na shuka ya jirani. Hivyo, Wamitila (2003) anaeleza kuwa, wahusika wengi wa Juan Rulfo katika *Pedro Paramo* ni wafu na msimulizi wa hadithi anaendelea kusimulia hata baada ya kufariki.

Kwa hivyo hii ndiyo nadharia mwafaka katika uchambuzi wa kazi hii kwa sababu kuna matukio yasiyoaminika ya kifantasia, yanasawiriwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida katika riwaya hizi. Vilevile mambo ya kiajabu yanaelekezwa kwa namna ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida.

Nadharia hii ina mihimili yake ambayo imetokana na kazi za Danow (1995), Cooper (1998), Zamora & Wendy (1995) na Encarta encyclopedia (2002). Wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu, hivi huvuka mipaka ya kitaifa au kimataifa. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu. Hivyo utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo;

Mhimili wa kwanza katika nadharia ya Uhalisiajabu ni ndoto. Ndoto huchukua nafasi muhimu sana kwani matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni. King'ei (2002) anaeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamano. Kwa kuwa ndoto huchukua nafasi muhimu katika nadharia ya uhalisiajabu, utafiti ulichunguza jinsi mwandishi Mohamed ametumia ndoto katika riwaya zake kufanikisha uwasilishaji wa utu wa wahusika wake wa kiuhalisiajabu.

Mhimili wa pili wa nadharia ya kiuhalisiajabu inaeleza kwamba matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Jambo hili hufanywa kwa kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Mwandishi hutumia mbinu rejeshi kuvunja mtiririko wa vitushi (Zamora & Wendy, 1995). Utafiti huu pia uliweza kurejelea matukio rejeshi katika riwaya za Said A. Mohamed ili kuweza kuthibitisha iwapo kuna ukosefu wa mantiki, vilevile nadharia hii iliwezesha utambulikaji wa mhusika mwenye uwezo wa kujibadilisha katika maumbo mbalimbali anapodhihirisha utu.

Mhimili wa tatu ni kwamba, simulizi zote hutegemea uhalisia ambapo kazi za fasihi za uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida. Hivi katika matini ya uhalisiajabu jambo lolote huweza kujiri wakati wowote. Mathalani, mtu aliyelala ndani anaweza kujikuta yuko nje asubuhi. Matokeo haya ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya (Zamora & Wendy, 1995). Mwandishi huyu anatumkumbusha kuwa, pamoja na kuwa tunaishi maisha ya kawaida yapo upande wa pili yaliyosheheni wazimu na maajabu. Kwa kuwa matokeo ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, hushangaza, huduwaza na huogofya, utafiti huu ulichanganua matokeo haya ya kiajabuajabu yalivyohusishwa na viumbe wa kiajabuajabu. Matokeo haya ya kuogofya na kuduwaza yatahusishwa na utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu unapodhihirika.

Mhimili wa nne inaeleza kwamba, mazingira ni sehemu muhimu katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu (Zamora & Wendy, 1995). Hivyo utafiti huu pia ulinua kurejelea mazingira na kutambulisha uajabu katika mazingira mbalimbali yalivyojitokeza kwenye wahusika wa riwaya za Said A. Mohamed kuafikisha mada na malengo ya utafiti. Katika mazingira haya mbalimbali, viumbe wa kiuhalisiajabu waliweza kudhihirisha sifa ya utu kwa binadamu.

Mhimili wa tano ni kwamba uhalisiajabu hutumia taswira kujengea msomaji picha mawazoni mwake na kumwezesha kutafakari kuhusu matukio hayo yanayotokea. Hii inatokana na ukweli kuwa kazi ya fasihi husawiri maisha halisi ya binadamu kupitia lugha ya picha na ishara kisha kuiwakilisha katika jamii. King'ei (2002). Mwandishi Said A. Mohamed ametumia taswira katika riwaya zake teule kujenga wahusika wa kiajabuajabu. Vile vile, taswira inajitokeza wakati viumbe wa kiuhalisiajabu wanadhihirisha utu kwa maumbo na mazingira mbalimbali.

Mihimili mitano iliyoelezwa hapa inawasilisha mawazo katika nadharia ya uhalisiajabu yaliyoongoza uchunguzi wa utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

2.2 Dhana ya Uhalisiajabu

Uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Franz Roh. Inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Wamitila (2003) anasema kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Kwa mujibu wa Alomo (2016) uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasaleo inavyotuhimiza kuwaza upya juu ya dhana ya kimapokeo kuhusu riwaya ya uhalisia ya karne za kumi na nane na kumi na tisa. Uhalisiajabu unatuhimiza kufikiria kuhusu ufaafu wa baadhi ya mitindo tofauti ya uandishi kwa kuangazia mada tofauti tofauti. Baadhi ya waandishi wanajadili uhusiano kati ya historia na masimulizi ya ubunifu, huku wakitumia visaasili katika kazi zao. Maoni ya mtaalamu huyu, yalisaidia utafiti huu kuhakiki mtindo alioutumia Mohamed kudhihirisha utu katika riwaya zake teule.

Istilahi hii ya uhalisiajabu inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida (Mbatia, 2002). Utafiti huu uliangazia matendo ya viumbe wa kiuhalisiajabu pamoja na matukio ya kiajabu yaliyotokea wakizuka kwa maumbo mbalimbali.

Akizungumzia “Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha Kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*” Walibora (2010: 147) anahoji na kusema kuwa “baadhi ya waandishi wa lugha ya Kiswahili wametekwa na mvuto wa ajabu wa uhalisiamazingaombwe” huku akiwataja Kyallo Wamitila, Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed kama masogora wa utunzi huu wa kimajaribio au utunzi mpya kama unavyotambuliwa na wengine. Ameonyesha kuwa Kezilahabi ametumia mtindo huo katika *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991); Kyallo Wamitila, katika *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo* (2004), na Said A. Mohamed kwenye *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Kwa kuzingatia kazi zao za fasihi, imeweza kubainika kwamba waandishi wote hawa wamo kwenye tapo moja linalosawiri uhalisia kama ulivyo lakini

unaojumuisha vipengele vya kimazingaombwe. Waandishi wote hao wameandika kazi zao hizo katika kipindi cha ubaadaukoloni katika karne ya 21 wakilenga jamii za Afrika mashariki. Kutokana na uandishi katika tapo hili jipya utafiti huu ulinua kushughulikia suala la utu wa viumbe katika riwaya hizi za kiuhalisiajabu.

Katika makala ya Khamis (2005) ya “Vionjo vya Riwaya Mpya” anabainisha kuwa riwaya za Kiswahili za Kezilahabi kama vile *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), na *Babu Alipofufuka* (2001) ya Mohamed pamoja na *Bina-Adamu!* (2002) ya Wamitila zinaweza kutazamwa kama kielelezo cha kuibuka kwa mitindo mipya ya kiutunzi katika fasihi ya Kiswahili. Sababu kubwa anayoitoa ni kwamba nchi nyingi za Afrika zimekumbwa na ukosefu wa uthabiti wa kijamii, kisiasa na kiuchumi na kwa hali hiyo waandishi hawa hutumia mtindo wa uhalisiamazingaombwe kujitakasa kwa kutumia mtindo wenye fujo na haiba” ili kuibua uozo wa maisha ya kisasa katika nchi za Afrika. Kwa hiyo, mtindo huo wa uhalisiajabu umehesabika kama mtindo mpya wa riwaya unaojipambanua kutoka katika mitindo mengine. Mtindo wa uhalisia hautoshelezi kubainisha mitagusano ya kimaisha katika nyakati za ubaadaukoloni ambapo sifa kuu ni kuwepo kwa uhalisia na uajabuajabu. Ijapokuwa waandishi wengi wametumia mtindo huu kuibua uozo wa maisha, utafiti huu utadhahirisha jinsi mwandishi Said A. Mohamed ametumia mtindo huu kuibua uzuri katika maisha kupitia utu.

Vutagwa (2013), anaeleza kuwa vigezo hivyo ni kama vile: kufufuka kwa wafu au kuwa katika hali ya mzimu au mzuka, pili uwezo wa kuponesha kimazingaombwe, tatu msaada wa kiungu, nne uajabuajabu wa kipekee na mwisho ushirikishwaji wa sanaa jaadiya na visaasili. Sifa hizo zilitumiwa katika kujadili kazi ya utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika utafiti huu kwa kuwa viumbe hao wanasheheni moja kati ya sifa hizo au zote.

Onchwati (2016) anasema: Istilahi ya ‘uhalisiajabu’ ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na hali kadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wanalinganisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yaliyotokana

na visasili na hekaya. Mawazo haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa uliweza kubainisha matukio yanavyobadilikabadilika kihalisia, kifantasia na hata kindoto.

Uhalisiajabu unahusu matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza au chochote kilicho kinyume cha uhalisia wa kawaida. Rio (2002), anaeleza kuwa la muhimu zaidi ni kwamba matukio yanayotendeka katika uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia. Vilevile nadharia ya uhalisiajabu imekuwa ya muhimu zaidi kwa sababu Rio anasema kuwa matukio ya kiuhalisiajabu yanayotendeka hayawezi kujitenga na uhalisia. Maoni haya yalifaa kwa kuwa kupitia utafiti ilibainika kuwa uhalisiajabu na uhalisia ni mambo ambayo hayawezi kutengwa.

Kwa mujibu wa Faris (2004), anasema kuwa uhalisiajabu si mchanganyiko wa uhalisia na ufantasia bali ni njia ya kuibua undani uliojificha katika uhalisia wa kila siku. Uhalisiajabu una sifa za msingi zifuatazo: kwanza sifa ya kukubali ufantasia kama sehemu ya kawaida ya maisha ya duniani. Pili, utambuzi wa uwepo wa nguvu ya kimya kimya na isiyo na umuhimu na tatu ni uwepo wa fahiwa iliyojificha. Sifa hizi zinafanya kazi pamoja kwa kuchangizana kufikia malengo ya kuonyesha uhusiano uliopo baina ya uhalisia na ufantasia. Mtindo huo humruhusu na kumpa mwandishi uhuru, ujasiri na ukunjufu wa kumchorea msomaji wake dunia na matukio ya kijinjini kama matukio ya uhalisia wa kawaida. Huoanisha dunia mbili za ufantasia na uhalisia na kukubalika kama sanaa ya kuziweka pamoja dunia hizo mbili. Mtindo huo pia unamruhusu na unamwezesha mwandishi kuvunja mipaka ya wakati. Mawazo haya yalifaa utafiti huu kwa kutambua jinsi mwandishi amekuwa na ujasiri na uhuru wa kumchorea msomaji dunia ya uhalisia na uhalisiajabu unavyojitokeza katika riwaya zake zilizoteuliwa.

Kadhalika, Faris (2004) anaeleza kuwa nyakati zilizopita na nyakati za sasa zinaweza kuendana sambamba katika usimulizi mmoja au kumfanya mhusika kuwa katika miktadha tofauti tofauti ya kipahali na kiwakati. Ni kutokana na kuoanisha ufantasia na uhalisia ndipo uhalali wa usimulizi unapata uthamani na kuaminika. Ni umoja wa kani kinzani za uhai na kifo, kabla ya ukoloni mkongwe na baada ya ukoloni, uhistoria na umazingaombwe. Dhana ya uhalisiajabu inahusishwa na visasili na utamaduni wa wazawa na hivyo kuepukana na utamaduni wa Kimagharibi wenye kumakinikia ubinafsi. Mwandishi wa kiuhalisiamazingaombwe hakusudii kuunakili uhalisia uliomzunguka bali hudhamiria kukinasa kile kilichojificha katika vitu mbalimbali vinavyoonekana

vya kawaida (Faris, 2004). Maoni haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa ulinuia kuonyesha dhamira ya mwandishi kuendeleza maudhui ya utu kupitia viumbe ambao watu hawatarajii wawe na utu.

Akifafanua kuhusu dhana ya uhalisiajabu, Mbatia (2002) ni istilahi inayotumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia. Uhalisiajabu hufanya hivyo kwa kuyaeleza matukio kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika, Mbatia (2002). Utafiti huu ulidhamiria kubainisha iwapo matukio haya ya kiajabuajabu yalitokea katika maisha ya kawaida ya jamii husika kwenye riwaya teule.

2.3 Utu wa Viumbe na athari ya utu kwa binadamu

Utafiti unadhihirisha kuwa dhana ya utu ulipata umaarufu kati ya karne za kumi na nne na kumi na saba (Battle, 2009). Utu ni hali ya kuwa na uadilifu. Utu huhusishwa na matendo mema kama vile: kulisha, kusaidia katika shughuli, kuongoza na hata kutahadharisha wengine kiasi cha kuwaathiri vyema kisaikolojia. Ni uzuri wenye nia ya kutia wengine mazuri na mema. Utu ni kufanya mema inavyotarajiwa na wanajamii (Oruka, 1990). Maoni haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa utafiti ulibainisha jinsi wahusika wa kiuhalisiajabu walitenda mazuri na mema kwa wenzao.

Neno linguine linalohusiana na utu ni Ubuntu. Neno Ubuntu linatokana na dhana “Umuntu” kutokana na lugha ya Kizulu ambayo inatafsiriwa kuwa “Mtu ni mtu kwasababu ya wenzake.” Tutu (2004) anaeleza kuwa, dhana ya Ubuntu inamaanisha upendo, ukweli, amani, furaha, uzuri, na kuwa na matumaini. Ubuntu ni sifa ya uzuri wa binadamu kwa binadamu mwenzake. Tangia awali, falsafa ya Ubuntu imekuwa ikiwaongoza Waafrika. Huonyesha jinsi binadamu hushirikiana na binadamu wengine, mazingira na Mungu muumba. Ni falsafa muhimu kwa binadamu kwa kuwa binadamu bila Ubuntu binadamu huwa mlafi, mwenye majivuno, hujipenda na hata kuwa na tabia ya uzinifu. Tutu alitumia falsafa ya Ubuntu kuongoza nchi ya Afrika Kusini wakati wa maridhiano alipokuwa kwenye tume ya maridhiano. Tutu (2000) alieleza kuwa Ubuntu unaendeleza haki. Pia anahimiza binadamu kuwa waimarishe uhusiano baina yao. Uhusiano baina ya binadamu ikiwa mzuri, basi utakuwa mzuri hata kati ya binadamu na wanyama. Tutu anaendelea kusema kuwa Ubuntu ni mojawapo ya ishara kubwa za dini za kiafrika. Ingawaje Suala la uhusiano lihasisitizwa

tu kwa binadamu, maoni haya yataweza kusaidia kutambua iwapo uhusiano nzuri ni kwa binadamu tu au pia hata viumbe wa kiuhalisiajabu kwa binadamu.

Akieleza kuhusu Ubuntu, Wichtner- Zoia (2012) anaeleza kuwa katika lugha ya Kinyarwanda na Kirundi, dhana ya Ubuntu inamaanisha ukarimu. Katika lugha hizi wanapotaja *gira Ubuntu*, wanaomba jamii nzima iwe na sifa ya ukarimu. Pia, Wichtner-Zoia anataja kuwa lugha ya Runyakitara inayotumika na Wanyoro, Watooro na Wakiga wa Uganda pia neno ubuntu kwao lina maanisha sifa ya ukarimu wa binadamu, na kushughulikia binadamu wenzake. Kupitia mawazo haya, utafiti utafanywa ibainike iwapo utu kweli ni ukarimu wa binadamu tu kwa kuwa kazi inanuia kubainisha utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

Ingawa Ubuntu ni falsafa yenye ukweli wa jinsi maisha yanapaswa kuwa. (Mandela, 1994) aneleza kuwa dhana hii haimanishi kuwa mtu hafai kujishughulikia tu, bali inamaanisha kuwa binadamu anapaswa kuangalia anachofanya kama itaweza kumsaidia yeye mwenyewe pamoja na jamii kwa jumla. Anaeleza kuwa watu ambao huhusika na Ubuntu hujitolea mhanga kufanya lolote bila kufikiria iwapo yupo katika hatari yoyote. Maoni haya yatamsaidia mtafiti kutambua iwapo kweli aliye na utu hujitolea mhanga katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

Akichangia kuhusu falsafa ya Ubuntu, Mugumbate (2013) anaeleza kuwa, mtu huweza tu kuongeza mibaraka yake kwa kusaidia wenzake katika jamii na hivyo hata kuinua hadhi miongoni mwa jamaa, (Mugumbate, 2013). Mugumbate anaendelea kusema kuwa, matendo ya Ubuntu hujitokeza kama vile kuenda kuwaona wagonjwa ambao hata si jamaa yako, kutuma rambirambi kwa waliofiwa, kupeana chakula kwa wasioweza kupata, kuwasaidia wazee na hata kusalimia watu kwa njia ya upole. Mawazo haya yaliweza kufaa utafiti kwa kuwa viumbe wa kiuhalisiajabu walionekana wakitenda matendo kama haya.

Utu ni kuonyesha upendo na huruma haswa kwa kiumbe. Utu ni muhimu katika maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu ni jambo linalo endeleza upendo na utangamano baina ya watu. Bila utu, panaweza kuwepo na vita, watu kuteswa, uongozi mbaya miongoni mwa mengine. Kwa mujibu wa (Gilbert, 2010) binadamu wana mahusiano kupitia kuishi kwao, kifo chao na hisia zao. Anaendelea kusema kuwa utu hupatikana tu kwa binadamu kwa sababu za tofauti za hisia zao na zile za wanyama. Watunzi mbalimbali wa kazi za kifasihi wameendeleza maudhui haya ya utu

husususan: Walibora (2002), Kithaka wa Mbeeria (2002) na wengineo. Kwa kuwa Gilbert anazungumzia utu kuleta utangamano, mawazo yake yaliweza kusaidia utafiti huu kwa kuwa suala la utangamano lilijitokeza viumbe wa kiuhalisiajabu wakidhihirisha utu.

Utu humsukuma mtu kumsaidia mwenzake mwenye maumivu ya kimwili, kifikra na hata ya kiakili. Kwa mujibu wa Gilbert (2010) utu una sifa za upole, unyenyekevu, maarifa na uvumilivu hivi kwamba, mtu aliye na sifa hizi ni rahisi awe na utu kwa wenzake. Maoni haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa yaliangazia sifa walizo nazo viumbe wenye utu.

Mabadiliko ya sasa yameathiri utu wa binadamu. Hili linadhihirika kwa kuwa kuna ongezeko la visa vya binadamu wasio na utu. Binadamu wanatengeneza vifaa vya kuumbua na kuharibu dunia. Vita na mauaji yanatendeka kila uchao kote ulimwenguni (Pietsern, 2012). Pietsern anaendelea kutaja kuwa mabadiliko ya ki anga, kutotoshana kwa rasilimali wanazopata wananchi na mambo mengine mengi yanamsukuma binadamu kukosa utu.

Wema na uovu kama sifa zinazotumiwa kupima thamani ya vitabu imeelezwa na (Thomas 2004). Anaeleza kuwa, suala kuu katika maisha ya mwanadamu ni wema na uovu ambao hutawala. Kadhalika, Thomas anasisitiza kuwa matendo ya wema lazima yajikite kwenye matukio na athari ya wema huo kuonekana kwa watu. Kwa vile wema ni sifa ya utu, maelezo haya yalinufaisha utafiti huu kwa kubainisha athari ya wema kutoka kwa viumbe wa kiuhalisiajabu wanapoonyesha utu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

Utu huhusishwa na wema. Mara nyingi, binadamu asiye na utu huwa mwovu, mwenye kutendea wengine maovu. Kulingana na Abraham (2005) kuna aina mbili za wema: Mtu binafsi atendaye mema na jamii itendayo mema kwa hiari au bila kupenda. Watu hutambua wema kwa kutumia vigezo vilivyowekwa kisheria, nao uovu hutambuliwa kwa kurejelea makataa ya sheria. Kwa kuwa sheria huongezeka mara kwa mara, watu hurejelea sheria hizo kuwaongoza katika shughuli za kimaadili. Kadhalika, Abraham anaeleza kuwa maadili ni mambo ya kawaida maishani ambayo hupatikana kwa kila mwanadamu anayeishi katika mahusiano ya kibinafsi, kijamii, nchini na hata kimataifa.

Wema na uovu ni kama pande mbili za sarafu moja. Awdhesh (2014) anasema kwamba ujuzi wa wema na uovu ndiyo ujuzi wa uhalisia. Anaendelea kuisitiza kwamba watu wenye hekima

wameelewa kuwa wema na uovu ni pande mbili za sarafu. Matendo hayo yanakaa tofauti mno, lakini yote hutendwa na mwanadamu. Mwanadamu anaweza kuwa mwema au muovu, hayo yatategemea uamuzi wake kuhusu maisha. Walimwengu mara nyingi hutarajia wenzao watende wema au uovu. Haya huonekana wazi hasa pale ambapo watu wema hulimbikiziwa sifa ilhali waovu wanakashifiwa. Mawazo haya yalisaidia utafiti huu kuweza kubainisha wahusika wema katika riwaya teule zilizoshughulikiwa.

Imani zetu za kidini hutuelekeza kuhusu utu, upendo na amani. Utu ni muhimu katika maisha ya binadamu. Mtu aliye na utu hujaribu kwanza kuelewa wenzake wenye shida na shida walizo nazo, kisha hujaribu kujitia katika hali yao ndiposa aweze kuwasaidia wenzake. Utu unaweza kuelezwa kuwa sifa ya ubinadamu ambayo inabainisha binadamu na viumbe wengine. Ila, kuwa binadamu haimanishi kuwa na utu. Ukitaka kuelewa kiwango cha utu wa mtu, tazama matendo yake kwa wenzake. Utu ni kuonyesha mapenzi ya dhati kwa kila kiumbe anayeishi humu duniani (“Humanity is The Only Religion Theology Essay” 2018). Ingawa viumbe wa kiuhalisiajabu hawana Imani, kazi hii itakuwa yenye manufaa kwa kuwa dhana ya utu itaweza kushughulikiwa katika viumbe wa kiuhalisiajabu.

Utu ni sifa muhimu kwa binadamu (Palmer, 1992). Hii ni kwa sababu kila mtu hutegemea mwenzake. Binadamu mwenye utu na upendo huwa tegemeo mzuri kwa mwenzake. Hupeana msaada pakihitajika. Watu wenye utu kila wakati huona kuwa ni wajibu wao kuwasaidia wenzao. Kadhalika, Fedor (1997) akichangia kuhusu sifa ya utu, anaeleza kuwa utu ni kuwa na upole na udhaifu, ingawa sasa binadamu hana utu kwa kuwa ana ubinafsi. Binadamu huweza kukataa kutoa msaada kwa wengine. Fedor anasisitiza kuwa duniani sasa kila mtu hujishughulisha tu na nafsi yake. Tofauti na maelezo ya Fedor, kazi hii itabainisha jinsi viumbe wa kiuhalisiajabu wanawajali na kuwashughulikia wengine.

Kwa mujibu wa Lamont (1997), watu wengi barani Afrika hawana maarifa kuhusu dhana utu kwa sababu ya kukosa kuhamasishwa kuhusu utu. Lamont anasema kuwa kutohamasishwa huku kumeendeleza tabia za kukosa utu baina ya watu. Vijana waafrika wanateta kuwa hakuna jinsi watakavyotakiwa kuendeleza utu na kina babu zao hawakuwafahamisha lolote kuhusu umuhimu wa utu. Tofauti na maoni ya Lamont, kazi hii itaweza kupitisha ujumbe wa uzuri wa utu na hivyo kuhamasisha wasomi kuhusu utu.

Imedhihirika kuwa binadamu hujihusisha kijamii sana kuliko kujihusisha mwenyewe katika mambo mengi. Hii inadhihirisha kwa nini vitu vingi katika tamaduni za watu waafrika zilifanywa kwa kuhusisha watu wengi katika jamii (Lutz, 2009). Lutz anaeleza kuwa Ubuntu unadhihirika tu kijamii kwa mtu kuhusiana na wenzake. Anaendelea kusema kuwa baadhi ya asasi katika Afrika ya sasa kama asasi ya elimu, viwanda mbalimbali vya kazi na hata serikali hawatimizi matakwa ya Ubuntu kwa kuwa wanataka tu kutumia binadamu wengine kwa manufaa yao. Mawazo haya ya Lutz yalisaidia kwa kiwango kikubwa kutambua jinsi Said A.Mohamed ameonyesha wahusika wengine wanaotumia wenzao kwa manufaa yao tu.

Mawasiliano yanasumbua binadamu wengine (Jackson, 2010). Anadokeza kuwa azma kuu ya Ubuntu ilikuwa kusaidia binadamu kuwasiliana na wenzake kupitia upendo, heshima na huruma kwa mwenzake. Jackson anasisitiza kuwa matukio mabaya yanayotendeka katika jamii sasa yanasababishwa na ukosefu wa mawasiliano bora.

Akieleza kuhusu dhana 'Ubuntu', Mokgoro (1997) anaeleza kuwa ni jazanda lililotumika kuonyesha uhusiano wa umoja wa watu hasa katika bara la Afrika. Mokgoro anasisitiza kuwa Ubuntu unaeleza kwa kina umoja wa kundi, ambapo kila mmoja kwenye kikundi anategemea mwenzake katika kikundi ili kuendeleza maisha yake. Anaendelea kusema kuwa Ubuntu ndio chanzo cha maadili mema katika jamii. Mokgoro (1997) anaendelea kutaja kuwa kwa sababu ya utandawazi, mabadiliko ya kiteknolojia, kuhama kwa watu kutoka jijini kuelekea mjini, kumesababisha kutoweka kwa Ubuntu, hii ni kwa sababu binadamu wa sasa wamepoteza mwelekeo kwa kukosa kuhamasishwa kuhusu kujijali na kuwajali wenzao. Hivyo, kizazi cha sasa kinapaswa kuhamasishwa na kukumbushwa kuhusu Ubuntu. Hivyo mwelekeo huu aliouchukua (Mokgoro, 1997) ulifaa utafiti huu kwa kuwa ilidhihirika wazi katika mojawapo ya riwaya teule za Said A.Mohamed jinsi wahusika walivyowategemea wengine kuendeleza maisha yao.

Athari ya kitu hufanyika iwapo mtu au kitu kimepokea tendo fulani. Binadamu akiwa amepokea tendo fulani huathirika kwa njia tofauti. Athari huweza kuwa chanya ama hasi. Hii hujitokeza kulingana na tendo alilopokea mtu au kitu. Tendo la utu linapojitokeza binadamu huwa na uwiano na watu wakaelewana, pia huleta furaha, mtu hupata nguvu, na hata kutoa shukrani.

Khoza (2014) na Tutu (2000) wanaeleza umuhimu wa utu. Khoza anaeleza kuwa utu ndio uti wa mgongo wa jamii za Kiafrika, hasa katika mahusiano yao katika jamii. Khoza anasisitiza kuwa utu umeleta umoja na maridhiano kati ya waafrika kwa kiasi kubwa na waafrika wanaoshirikiana na kupendana ni wengi kuliko wale ambao hawapatani. Khoza anadhihirisha kuwa kabla ya ukoloni wa waafrika, waafrika walikuwa wakisaidiana hasa kuwasaidia wale waliokosa vitu Fulani, kuwa mtu hangekuwa na mengi ilhali mwenzake amekosa. Tutu (2000) anaonyesha jinsi utu ulikuwa suala muhimu katika jamii ya waafrika. Anaeleza kuwa utu ulileta uhusiano mzuri baina ya watu katika jamii, kuwa kuna wale waliobarikiwa kupata mali nyingi na walikuwa na utu na kuweza kuwasaidia waliokosa. Khoza na Tutu wanalaumu wakoloni kuwa waliweza kuondoa umuhimu wa utu akilini mwa waafrika jinsi walivyowatesa, kuwanyanyasa na kuwadhulumu Waafrika. Kazi hii ilifaa kwa kuwa Said A. Mohamed alidhihirisha wahusika ambao walikuwa na utu wa aina hii.

Dhana Ubuntu ni neno la Kiafrika ambalo limehusishwa sana na neno utu kwa lugha ya Kiswahili. Gade (2011) anaeleza kuwa Ubuntu ina maanisha upendo, ukweli na uzuri wa ndani wa mtu yaani tabia. Kwanzia awali misingi ya Ubuntu imekuwa ikiongoza waafrika wanavyoishi na kutangamana. Mtu asiye na utu hujivisha sifa mbovu kama vile usherati, majivuno na ubinafsi. Panapo uhusiano mzuri watu hutangamana vizuri. Msimamo huu wa Gade umehusiana kwa kina na kazi hii ambayo inaeleza mambo ambayo hujitokeza mtu akipokea tendo la utu.

Kwa mujibu wa Venter (2004), Ubuntu huweza kusaidia kudumisha uhusiano uliopo baina ya walimu na wanafunzi. Venter anaendelea kusema kuwa tabia hii ya utu ni muhimu katika mazingira ya shule na maisha ya mwanafunzi mle shuleni. Ni tabia anayopaswa mwalimu kuikuza katika miaka yake ya kazi ya ufunzaji. Venter anaendelea kusema kuwa, uhusiano wa namna hii ikiwepo, hata matokeo ya wanafunzi huenda yakawa mazuri na kukuza uhusiano baina ya wanafunzi pia. Kupitia kazi hii, inadhihirika wazi pia kupitia kazi za Said A. Mohamed kuwa athari moja ya tendo la utu ni kujenga uhusiano baina ya watu.

Mtu anapokea matendo ya utu kutoka kwa wenzake, huleta uwiano kati yao. Msila (2015), anataja kuwa Ubuntu ni dhana ambayo tu inaweza kushirikishwa kwa umati wa watu na wala si kwa mtu binafsi. Msila, anasema kuwa, athari ya Ubuntu itajitokeza wazi wapokezi wakiwa wengi kuliko mtu mmoja. Anaendelea kusema kuwa, tendo hilo hupokelewa kwa matendo mahususi yenye uzuri wa kimo ya yaliyotendeka. Msila anasisitiza kuwa, jambo hili litaweza kusaidia hata kurehemu watu kutokana na tabia mbovu.

“Sisi ni watu tu kwa sababu ya wenzetu,” Haya ni mawazo ya (Tutu, 2004, uk. 44) kuhusu Ubuntu ambayo amehusisha na utu. Anaeleza kuwa kwa sababu hii, hata tunapozaliwa tukiwa wadogo, wazazi wetu huwa wapo kutulinda na kutuongoza. Kando na hao, pia kuna baadhi ya wanajamii ambao huwasaidia wazazi katika kulea watoto kmwili, kiakili na kwa nyanja zote zile. Kutokana na malezi haya, watoto hujitokeza wakiwa wakubwa na kuwasaidia wazazi wao. Wengi wao hujikaza kuwakimu wazazi wao. Maoni haya yanaafiki utafiti huu kwa kuwa viumbe wa kiuhalisiajabu walionekana kukumbushwa malezi mema ya wazazi yao

Kulingana na Mbigi (1995), familia yake, ilikuzwa kuelewa kuwa mtu aliye na utu anapaswa kuigwa. Hii ni kwa sababu huwa na heshima kwake mwenyewe na hata kwa wenzake. Anaendelea kuisitiza kuwa ukiwa unaweza kuwaona wenzako kama binadamu hutamfanyia lolote ambalo hapaswi kutendewa binadamu. Anaeleza kuwa athari kuu ya Ubuntu ni kujiona kwa wenzako. Maoni haya ya Mbigi yameafiki kazi hii kwa kuwa mwandishi Said A. Mohamed ametumia wahusika wengine kuiga wenzao.

Kulingana na Hailey (2008), dhana Ubuntu ni neno linalohusishwa na Waafrika. Anaeleza kuwa, Ubuntu ni neno linalohusishwa na utu wa binadamu kwa wenzake. Hailey anasisitiza kuwa, Ubuntu unapojitokeza kati ya watu kazini, ushirikiano hudhihirika. Anahimiza umuhimu wa watu kushirikiana kazini. Hivi, kazi huweza kufanyika vizuri bila tashwishi yoyote na kukuza jina la kampuni. Hailey pia anaendeleza kuwa sifa hii hujitokeza tu kwa binadamu na wala si wanyama. Hivi ukiwa binadamu aliyekosa Ubuntu basi una unyama, kwa kuwa umekosa hisia za utu kwa binadamu wenzako. Maoni ya Hailey yalifaa kazi hii kwa kuwa mwandishi ameonyesha ushirikiano wa wahusika kupitia viumbe wa kiajabu wanaowaonyesha utu.

Serikali ya Kenya sasa inawasaidia mayatima, walemavu, wazee na hata wafungwa. Wazee walio na umri wa miaka sabini na Zaidi wametengewa pesa za kujikimu ambazo wao hupata kila mwezi. Watoto mayatima na wasiojiweza wanapata usaidizi kupitia hela kutoka kwa taasisi kama vile HELB (Higher Education Loans Board) na CDF (Community Development Fund). Samkange na Samkange (1980), wanaeleza kuwa dunia imeimarika kwa kuwa hapo awali kikundi hiki cha watu hakikuwahi shughulikiwa. Matokeo ya utafiti huu wa Samkange yamefaa utafiti huu kwa kuwa inadhihirisha jinsi binadamu humtunza mwenzake. Utafiti huu nao umeshughulikia jinsi viumbe wa kiuhalisiajabu wanawatunza binadamu kwa njia mbalimbali. Vile vile, kupitia kitabu cha

Nyuso za mwanamke (2010), tunamwona Nana akiwa amelindwa na kutunzwa na aila yake hata kama mama yake hayupo.

2.4 Umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu

Umbo ni mkao au jinsi kitu kilivyotengenezwa au kilivyotengenezwa. Pia ni fomu ya kitu au mipaka yake ya nje au uso wake wa nje (TUKI, 2013). Kitu kile kilichotengenezwa huwa na umbo lake linaloweza kutambulika na kupewa jina maalum kwa mujibu wa lugha husika. Kimsingi, chochote kinachoundwa huwa na vipashio au vijenzi vyake vinavyosukwa kwa ustadi maalum. Maathalani umbo la mwili wa binadamu linaundwa na vijenzi kama vile kichwa, shingo, mikono, kiwiliwili na miguu (Alexander, 1990). Viumbe wa kiuhalisiajabu kama wanavyoitwa ni viumbe wenye sifa za kustaajibisha na kuogofya. Ni viumbe tofauti na binadamu halisi na wenye nguvu fulani. Kutokana na nguvu hizo, huweza kujibadilisha katika maumbo mbalimbali kama vile mawe, mizuka, kivuli, binadamu mwingine, wanyama mbalimbali na mengineo.

Dhana hii ya uumbaji wa wahusika hujitokeza hasa katika uhusika. Kwa sababu hii, mapitio ya uhusika yatasaidia kueleza kwa kina suala la umbo. Uhusika hutumiwa kuelezea mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake (Wamitila, 2003).

Kulingana na Miruka (1994), neno uhusika limetumika kumaanisha tofauti iliyoko katika mazungumzo ya watu, tabia, matendo na maingiliano yao na watu wengine. Ufafanuzi huu unaeleza uhusika kuwa kile kinachomfanya mtu mmoja kuwa tofauti na mwingine. Uumbaji wa wahusika katika riwaya teule za Said A. Mohamed zimesawiri tofauti kati ya wahusika kitabia.

Uhusika ni ile hali au sehemu inayochangiwa na wahusika katika kazi ya fasihi. Mchango huu unaweza kuonyeshwa kupitia kwa vitendo vyao, mazungumzo yao, mawazo yao au hata kwa malengo yao (Syambo, 1992). Huku ni kufinyanga tabia na sifa bainishi za watu na vitu kupitia wahusika na vihusika kibunifu. Wahusika na uhusika hutumiwa kwa lengo la kuonyesha ufaafu wakazi fulani ya fasihi.

Mbali na ufafanuzi wa uhusika uliotolewa na wataalamu mbalimbali, uhusika unaweza kumaanisha dhana dhahania zinazowasilishwa katika kazi za kidrama na za masimulizi. Dhana zilizo na sifa adimu na zinazoweza kuingiliana ama kuhusiana na mawazo au hoja kama ilivyo

kwa binadamu walio na maadili na sifa za kihisia zinazoweza kuonekana. Aidha lugha ya kifasihi huwezesha dhana zisizo na uhai kutekeleza haya (Samba, 2018). Kutokana na maelezo haya inaeleweka kuwa mhusika ni mshiriki katika kazi ya sanaa. Aidha uhusika ni sifa na thamani zinazoweza kuelekezwa kwa mshiriki kwa kuzingatia matendo, fikra na mazungumzo au yote kwa pamoja. Ieleweke kuwa mshiriki katika kazi ya sanaa si lazima awe binadamu bali vyombo vinaweza kutumiwa, mawazo na maswala kuwa viwakilishi vya binadamu. Hivi ni kusema kwamba tunahushia dhana zisizo za kibinadamu. Suala hili litafaa kwa kuwa katika riwaya hizi teule za Said A. Mohamed, ametumia wahusika viumbe pamoja na binadamu.

Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kuunda kazi yoyote ya kifasihi. Kipengele hiki hushirikiana na vipengele vingine vya kifani katika kutoa maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Kwa kawaida wahusika hujengwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii (Msokile, 1992). Mwandishi huwajenga wahusika wake kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuwatofautisha na hivyo kuiwezesha hadhira yake kutambua sifa au tabia za mhusika fulani zinazomtofautisha na mhusika mwingine katika kazi husika. Hata hivyo, ni vema ifahamike kuwa kila msanii wa kazi ya kifasihi ana mbinu zake za kuwajenga wahusika wake. Hii ina maana kuwa, msanii wa kazi ya kifasihi anaweza kutumia mbinu moja au zaidi katika kazi fulani kutegemeana na aina ya utanzu anaoushughulikia. Kwa kutambua hoja hiyo, maelezo haya yalisaidia utafiti huu kuelewa jinsi ya kusawiri sifa ya utu za wahusika katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

Neno wahusika linatokana na kazi ya Theophrastus; *The Characters*; katika karne ya tatu kabla ya Kristo, (Baldic, 197). Baldic akielezea kuhusu mhusika, katika fasihi anasema kuwa ni kiumbe wa hadithini aliyebuniwa na msanii ili kuendeleza hoja na maudhui yake katika kazi yake. Mhusika husaidia katika kuendeleza mada nzima anayoizingatia msanii hususan kwa kufululiza vitushi na visa mbalimbali katika kazi ya msanii ili kuwafikia wasomaji au wasikizi wake. Aghalabu, kila kazi ya fasihi huwa na mhusika au wahusika na huwa wamebuniwa na msanii ili kuchukua na anachotaka kukifafanua. Wamitila (2008) anatoa hoja kuwa wahusika ni watendaji wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi za kifasihi. Ni vielelezo vinavyowakilisha viumbe wanaopatikana ulimwenguni.

Uhusika katika riwaya teule zilizoongoza utafiti huu ulijengeka kutokana na hadithi za kawaida katika jamii zetu. Watunzi wanaosawiri wahusika kwa kutumia mbinu za kimazingaombwe wanafanya hivyo kwa kuiga mbinu za fasihi simulizi zilizokuwa zikitolewa na kusambazwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, kwa kusimuliwa ama kwa kupitia mazungumzo katika jamii. Ni simulizi ambayo wahusika kama vile majitu, mizimu na hata wanyama waliaminika kuwa walikuwa na uwezo wa kutangamana na wanadamu katika ulimwengu halisi. Utafiti huu ulichanganua sifa ya utu wa wahusika wa kimazingaombwe. Ulibainisha upekee wa kila mhusika kuonyesha sifa bainifu ya utu kiuhalisiajabu kama inavyojitokeza katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

Wahusika huwa nguzo kuu katika kuwasilisha mawazo ya mtunzi katika kazi za sanaa. Kijisehemu hiki kinawasilisha uhakiki wa maandishi kuhusu sifa za utu wa wahusika wa kiuhalisiajabu. Kuhusu usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe, Wamitila (2003) anasema kuwa umazingaombwe hutumiwa kuelezea jinsi wahusika wa kifasihi walivyosawiriwa au wanavyowasilishwa na msanii au mtunzi wa fasihi katika kazi fulani. Usawiri wa wahusika hufanywa kwa kuhusisha majina yao, maumbo yao, hisia zao, lugha wanazopewa na matumizi yao ya maneno na kwa kuwatambulisha kwa matendo yao wenyewe. Hivyo, utafiti huu ulisawiri wahusika kwa maumbo wanayodhihirisha wakati wanatenda matendo ya utu.

Akichanganua kuhusu usawiri wa wahusika, Wamitila (2008) anafafanua kuwa mwandishi anaweza kutumia njia kadhaa na tofauti katika kuwasawiri wahusika wake. Msanii ana uhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuiteua namna ya kuwawasilisha wenyewe. Wasomi na wahakiki wa fasihi, hutegemea sifa kadhaa kuwaelewa wahusika hao, zikiwemo sifa kama vile: maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao kwao na wengine, mazingira na mandhari yao, kiwango chao cha elimu na jamii yao. Wamitila, amebainisha na kuchambua mbinu mbalimbali za kuwasawiri wahusika kama zifuatazo:

Mbinu ya Kimaelezi: Mwandishi hutumia mbinu hii kuzieleza sifa za mhusika na mara nyingine kutoa picha ya maneno inayomweleza muhusika. Mwandishi anakuwa na nafasi ya kubainisha mapenzi au chuki yake dhidi ya wahusika fulani. Mbinu hii haimpi msomaji nafasi ya kushiriki

katika kutathimini tabia ya muhusika fulani. Analazimika kuukubali msimamo na kuridhika na maelezo ya mwandishi.

Pia, Wamitila (2010) anaeleza mbinu nyingine kama mbinu ya Kidrama: Mbinu hii ya ki-muhakati (ki -mimesia), kama ilivyo katika tamthilia, huonyesha wasifu wa muhusika wake. Pia mbinu hii inamwezesha msomaji au mhakiki kumjua na kumweleza mhusika bila ya kuathiriwa na mtazamo wa mwandishi au msimulizi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2010), mwandishi anaweza kutumia mbinu za usambamba na ulinganuzi katika kuwasawiri na kuwakuza wahusika wake. Ulinganuzi ni ulinganishi kwa kinyume. Kuwoko kwa mhusika ambaye ni kinyume cha mhusika fulani huweza kuwa ni moja wapo ya uhusika. Mwandishi anaweza pia kuwaweka wahusika au kuwaonyesha kwa namna ambazo ni sambamba na kwa njia hii humfanya msomaji au mhakiki aziwazie tofauti au mfanano wa sifa zao. Ulinganuzi sio tu mbinu ya kujenga uhusika bali pia hutumika katika usimulizi wa matukio na ukuzaji wa dhamira na maudhui. Wakati huo huo mwandishi anaweza kuwasawiri wahusika kwa namna ambavyo tabia zao zinaonesha kupingana kwa namna fulani, yaani tukimwagalia mhusika kwa makini tunahisi kuwa kuna kupingana kwa sifa fulani katika uhusika wake. Hapa tunasema kuwa ni mbinu Ki-nzani.

Wandishi huwajenga wahusika wao kwa njia mbalimbali ikiwemo; kimatendo, kimatamshi, kimazingira, kiuzungumzinafsiya, wanavyozungumza kati yao na kwa kutumia mbinu ya uwasilishaji dhahiri (Madumulla, 2009). Mbinu ya Kimatendo ni miongoni mwa mbinu ambazo msimulizi-mwandishi amezitumia katika kuwajenga wahusika wa simulizi yake. Kwa kawaida matendo ya mhusika yanaweza kuainishwa katika makundi matatu kama asemavyo Shen (2006) akitaja makundi hayo kuwa ni: tendo linalotendwa na mhusika “*act of commission*,” tendo ambalo mhusika anapaswa kulitenda lakini halitendi “*act of omission*,” na tendo ambalo halijafanikiwa ingawa mhusika amekusudia kulifanya “*contemplated act*.” Mbinu hii humfanya msimulizi atumie ufafanuzi kidogo huku msimuliwaji akipewa nafasi kubwa ya kutafsiri maana na sifa au tabia ya mhusika kutokana na matendo yake. Msokile (1992) anaeleza kuwa, “msanii huwaunda wahusika kwa kutoa matendo nusunusu, hatoi maelezo juu ya matendo yote kwa mara moja.” Mawazo haya ya kujenga mhusika kimatendo yatanufaisha sana utafiti huu kwa kuwa wahusika wa vitabu teule vya Said A. Mohamed wameainishwa kutokana na matendo yao ya utu.

Njia nyingine ya kuwajenga wahusika ni kupitia mbinu ya matamshi. Kwa mujibu wa Senkoro (1982) katika mbinu hii, msimulizi huwajenga wahusika kwa kuwafanya wazungumze ili lafudhi zao ziweze kuwabainisha. Kwa mfano, katika simulizi fulani msimulizi-mwandishi anaweza kumjenga mhusika wake kwa kumfanya azungumze kwa lafudhi ambayo ni tofauti na wahusika wengine ili kumtofautisha na wahusika wengine. Lafudhi itakayosikika kutoka kwa mhusika huyo huweza kusawiri usuli wake na kuibua dhamira fulani.

Mhusika pia huweza kujengwa kulingana na mazingira yake. Kimani (2003) anakariri kuwa maisha ya mwanafasihi na mazingira yake ya kihistoria, kisiasa, kijamii pamoja na hall za kiuchumi zina uhusiano mkubwa na uandishi wa kazi zake. Hivi ni kumaanisha kuwa mwandishi huathiriwa na tajriba zake za maisha, na hivyo wahusika wanaopatikana katika kazi yake ya kifasihi wanaweza kusawiriwa kulingana na mazingira na wanaweza pia kupatikana katika mazingira halisi anayoishi.

Ujenzi wa wahusika wakati mwingine hutegemea mbinu ya uzungumzinafsiya. Mbinu hii inafafanuliwa na Wamitila (2008) kuwa mtindo wa kuyawasilisha mawazo ya mhusika kwa mtindo au njia ya kujizungumzia. Anaendelea kueleza kuwa, katika uchunguzi wa dhana hii tunaweza kubainisha kati ya aina kuu mbili: uzungumzinafsiya wa moja kwa moja, na uzungumzi nafsiya usio wa moja kwa moja. Kutokana na maelezo hayo tunaweza kueleza kuwa, uzungumzinafsiya unahusu monolojia, yaani mhusika anajizungumzia peke yake. Kutokana na kujizungumzia huko, wasimuliwaji hupata fursa ya kufahamu kile kinachoendelea katika akili ya mhusika, kwa hivyo wasimuliwaji huweza kubaini sifa au tabia za mhusika huyo pamoja na maudhui yanayoibuliwa.

Wahusika pia huzungumza baina yao. Mbinu hii hutumika kwa kiasi kikubwa katika riwaya, ambapo msimulizi-mwandishi huwapambanisha wahusika ili wazungumze wao kwa wao. Msokile (1992), anaeleza kuwa kadiri wanavyoendelea kuzungumza, wazo la mhusika pamoja na tabia yake hujulikana taratibu katika kazi hiyo. Kadhalika, mwandishi huweza kumjenga mhusika kwa kutaja moja kwa moja na kwa uwazi sifa zake fulani katika matini husika. Hii ina maana kwamba sifa na matendo ya mhusika yanaelezwa waziwazi na msimulizi. Mbinu hii ya kuwaumba wahusika husaidia kumfanya msomaji asipate taabu katika kutambua wasifu wa ndani na wasifu wa nje wa mhusika. Pia, mbinu hii humsaidia msomaji kutambua kiini cha kisa, wazo au dhamira

(Msokile, 1992). Mbinu hii ya kujenga wahusika, ilinufaisha utafiti huu katika kubaini jinsi mwandishi Said A. Mohamed amewasawiri wahusika wake kwa njia ya moja kwa moja katika riwaya zake teule zilizotumika katika utafiti huu.

Wahusika wana umuhimu mkubwa katika kuiunda simulizi ya kifasihi. Hii inatokana na ukweli kuwa, wahusika huweza kuathiri simulizi inayosimuliwa, yaani wao ndio hupeleka mbele matukio katika simulizi. Wahusika wanaelezwa kuwa ni sehemu muhimu ya fani (Msokile, 1992; Njogu & Chimera, 1999) na kwamba, wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira na malengo ya msimulizi. Msokile na wenzake wanaeleza kuwa, wahusika hushabihiana na watu kwa kuwa fasihi huandikwa kwa ajili ya watu na kwa hiyo huwahusu watu hao. Kwa kawaida wahusika si watu halisi, bali ni matokeo ya ubunifu wa msanii ili kuakisi masuala kadhaa ya kijamii ambayo msanii ameyakusudia.

Suala la usawiri wa wahusika limezingatiwa na wahakiki mbalimbali wa kazi za fasihi. Njogu na Chimera (1999) wameshughulikia wahusika katika tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi, kwa kuainisha wahusika kama wanavyodhihirika katika fasihi. Wamezingatia aina mbalimbali za wahusika, sifa zao mazingira yao na umuhimu wao katika kazi husika.

Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kuunda kazi yoyote ya kifasihi. Kipengele hiki hushirikiana na vipengele vingine vya kifani katika kutoa maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Kwa kawaida wahusika hujengwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii (Msokile, 1992). Mwandishi huwajenga wahusika wake kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuwatofautisha na hivyo kuiwezesha hadhira yake kutambua sifa au tabia za mhusika fulani zinazomtofausha na mhusika mwingine katika kazi husika. Hata hivyo, ni vema ifahamike kuwa kila msanii wa kazi ya kifasihi ana mbinu zake za kuwajenga wahusika wake. Hii ina maana kuwa, msanii wa kazi ya kifasihi anaweza kutumia mbinu moja au zaidi katika kazi fulani kutegemeana na aina ya utanzu anaoushughulikia.

Uteuzi wa wahusika katika kazi yoyote ya fasihi huchangiwa na mambo kadhaa. Ntarangwi (2004), anasema kuwa waandishi wengi wa Kiswahili hujishughulisha na utunzi wa kazi za fasihi kufuatana na matatizo au ufunuo uliowafikia wakati huo, au kufuatana-na mkondo wa wakati na mabadiliko yake. Hivi ni kumaanisha kwamba mwandishi hutunga kwa kuongozwa na mambo

yanayotendeka katika jamii yake wakati wa utunzi au mabadiliko yanayoikumba jamii anayoishi. Changamoto zinazowakumba wanajamii kutokana na mabadiliko haya hudhihirishwa kupitia wahusika waliomo katika tungo za wakati huo. Mwandishi pia anaweza kutabiri mambo yatakayokuja baadaye na hivyo kuyaakisi kupitia wahusika wake. Ntarangwi (2004), aidha anaeleza kuwa usawiri bora wa wahusika huhitaji hali ya juu ya ubunifu ili kuwafanya wahusika hao wadhihirishe hali halisi zinazopatikana katika mazingira ya kawaida. Hill anasisitiza kuwa mtunzi huwa mfasiri wala si muumbaji kwani hujihusisha zaidi na udhihirishaji wa vivutio ambavyo tayari tunavifahamu, wala sio ufichuaji wa yale tusiyoazoea wala kuyaona. Hili linadhihirisha kuwa mtunzi hawateui wahusika wake kiholela bali huwatumia kuakisi hali ya mazingira kwa mujibu wa wakati. Mwandishi Said A. Mohamed aliweza kuwateua wahusika wake kwa kuakisi hali ya mazingira na wakati.

Wahusika wamehakikiwa katika fasihi kwa jumla. Mazrui na Syambo (1992) walihakiki kwa kina wahusika katika fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kushughulikia wahusika wa aina mbalimbali. Wahusika hawa ni kama vile; wahusika mkuu, wahusika wasaidizi, wahusika bapa, wahusika duara na wahusika wafoili. Aidha, Msokile (1992) amezingatia suala la wahusika kama mojawapo wa misingi ya uhakiki wa fasihi. Msokile amedokeza juu ya umuhimu wa kuzingatia aina kadha za wahusika katika uhakiki wa riwaya, tamthilia na mashairi. Kazi hii ilifaa utafiti huu kwa kuwa ilishughulikia wahusika katika uhakiki wa riwaya teule za Said A. Mohamed.

Ubunifu wa msanii humwezesha msanii kuwaumba au kuwasawiri wahusika kinafsia, kiakili, na kimwili. Usawiri wa wahusika unaofanywa na msanii hutegemea mbinu mbalimbali ambazo msanii huyo amezitumia. Madumulla (2009), anaeleza kuwa, mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi na ni kiini cha vitu vyote vipya, dhamira na mada katika fasihi. Madumulla anaendelea kueleza kuwa, katika mhusika kuna uwili: kwanza, kuna usawiri wa kisanaa wa mtu kwa upande mmoja; pili kuna sura ya mtu kwa upande mwingine. Hivyo, mawazo haya yalisaidia mtafiti kuweza kubaini njia mbalimbali mwandishi alivyowasawiri wahusika wake kimaumbile, kitabia na kwa njia zote.

Wahusika ni muhimu sana katika fasihi. Kupitia kwao mwandishi huweza kupitisha ujumbe aliokusudi kwa wasomaji. Wahusika huwa wa aina mbalimbali ikiwemo wahusika wa kiuhalisiajabu, wana umuhimu katika jamii yetu. Waandishi wengi ambao wameshughulikia

masuala ya uhalisiajabu wameweza kutumia wahusika kufanikisha hali hii katika kazi zao za fasihi. Hivyo basi, swala kuu hapa ni kwamba wataalamu hawa wanatudhihirishia kuwa wahusika ni nguzo muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Utafiti huu uliwashughulikia wahusika viumbe kwa lengo la kudhihirisha umuhimu wao katika udhihirishaji wa hisia za utu wa mwandishi. Aidha, imebainika kuwa uteuzi wa wahusika ulitegemea mazingira ya mtunzi ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Hii ni kwa sababu kazi ya fasihi haitoki katika ombwe tupu bali huyasawiri mazingira, matukio na hisia za msanii. Utafiti huu uliwashughulikia wahusika binadamu, wahusika wanyama na wahusika vitu kwa lengo la kudhihirisha umuhimu wao katika udhihirishaji wa hisia ya utu. Riwaya za kiuhalisiajabu zimevuka mpaka ya urazini kwa kusawiri wahusika ambao nafsi ,wasifu wao,tabia na hulka zao pamoja na kuakisi wasifu wa kibinadamu, huwa na wasifu wa kiajabu wa ziada. Ndio maana katika riwaya teule za Said A. Mohamed kuna usambamba wa wahusika mizuka, picha, ishara, jini na sauti wapo kwa wingi kuliko wahusika wa kawaida. Ili kufanikisha madhumuni ya utafiti huu ya jinsi viumbe wa kiuhalisiajabu wanavyosawiri utu, uhusika umetumiwa kama dhana ya kurejelea viumbe, vitu na hali. Hivyo basi utafiti umetumia virejelewa hivi kumaanisha wahusika kwa kuchunguza matendo au vitendo vyao dhidi ya viumbe au wahusika na namna wanavyoathirika kutokana na matendo ya viumbe hawa wa kiuhalisiajabu.

2.5 Hitimisho

Sura hii imehusisha mapitio ya maandishi yaliyofanywa kuhusu dhana ya uhalisiajabu, utu wa viumbe na uwasilishaji wa wahusika na uhusika. Utafiti huu unanuia kudhihirisha ya kuwa, ingawa viumbe wa ajabu wamehusishwa na maovu katika jamii, pia wana wema wanaoweza kutendea jamii.

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, data itakavyokusanywa, data itakavyochanganuliwa na hatimaye jinsi data itakavyowasilishwa. Riwaya teule zilisomwa kwa kina kwa misingi ya nadharia ya uhalisiajabu ili kupata mwanga na mihimili ya kufikia upeo wa kiuchanganuzi na wenye ithibati za kinadharia.

3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ambao ulihitaji kusoma riwaya teule kisha kuhakiki, kuchunguza na pia kutathmini ili kueleza utu wa viumbe wa uhalisiajabu katika riwaya za Said A. Mohamed kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Kulingana na King'ei (2002), utafiti wa kimaelezo hulenga kujua nini, lini, wapi na vipi na wala sio kwa nini. Utafiti wa kimaelezo ni utafiti ambao data hukusanywa bila kubadilisha mazingira kinyume na ilivyo katika utafiti wa kimajaribio. Muundo huu uliafiki utafiti kwa kuwa mazingira ya usomaji yalikuwa maktabani, vitabu teule vilivyochaguliwa vilikuwa riwaya tatu bila mabadiliko yoyote. Hatimye, malengo ya utafiti yalielezeka vema.

3.2 Wango la Utafiti

Wango la utafiti huu ni fasihi ya Kiswahili, utanzu wa riwaya. Utafiti huu uliangazia baadhi ya riwaya za kiuhalisiajabu 9 za Kiswahili kama vile mbili za K. Wamitila: *Bina- Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004), mbili za E. Kezilahabi: *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), Tatu za S. A. Mohamed: *Babu Alipofufuka* (2002), *Nyuso za Mwanamke* (2010) na *Dunia Yao* (2006) na mbili za T. Olali: *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* (2012) miongoni mwa zingine. Kati ya riwaya hizo, utafiti ulilenga riwaya teule za Said A. Mohamed ambazo ni: *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Riwaya hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa kuwa ziliwasilisha vizuri suala la utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu. Aidha mwandishi naye ameshughulikia suala la wahusika wa kiuhalisiajabu kiwakati baina ya miaka ya (2001-2010). Vilevile ilidhihirika kuwa kati ya waandishi hawa wa Kiswahili wa Kiuhalisiajabu, alikuwa na riwaya tatu wenzake wakiwa na mbili mbili.

3.3 Sampuli na Usampulishaji

Mohamed ameandika vitabu vingi vikiwemo riwaya, tamthilia na ushairi. Riwaya zake ni kama vile: *Kiza Katika Nuru (1988)*, *Asali Chungu (1977)*, *Utengano (1980)*, *Dunia Mti mkavu (1980)*, *Tata za Asumini (1990)*, *Kiu (1972)*, *Nyota ya Rehema (1976)*, *Kivuli kinaishi (1990)*, *Amezidi (1995)*, *Sadiki ukipenda (2002)*, *Mhanga Nafsi Yangu (2012)* na *Makadume (2013)*. Kazi zake za Ushairi ni kama vile: *Sikate Tamaa (1980)*, *Kina Cha Maisha (1984)* na *Jicho la Ndani (2002)*. Ameandika tamthilia kama vile: *Pungwa (1988)*, *Posa za Bi. Kisiwa (2007)*, *Kitumbua Kimeingia Mchanga (2004)*, na *Mashetani Wamerudi (2013)*. Pia, ana mikusanyiko nyingi ya fasihi simulizi kama vile, *Vito vya Hekima, Gharama ya Amani (2014)* *Semi na Maneno ya Mshangao (1974)* na *Semi, milio* na *Tashbihi (1981)*. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumika kuteua mwandishi pamoja na vitabu vyake. Mbinu hii ilitumika kuteua riwaya hizi teule za mwandishi Said A. Mohamed kwa kuwa, kati ya waandishi ambao wameendeleza maudhui ya utu, Said A. Mohamed ameendeleza maudhui ya utu kupitia viumbe ambao si binadamu ambao kwa kawaida huwa hawadhahirisha utu. Mbinu hii ya usampulishaji pia ilitumika kuteua riwaya kwa kuwa uhusika hujidhahirisha wazi kwenye riwaya. Sampuli ya kimakusudi ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa. Hivyo riwaya za Said A. Mohamed zilizoteuliwa ni; *Babu Alipofufuka (2001)*, *Nyuso za Mwanamke (2010)* na *Dunia Yao (2006)*.

3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data zilikusanywa maktabani kwa kudurusu na kuchanganuliwa kwa riwaya tatu za Said A. Mohamed; *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)*. Usomaji wa kina ulifanywa kwa majarida na machapisho yalioandikwa kuhusiana na mada ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu. Aidha, palikuwepo na usomaji wa vitabu vya wataalamu mbalimbali vinavyotaja mambo ya utu ili kupata uelewa zaidi kuhusu dhana hiyo. Tasnifu zilizohusiana na mada ya utafiti pia zilipitiwa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti katika ukusanyaji wa data. Majarida mbalimbali zilizopo katika mtandao na wavuti pia zilitumika ili kupata data faafu. Kwa kutumia mbinu hizi, mtafiti aliweza kubainisha vipengele mbalimbali

vya utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu. Data faafu zilidondolewa kutoka kwenye machapisho na maandiko haya na kunakiliwa kwa kurejelea malengo ya utafiti.

3.5 Uchanganuzi na Uwasilishaji Data

Uchanganuzi ulilenga utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu. Data iliyokusanywa ilinukuliwa, ikapangwa na kisha kuchanganuliwa ili kuafiki malengo ya utafiti. Mtafiti alichanganua umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu wanapodhihirisha utu, jinsi wanavyodhihirisha utu na athari ya utu wa viumbe hawa kwa binadamu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)* katika mkabala wa nadharia ya Uhalisiajabu. Mifano mbalimbali ilitumiwa katika riwaya teule za Said A. Mohamed ilitumiwa kudhihirisha matumizi ya uhalisiajabu kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia. Nadharia iliweza kueleza hali mbalimbali yaliyowezesha kuafiki malengo ya utafiti. Matukio ya utu yalisawiriwa na kuelezwa bayana kwa kufuata hatua zifuatazo, kudondoa sehemu matukio ya utu yamesawiriwa, kuonyesha umbo wanalochukua wahusika viumbe wakionyesha utu na kuonyesha athari ya utu kwa wahusika binadamu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)*. Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo na maandishi. Pia, mifano yenye kunukuu sehemu za riwaya ya kubainisha ujumbe husika ilitolewa baada ya usomaji wa kina, kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu iliyoongoza utafiti huu.

3.6 Utegemezi na Uaminifu katika Data

Utafiti huu ulizingatia uthibitishwaji data ili kupata data za utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Usomaji ulifanywa kwa vitabu kadha vya uandishi wa kiuhalisiajabu. Lengo kuu lilikuwa kukusanya data mapema ili kubaini ufaafu wa riwaya zilizoteuliwa kabla ya utafiti mkuu kufanywa. Usomaji awali ulifanywa kwa kutumia riwaya za kiuhalisiajabu. Mtafiti aliwashirikisha watafiti wenye ujuzi na tajriba katika Kiswahili ili kufanya marekebisho yanayostahili. Pia kulikuwepo na urudiaji na upekuzi wa data maktabani kwa kuzingatia malengo na nadharia ya utafiti ambapo vyanzo vya data zilizorekodiwa vilionyeshwa kwa kutaja maandishi na mwaka wa uchapishaji palipohitajika. Matokeo yalisaidia kuchaguliwa kwa riwaya teule za Said A. Mohamed.

3.7 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu, ulizingatia maadili ya utafiti kabla na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti huu ni wa maktabani mtafiti alihakikisha kuwa madondoo kutoka riwaya teule yalidondolewa kwa usahihi na kutumika tu katika kazi hii na si nyingineyo. Mtafiti alipata idhini kutoka Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia na kumpa kibali cha kuweza kukusanya data kutoka katika maktaba mbalimbali.

3.8 Hitimisho

Sehemu hii ya mbinu za utafiti imeweza kushughulikia, muundo wa data ambao ulikuwa muundo wa kimaelezo, wango la utafiti ambao ulionyesha riwaya zilizoteuliwa, sampuli na usampulishaji ambapo mbinu ya kimakusudi ilitumika kuteua riwaya teule za Said A. Mohamed, mbinu za ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake. Katika ukusanyaji, imetambulika kuwa utafiti huu ulikuwa wa maktaba na hivyo maktaba ya vyuo mbali mbalimbali zilitumika, kisha kusomwa na kuchanganuliwa. Katika sehemu hii pia, mwandishi alihakikisha amewasilisha data yenye uaminifu na hata kuhakikisha amepewa kibali na idhini mbalimbali kufanikisha utafiti. Haya yaliongozwa na madhumuni ya utafiti. Uchanganuzi wa deta ulijumuisha kuteua maudhui yaliyo na uhusiano na utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu. Mbinu zilizotumika zilitathminiwa na kisha kufasiri yaliyomo kwenye mbinu hizo. Hivyo, mifano michache ikaonyeshwa kuthibitisha uwasilisho wa utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika sura inayofuata.

SURA YA NNE: UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha, inachanganua na kujadili data kwa kuzingatia umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu wanapoonyesha utu, jinsi wanavyonyesha utu na athari ya utu wao kwa wahusika binadamu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Uchanganuzi wa data ulifanikishwa kwa vipengele vya nadharia ya Uhalisiajabu kama vile: usawiri wa matukio yasiyoaminika na ya kifantasia, matumizi ya ndoto kufanikisha uhalisiajabu, kutofuatana kwa matukio kimaantiki, matumizi ya mazingira kufanikisha uhalisiajabu na mambo ya kiuhalisiajabu kuonekana kuwa ya kawaida. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa katika sehemu tatu kuu ambazo ni: udhihirishaji wa umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu, udhihirishaji wa utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu na athari za utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa wahusika binadamu. Hatimaye, hitimisho la sura limehusishwa.

4.1 Umbo La Viumbe wa Kiuhalisiajabu

Umbo ni mkao au jinsi kitu kilivyotengenezwa au kilivyotengenezwa. Pia ni fomu ya kitu au mipaka yake ya nje au uso wake wa nje (TUKI, 2013). Kitu kile kilichotengenezwa huwa na umbo lake linaloweza kutambulika na kupewa jina maalum kwa mujibu wa lugha husika. Kimsingi, chochote kinachoundwa huwa na vipashio au vijenzi vyake vinavyosukwa kwa ustadi maalum. Maathalani umbo la mwili wa binadamu linaundwa na vijenzi kama vile kichwa, shingo, mikono, kiwiliwili na miguu (Crystal, 1987). Viumbe wa kiuhalisiajabu kama wanavyoitwa ni viumbe wenye sifa za kushangaza na kuogofya. Ni viumbe tofauti na binadamu halisi na wenye nguvu fulani. Kutokana na nguvu hizo, huweza kujibadilisha katika maumbo mbalimbali. Maumbo yanayodhihirika ni kama vile mzuka, jini, ishara na binadamu,

Mojawapo wa mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu inaeleza kuwa; mazingira ni sehemu muhimu katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu (Zamora & Wendy, 1995). Kupitia usaidizi wa mhimili huu, utafiti huu

umebaini jinsi mwandishi Said A. Mohamed ametumia mazingira ya kiajabu kudhihirisha maumbo mbalimbali yanayochukuliwa na viumbe wa kiuhalisiajabu.

4.1.1 Mzuka

Mzuka huhusishwa haswa na mwili wa mfu unaojitokeza kwa walio hai (TUKI, 2013). Kutokana na uchanganuzi wake wa vigezo vya uhalisiajabu katika riwaya za Toni Morrison Zenisek, Vutagwa (2013) anaeleza kuwa vigezo hivyo vya uhalisiajabu ni kama vile: kufufuka kwa wafu au kuwa katika hali ya mzimu au mzuka, pili uwezo wa kuponesha kimazingaombwe na tatu msaada wa kiungu.

Kwa mujibu wa Vutagwa (2013), mzuka ni mhusika wa kutathmini, ana mawazo, ujuzi, utambuzi, hekima na uwezo wa kuhisi mambo haraka. Ana ukarimu na huwa tayari kusaidia kila wakati. Sifa zake za "kiroho" zinadhahirishwa na mambo haya yote. Huyu mzuka ana uwezo wa kuonyesha jambo la asili linalotatanisha. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka (2001)*, mwandishi amemuumba mhusika na kumpachika jina la Mzuka kutokana na sababu kwamba ni mfu aliyefufuka. Ni mzuka. Mzuka ni marehemu Babu yake K, hivi, K ni mjukuu wake. Mzuka anajitokeza mara kwa mara kwa K. Mzuka anazungumza akisema:

N'amwona lakini hanioni... Kuna pingamizi bila shaka. K haamini ufufuzi wangu ela ule wa Yesu. Sijui kwa nini amekuwa hivi siku hizi! Zamani sote tulihamini juu ya ufufuzi wa wahenga...kwamba hatupotei tunapita tu, kutoka ng'ambo moja kwenda nyingine; dunia ya kuwepo katika ombwe na ububu (Uk 1).

Babu Mzuka anaamini falsafa ya ufufuzi kwani wakati wao waliwaona hata wafu na vivuli vyao katika ndotomacho. Walisema na mizimu na mizuka, kuomba msamaha kwa makosa yao na roho ya mfu kufufuka haikuwa uchawi wa aina yoyote. Anachoamini ni kinyume na kile K anachokiamini. K anaamini kuwa aliyekufa hafufuki na sio vibaya kujitenga na mfu.

Kutokana na maelezo haya, msimulizi ni mfu, alikufa ila kwa sasa amefufuka tena na yuko ulimwenguni. La kushangaza ni kuwa, haonekani na K anayetarajiwa kumwona. Hili linajitokeza kwa kuwa K haamini ya kwamba mtu huweza kufufuka akarudi duniani. Mzuka ni mhusika wa kiajabu sana na mtunzi anatumia fikra zake pamoja na za K kudhihirisha jinsi mtunzi ana uwezo wa kutawala fikra za wahusika. Mtunzi kwa kutumia utunzi huu wa kiajabu, anadhahirisha uwezo wa binadamu wa kuwaza katika uhalisia na katika ndoto. Mzuka ana uwezo wa kujibadilisha

kiajabuajabu, mara anageuka na kuwa moshi au mvuke, mara sura ya fuvu, mara anakuwa sauti ya chura au sauti ya mfu, pia anageuka na kuwa mchwa, maitikwenenda na vile vile kuwa binadamu halisi.

Vile vile, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), Mzuka anajitokeza kwa K tena. Mara hii anajitokeza katika sura ya fuvu. K anazungumza na kile kiumbe, anasema:

Mimi babu yako! Sauti nene, la tutu na mwangi.
Sikiliza...usinizonge kwa mazingaombwe mimi. Aliyekufa hafufuki; babu yangu au nani!
Kama wewe babu yangu, ulikufa zamani...
Aliyekufa anaweza kufufuka K. Hasa hapa petu! Hapa penye maisha ya uhenga, maisha ya kufa na kufufuka!” Kauli hiyo ilimshutua sana K. Kauli na sauti lenyewe. Maramoja alihisi kama sauti lile alilitambua. Aliisikia sana alipokuwa mdogo. Lakini ngoja kwanza-haiwezi kuwa! Aliyekufa hawezi fufuka.
Itakuwaje? Aliemewa
Sikiliza K... aliendelea yule mtumaiti. Mimi babu yako; na hii ni kweli. Ukitaka usitake. Nimefufuka kitambo ...au tuseme roho zetu zimo katika duru ya wakati wa daima usiomalizika. Ndiyo kusema hatukufa. Hatufi, wala hatutakufa. Hupotea kwenye macho yen utu (Uk 20).

K yupo kwenye gari akiendeshwa na dereva wake Mzula, ghafla panatokea tukio fulani ambalo hata yeye haelewi. K anaona dirisha lake la nyuma ya gari likifunguka, anashangaa na kutaka kumpigia kelele Mzula kwa kosa, linalofuata ni kuwa anaona sura nyingine. Kile kichogo alichokuwa akitazama K hakikuwa kichogo kamwe, bali kitu chenye sura ya fuvu. Tuseme nyuma fuvu na mbele mgandamo wa nyama. Na ngozi yake imekunyaakunya, na mwili wake upongo kamili. K hakuamini.

Mzuka bado anamzuru K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2010), anamjia K kwa umbo abacho halieleweki. Mwandishi anaeleza kuwa:

Mzuka alikuja kumzuru hangeweza kumzuia. Na safari hii alikuja kuketi mbele yake. Alikuwa vilevile: moshimoshi tu; uso wa bango, mfuto; si wa mdomo wala pua, si wa miguu wala mikono- mzuka! (Uk 69).

Mzuka anamzuru K afisini mwake. K anahisi kiwiliwili chake kinaregea na hali ya usingizi mzito unamkwea. Siku hizi anatambua hali hiyo vizuri na kujua maana yake nini. Ilikuwa ishara kuwa yule mzuka alikuja kumzuru. Katika mazingira hayo ya ofisini, makuu yanamtokea K, hajielewi, jambo hili linadhihirisha wazi mojawapo ya mhimili wa mazingira ya uhalisiajabu inayohusu

taswira. Pale ofisini matukio ya kiajabuajabu yanamtokea. Tukio hili linapeana taswira halisi ya uhalisiajabu ambapo mhusika anatoka katika ulimwengu halisi hadi ulimwengu wa kiajabuajabu kupitia fantasia.

Kutokana na mazungumzo haya ya babu na K, inabainika kuwa babu ni mfu, na mzuka wake unamtokezea K.

K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), Mzuka ni sauti ya mtunzi ambaye anajaribu kumulika athari za utandawazi katika uchumi, athari ya mienendo mipya ya kuiga chochote kutoka Ulaya na kusahau utamaduni wa jamii. Anawashawishi Waafrika wajikubali walivyo badala ya kuiga watu wengine. Anawaonya dhidi ya ubinafsi, uchoyo, ufisadi na uchu wa kutaka kukwea juu wafike kiwango cha marafiki wao kutoka Ulaya bila kuwajali waafrika wenzao.

Mambo ya kiuhalisiajabu huonekana kuwa vitu vya kawaida. Matokeo haya ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya (Zamora & Wendy, 1995). Mwandishi amewatumia viumbe wa kihalisiajabu ambao wanajitokeza kwa maumbo mbalimbali yasiyoweza kupewa jina mahususi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), tunamwona Bi Mkubwa, marehemu mamake Nana anajitokeza kwa sura mbili ya kienyeji na ya kigeni. Sura ya kigeni na ya kienyeji si sura bainifu inayoweza kuelezewa mtu hadi akaelewa. Kwa kawaida sura ya kienyeji ni sura ya kitu au mtu ambaye umezoea kumwona ilhali sura ya kigeni itakuwa sura ya kitu au mtu unayekutana naye kwa mara ya kwanza. Hili linadhihirika katika riwaya;

Mamake anamjia kwa njia mbili: kwa sura ya kienyeji na sura ya kigeni. Majilio ya sura ya kienyeji yalikuwa majilio mema; yenye murua, huruma, nasaba na ucheshi (Uk 284).

Nana akiwa ameganda kitandani kwa uchovu na mawazo. Walio kando yake mle nyumbani wanadhani kuwa ni mgonjwa mahututi na anakaribia masaa yake ya mwisho ya kufa. Baada ya marehemu mamake kutoka mle chumbani, Nana anaamka akiwa mwenye nguvu zaidi. Kule kumwona marehemu mamake kunamchawiza nguvu na anainuka. Hili si jambo la kawaida ingawa litachukuliwa kuwa la kawaida kwa kuwa aghalabu mtu hujikuta myonge na baada ya muda hupata nguvu. Kuwepo kwa marehemu mamake Nana ni ishara ya nguvu. Amekuja kumpa nguvu mwanaye. Nguvu ya mwilini hutoka kwa sababu ya viini na virutubishi tupatazo kutoka kwa

vyakula tofauti tofauti ila hapa inaonekana ikitoka kwa mzuka wa mama. Kutokana na fasihi simulizi za jamii ya Wakikuyu na zinginezo, mizimu huwatokea walio hai hasa ndotoni ili kujaribu kuelekeza jamii inapokosa mwelekeo (Olali, 2010). Nana amekata tamaa maishani na hivyo mzimu wa mamake upo pale kumwelekeza asikate tamaa.

4.1.2 Kivuli

Viumbe wa kihalisiajabu vilevile huchukua umbo la Kivuli. Mwandishi Said A. Mohamed anatomia kivuli kama mhusika wa kihalisiajabu kupitisha ujumbe wake. Hali hii hutokea kwa kuwa sifa mojawapo ya kihalisiajabu ni matumizi ya viumbe wasouhai kama wahusika. Husaidia kujenga mazingira ya uhalisiajabu (Zamora, 1995). Kwa kawaida kivuli hujitokeza tu kando ya chombo au mtu haswa panapo mwanga.

Ni kinaya kuwa Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi anaelezea kuwa wazungumzaji wake wote hai aliwapoteza na anazungumza na vivuli vyao. Anasema:

.... Unafanyaje unapokosa kuzungumza na mtu mwingine ila nafsi yako mwenyewe tu? Lazima niseme na kivuli changu na kivuli change kiseme na vivuli vingine. Viumbe pekee vilivyobaki kuzungumza navyo na kuvielewa kama vinavyonielewa. Viumbe ninavyoviweka kichwani na kisha kuja kuvisimamisha karatasini! Nahisi lazima nizungumze navyo kama nataka kubaki. Kubaki sio kuishi tena! (Uk 3).

Ndi anasema kuwa yeye husema na kivuli chake na vivuli vya wengine. Hii ni kwa sababu amepagazwa na ugonjwa wa wendawazimu. Kila mtu anadhani yeye ni mwendawazimu. Hivyo akiwa katika hali hii, hubakia kuzungumza na nafsi yake mwenyewe na vivuli vya viumbe wengine. Ndi anaeleza kuwa anapotembea hukutana tu na vivuli vya watu. Kulingana naye, maisha yamemgeukia ndoto. Ndoto katika kweli. Ndi anahisi kuwa yeye anaishi tu ndotoni, haelewi iwapo anaishi katika dunia halisi au dunia ya ndoto. Dhana hii inaafikiana na mhimili mojawapo wa nadharia ya uhalisiajabu inayoongoza utafiti huu unaoeleza kuwa, ndoto huchukua nafasi muhimu sana kwani matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni (King'ei 2022). Vile vile Ndi anasema katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006) kuwa, kule kuona kwake kwa kivuli kinamkalia ni kama yupo ndotoni. Anaeleza kuwa;

Baada ya taaluma. Tulikuwa peke yetu. Mimi na Shaib. Ndiye pekee niliyeweza kuzungumza naye hapa. Kivuli chake nakusudia. Siku hizi sisemi na mtu ila kivuli cha Shaib. Ye-, yaani Shaib, huzungumza nami ingawa simwoni. Alikuwa ameshakufa – kwa namna halisi ya kufa. Lakini bado alikuwa na uwezo wa kuniingia na kunining'inia kichwani. Niliweza kumhisi ndani ya nafsi yangu wakati wowote. Lakini zaidi nilipokaa kwenye baraza hii ya taaluma (Uk 40).

Mzuka wa Shaib unajitokeza kwake Ndi kama kivuli. Anaeleza kuwa siku hizi huzungumza tu na kivuli chake Shaib. Mara kwa mara huwa hamwoni. Shaib alikuwa mfu ila bado alikuwa na uwezo wa kumuingia akilini Ndi kila alipokuwa ameketi kwenye baraza ya taaluma.

Vilevile, Nana, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), naye anakiona kivuli cha marehemu mamake. Kivuli cha marehemu mamake kilimtokea na kwa nyakati hizo kilikuja kumtahadharisha, kumliwaza, kumwonya au kumwelekeza kufanya kitu fulani. Inabainika kuwa;

N'najua hujenda moja kwa moja. Kabla ya kuingia msalani usiku, huona mlango unafunguliwa. Ndipo tena hukifuma kivuli chako, haraka kinatoka msalani na kisha kinatoweka ombweni (Uk 18).

Nana ambaye amekuwa bila kumwona mamake mzazi, ana hisi kuwa yupo japo anaambiwa hayupo alienda safari is'o marejeo, yaani aliaga dunia. Nana ameishi na babake na mamake wa kambo. Anahisi mamake mzazi yupo kwa kuwa humwona kwa ishara ya kivuli. Hali kadhalika, Nana bado anaendelea kuuona kivuli cha mamake kwa wakati tofauti. Anasema kuwa;

Katika upeo huu nilishutukia wasifu wa mamangu umekuja kunisimamia mbele ya macho yangu. Kisha kivuli chake hai kikaketi juu ya kiti cha enzi. Kavaa gauni jeupe pana la arusi. Na taji la maua kichwani. Muda si muda, akaanza kunipigia makofi, na mara watu wakayapokea makofi kwa mizani ya kichawi. Uwanja mzima ukanguruma makofi kabla hata sijaanza kuimba. Hatimaye nikafumbua mdomo. Nikaanza kuimba wimbo nilioutunga mimi mwenyewe huku nikiikogesha furaha yangu machozi (Uk 54).

Siku ya sherehe ya Nana, sherehe yake ya kufaulu daraja la juu ya masomo na sherehe ya kuvunja ungo na kuwa mtu mkubwa, kivuli cha mamake kinamtokea. Nana amemwalika mpiga gita kwenye sherehe. Nana anapenda sana muziki. Ana imani kuwa kwa wakati mmoja atakuja kuwa mwana taarabu aliyezinduka. Atakayesimama kidete kuwatetea wanawake katika uga wa taarabu. Anapata motisha kutoka kwa mpiga gita aliyekutana naye njiani enzi zake za kuenda shuleni. Alikutana naye baada ya babake kumpa uhuru wa kutoka shuleni bila kuja kuchukuliwa kwa gari na dereva. Sherehe inakaribia kuanza. Mpiga gita anamwambia Nana yuko tayari. Nana anapiga

gilasi na kila mtu anamtazama. Mpiga gita anampa motisha ya kuimba wimbo wake wa kwanza maishani. Anapojitayarisha kuandama sauti ya gita kwa wimbo, wasifu wa mamake unajitokeza mbele yake. Kisha anaona kivuli chake kikiketi kitini. Akaanza kumpigia makofi na mara watu wote uwanjani wakayapokea makofi na hatimaye akaanza kuimba.

Nana anakuwa na uwezo wa kuupembua ukweli wa nyumba ile aliyoishi. Ukweli ambao kwao binadamu wa kawaida hawezi jua. Ni mmojawapo aliyeweza kuupembua ukweli kwenye ndoto, ila ndoto hauna ukweli na ukweli hauna ndoto. Waliokuwepo pale wakadhani kuwa aliambukizwa na kivuli cha mamake.

4.1.3 Binadamu Halisi wenye Uwezo wa Kiungu-Utu

Katika riwaya teule, mtunzi ametumia usawiri mseto kuwabuni wahusika wake ambapo amechanganya wahusika halisi kama wanavyoweza kumithilishwa na vitendo vya ulimwengu razini. Kuna wahusika wanaosawiriwa kuwili- kama binadamu razini na kama binadamu mwenye uwezo wa kiungu ungu- yaani wale wahusika wa kimazingaombwe au kifantasia. Mtunzi anafanya hivi kujenga mtagusano wa maingiliano ya ulimwengu wa kihalisia na ulimwengu wa kiuhalisiajabu, ulimwengu wa kufikiria na ulio katika upeo wa uwezekano. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), mwandishi anawatumia wahusika binadamu lakini walio na uwezo wa kiungu-ungu. kama inavyoshadidiwa na madondoo yafuatayo:

Picha ya Bi. M inanyanyuka kutoka kwenye albamu (Uk 21).

Bi. M ni mkewe Ndi. Ndi hana uhakika ikiwa aliona picha ikinyanyuka au ni mwili wa Bi. M Hajui kama ni kuota anaota au ni fikira tu kutokana na athari ya video vya kutazamwa. Kisha tena anajihakikishia kuwa ni dhahiri amemwona Bi. M akinyanyuka akaemewa. Bi. M anapotoka pale Ndi anamwona akitenda kitendo chake cha kawaida. Alikuwa na tabia ya kugonga mlango kwa nguvu, na alipohisi kuwa amechoka, alitishia Ndi kuwa angeita polisi au majirani iwapo mlango haungefunguliwa. Ndi anamwona Bi. M akiwa amenyanyuka kutoka kwenye albamu ila tena anaona akitenda matendo yake halisi aliyotenda kama binadamu wa kawaida. Vile vile tunamwona mtu wa pili, Yungi, akinyanyuka kutoka kwenye albamu. Mwandishi anaeleza kuwa:

Yungi naye pia anainuka kutoka katilka lile albamu alimotoka mamake (Uk 23).

Yungi ni mwanawe Ndi. Sasa Yungi aliinuka katika lile albamu. Bi. M akawa amesimama vilevile. Ndi alimtarajia Bi. M aende kulala ila hakwenda kulala. Yungi naye alikwenda kulala kule kwenye bapa la albamu. Ndi katika maisha yake halisi alikuwa akifunguliwa mlango na Yungi wake hata alipoingia nyumbani usiku wa manane. Ndi anashangaa kuwa Yungi aliyemwona akienda kulala tene sasa anaambiwa kuwa hayupo. Yungi alitoka alfajiri na mapema kwenda katika harakati za kutafuta mihela kwa kuwa aliona babake sasa hawezani na majukumu yale. Ndi babake Yungi naye anachukua fursa ya kumsubiri hadi wakati atakapokuwa amerudi nyumbani. Yungi kama binadamu halisi ameingia katika biashara ya ukahaba. Kila uchao hurejeshwa nyumbani kwa mabarubaru tofauti wenye magari. Yungi anapoingia nyumbani anaanza kubishana na babake kuwa dunia imwbadilika na kuwa sasa vijana wamechukua usukani wa kuwaongoza wanaume. Yungi ananyanyuka kutoka kwenye albamu. Ima tunashuhudia akiingilia masuala yaliyokosa maadili katika jamii. Yungi anaonekana kupenda kupigana na wenzake na kukosa kuishi nao kwa amani.

Yungi aliganduka pale alipokuwa kaganda, akajitupa juu ya albamu na kulala. Njiani, alipishana na kupigana kumbo na Bori. Ghafila, nilimwona Bori, kabeba mredio mbovu ambao sijui kauokota wapi ... Bori aliruka na hakurejea kulala kwenye albamu (Uk 115).

Yungi na Bori ni wanawe Ndi na Bi. M. Yungi na Bori pia wanatoka kwenye albamu. Yungi alitoka kwanza. Alipokuwa akirudi kulala kwenye albamu, alipishana na Bori. Bori anatembea sokoni kote na kila mahali akirokota mali. Alikuwa akitembea akisema kuwa “Naitwa Babu Rokotea.” Bori alionekana kwa b Bori pia anapomaliza mazungumzo na babake, anarudi kulala kwenye albamu.

Dubwa naye anaonekana akinyanyuka kutoka kwenye albamu. Linadhihirika wazi kuwa;

Albamu li wazi. Dubwa anaibuka na kutoka nje ya karatasi. Ajabu! Miaka yote hii picha yake ilikuwa imefichama kwenye albamu. Leo imezuka na kusimama kwa mapana na marefu. Imezingia dunia nzima! (Uk 139).

Dubwa pia ni mtoto wa Bi. M na Ndi. Dubwa, kifungua mimba wao, anaibuka na kutoka nje ya albamu. Picha yake ilikuwa imejificha kwenye albamu. Babake anashangaa ni vipi ameipata picha ile. Dubwa yuko pale kumswalisha babake. Anamtia makosani kwa kusema kuwa babake Ndi ameitenga nafsi yake na hivyo anapaswa kutubu kwa Mwenyezi Mungu. Aidha, Dubwa anamlaumu babake kwa kuwatenga watoto wake. Anaendelea kumwelekezea Ndi babake lawama

kuwa amejipandikizia wendawazimu ili kukwepa majukumu yake kama baba. Dubwa alipomaliza kusoma hakutaka kurudi tena nyumbani.

Wahusika hawa ni wenye nafsi mbili. Bi. M, Dubwa, Bori na Yungi. Ni wahusika wa kiuhalisiajabu ambao wanageuka kuwa binadamu halisi. Matukio haya yanapotokea, Ndi hufikiria yu ndotoni. Hili linadhihirisha wazi wazo la Zamora & Wendy (1995) wanaeleza kuwa ndoto na uhalisia haviwezi kutenganishwa. Mtunzi naye ametumia mbinu hii ya kuchanganya wahusika ili kutoa uaminifu wa kuwa mambo ya kiuhalisiajabu yanaweza kutendeka katika mazingira halisi kama matukio yale yanavyojitokeza kwenye nyumba ya Ndi.

4.1.4 Kiumbe Bila Umbo Dhahiri

Kiumbe kisicho na umbo dhahiri ni kiumbe cha uhalisiajabu. Kwa kawaida kila kiumbe huwa na umbo dhahiri ambalo mtu huweza kuelezea kwa kina na taswira yake kuonekana. Umbo la kitu ndicho huleta tofauti za kina baina ya vitu ambavyo hukaribia kuambatana. Mwandishi Said A.Mohamed ameumba viumbe katika riwaya hizi teule ambao hawana umbo dhahiri.

Bi Muse, katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), anapomtokezea Ndi, Ndi anachanganyikiwa kwa kuwa hawezi kumwona vizuri. Mara nyingi Ndi anasikika akimwuliza umbo lake linakaa aje wakati anajitokeza kumsaidia. Ndi anauliza:

Unaonekanaje; yaani umbo lako? Nilimtosha kwa swali.

Vyovyote vile unavyoweza wewe kufikiri. Alisita akanitunga macho yake ya usingizi.

Kwa kawaida, aliendelea, sina umbo maalum. Ni aina ya jeteta linalochanua jinsi andasa zangu na zake zinavyokubaliana kuchanua. Sikuzaliwa katika dhati na bayana ya mambo. Mimi ni binti wa Zeus na Mnemosyne. Asili yangu inasimamia kumbukizi na dhana tu. Ndio maana nina majina mengi kwa mujibu wa kazi yangu ya kutia ilhamu. Calliope, Clio, Erato, Euterpe, Melpomene, Polyhymnia, Terpsichore, Thalia, Urania. Hata unaweza kuniita Bi Mize, kwa jina la kikwenu, kwani hapa nilipo nimekuja kwa sura ya kikwenukwenu, kipande samaki, kipande mtu, kipande ndege (Uk 69).

Inajitokeza bayana kuwa, Bi Muse, anajitokeza kwake Ndi bila umbo dhahiri. Hata yeye katika maongezi yake na Ndi anamhakikishia kuwa hana umbo maalumu na ana majina mengi. Katika hali hii anajitokeza kumsaidia Ndi kuhusiana na maandishi yake. Amekuja kumwongoza jinsi ya kuandika. Kimsingi, anajaribu kueleza kuwa umbo lake si muhimu ila kazi aliyokuja kufanya.

Vile vile katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi mle bustanini, kwa wakati mwingine anahisi Bi Muse kamwacha peke yake ingawa bado huwa anahisi kama kwamba kuna nguvu zingine tofauti mle. Anaeleza jinsi majitu yalivyotaka kumvamia katika kibanda alimokuwa lakini hayangefaulu. Majitu waliposhindwa kumvamia, wakaanza kumwita jina kwa sauti naye hakuitika kamwe. Katika harakati zake za kutembea msituni mle alihisi mtu au kitu kimekata njia. Lakini alipoangalia hakuona kitu.

Ndi bado ana hamu ya kumwona na kumtambua Bi Muse, anamwuliza;

Sura yako ikoje hasa?

Samakimtundege, alijibu kwa tamko moja na kicheko.

U kama nguva mwenye mbawa? Lazima u kichinchir....

Alisita, sikumwona, lakini nilihisi msito wake katika upofu wangu...

Bibiye Mize, usinivunje. Nilitafadhalisha.

Sawa, nitajibainisha,” alinihakikishia, Lakini kipicha tu. Kupitia kwenye kompyuta yako (Uk 72).

Katika ile harakati ya kutaka kumwona Bi Muse, Ndi anamsihi mara hii ajitokeze amwone umbo lake alivyo. Bi Muse anamwambia atajitokeza tu kama picha kwenye kompyuta yake na si kiwiliwili chake chote.

Katika dunia ya kiuhalisiajabu, wahusika viumbe wanajitokeza hata kwa umbo lisilodhihirika. Hata hivyo, mwandishi bado anawatumia ili kufikisha ujumbe wake kwa wasomaji. Si jambo la kawaida kukutana na kiumbe ambaye huwezi kueleza umbo lake lilivyo. Hivyo jambo hili linaafikiana na Chanady (1985) aliposema kuwa uhalisiajabu unahusu matukio yasiyo ya kawaida, si ya kimiujiza na ni kinyume cha uhalisia wa kawaida.

Mwandishi katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2010), anaeleza kuhusu Moshi anayemzuru K. K anaketi macho juu na kusema nalo hilo dubwana lenye mwili wa moshi na uso wa bango usio macho, nyusi na kope, pua wala mdomo-nila labda masikio yaliyoning'inia pembeni kama tojo za mgomba.” Na kwa hivyo kila mtu aliyekuwepo hapo alikuwa akimshangaa K. Mazingira kama asemavyo Zamora & Wendy (1995) ni sehemu muhimu ya kazi za fasihi. Mazingira huchangia katika kuelewa mambo mengi kama kuimarisha matendo ya wahusika, kueleza sifa na tabia zao na hali zao. Mazingira huweza kuwa mhimili mkuu wa kuyaendeleza maudhui ya kazi ya kifasihi (Wamitila, 2003). Katika mazingira ya kiuhalisia mambo yanayohusiana na dunia halisi

hutendeka. Katika mazingira ya kiuhalisiajabu, mambo na matukio ya kiajabu ajabu hutendeka. Hivyo, mazingira anamotokea jini la Sinbad kwa K, yanaendeleza utu unavyodhihirishwa na jini hili.

4.1.5 Sauti

Kuhusu mhusika Sauti, TUKI (2013: Uk 482) inafafanua sauti kuwa ni “mlio unaotokana na mgongano wa vitu k.v. chuma, msugvano wa ala za kinywa au mwili au kiumbe.” Lakini pia dhana ya sauti kwa mujibu wa kamusi hii inaweza kutumiwa kurejelea hali au kitendo cha “kukubaliana na jambo kwa pamoja” (kwa mfano, walisema kwa sauti moja), auni hali ya “kuwa na uwezo au madaraka kuhusu jambo fulani” (kwa mfano, usikubali kudhalilika hivi hivi. Lazima uwe na sauti na wote watambue u nani kwao). Kifasihi, hususani, sauti haisimami kama dhana ya mlio, kitendo au hali bali kama mhusika au wahusika wenye kauli moja kimaadili na kimamlaka dhidi ya watu wema au wanaokwenda kinyume na maadili ya jamii. Matumizi ya Sauti kama mhusika bunilizi ni mhusika na mbinu kongwe zaidi katika kazi bunilizi za Fasihi Simulizi za Kiafrika zenye kubeba mithiolojia ya kimazingara (Bertoncini, 1989).

Aghalabu kila mazingira huwa na sauti inayohusishwa nayo. Kwa mfano shuleni sauti inayohusishwa huwa kengele, barabarani tuna honi ya magari, hospitalini tuna sauti ya ambulensi na zenye mashine za hospitalini. Hivyo sauti ni chombo muhimu sana. Sehemu hii itadhihirisha sauti ilivyojitokeza kupitia wahusika wa kiuhalisiajabu. Kipengele hiki kinaingiliana na kuhusishwa na mazingira yanapotokea uhalisiajabu. Mazingira yanaathiri sana matukio ya kiuhalisiajabu kama asemavyo (Zamora & Wendy, 1995).

Sauti ya mhusika katika kazi za fasihi huweza kutumika kwa dhamira mbalimbali. Mhusika sauti huweza kutumika kuendeleza maudhui mbalimbali kufikisha ujumbe mbalimbali. Sauti katika kazi za kifasihi nayo huweza kutumika kuonya, kutoa nasaha na kufanya mambo mengine mengi. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), sauti inamkanya Ndi, inamwonya kuwa;

Ndi- mbele yako kunakuja dhoruba na vumbi, fumba macho. Kimbia! Usirudi nyuma!” Nami nilifumba macho na kukimbilia mbele. Mara kwa mara nilijikwaa au kugongana na mpitanjia au baiskeli iliyokata vichochoro pasi na mwendeshaji. Mara nyingine nilihisi alikuja mtu aliyeniongelesha nifanye hivi au kunionya nisifanye vile. Nilipomtafuta, sikumwona. Sikumjua mtu gani wala sikuweza kutambua kama alikuwa mtu kweli au la (Uk 70).

Sauti ya Bi Muse inasikika bustanini ikimwonya Ndi kuhusiana na yanayokwenda kumkuta na kumwongoza jinsi ya kujinusuru. Ndi anajitahidi kutambua anayemwonya na kumwongoza lakini anashindwa. Muhimu ni kwamba, kuna sauti yenye sifa ya utu ambayo kwayo kumtahadharisha Ndi unadhihirisha upendo wake kwa Ndi ili Ndi asiangamie.

Sauti vilevile huweza kutumika kumwelekeza mtu kuhusu jambo fulani. Kwenye riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), sauti ya mamake Nana inatokezea na kumwongoza atakapopata stakabadhi Fulani muhimu. Nana anaeleza kuwa;

Leo lakini jambo la ajabu lilimzukia. Kumbukumbu zilikuja kumvaa ghafla. Akaisikia sauti ya mamake inamnong'onezea: 'Ile amana, ule mzigo niliokupa uutunze, umeufungua? (Uk169).

Mama anamwongoza Nana kwenye begi aliloambiwa hapo awali. Mle ndani ya begi alitoa barua ya kwanza ambayo mama alimwandikia kuhusu cha kufanya hadi akavunja ungo. Mara tena sauti inamwelekeza kwenye begi kuchukua barua ya pili. Nana amekosa kuanza alichodhamiria kwa sababu ya kukosa fedha. Mle ndani ya begi anamomtuma Nana, kuna fedha na kitabu cha benki. Mwandishi anaeleza kuwa:

Masatu (2019) amegusia uhusika wa mhusika sauti. Masatu anaeleza jinsi mhusika sauti amedhamiria vitu mbalimbali kama vile kuwasuta watu wa maovu wanayotenda na hata kuwaongoza kwa mema wanayopaswa kufanya. Sauti kama mhusika, anaonekana pale akizungumza na Joan. Yeye ni kitoto kidogo kinachotaka kuavya. Sauti yake inamzungumzia mamake Joan kwa kumuuliza kosa lake ni lipi ndiposa akataka kunyimwa haki ya kuishi. Sauti ya pili inasikika ikimuuliza Joan kwa nini ameamua kumwua mjukuu na kwa nini ameamua kuitwa mama ya marehemu. Masatu (2019), ametumia sauti kama mtetezi wa haki za watoto. Utafiti wa Masatu na utafiti huu umedhihirisha sauti kama mhusika ambaye huweza kutimiza malengo mbalimbali. Aidha, katika utafiti huu sauti inatumika kuonyesha utu tofauti na utafiti wa Masatu ambapo sauti inajitokeza kama mtetezi wa haki.

4.1.6 Ishara

Ishara ni kitu kinachosimama kuwakilisha kitu kingine (Mturo & Omboga 2018). Kwa mfano msalaba ni ishara ya ukristo. Kwa upande mwingine ishara huwakilisha kitu kinachoashiriwa. Mturo anaendelea kufafanua ishara kwa kusema katika muktadha wa kawaida wa jamii, maji ni

ishara ya uhai lakini katika muktadha wa kidini ni ishara ya majaribio, uzima, usafi na matumaini. Hata hivyo, ndani ya matini, muktadha na dhamira husaidia ishara kutokeza. Kimsingi ishara hailengi maana mahususi bali hupendekeza maana inayohusiana na kiashiria mahususi.

Katika kazi ya (Lynch & Roberts, 2010) ishara zimetumika kuashiria mambo mbalimbali. Mfano, katika usaili na wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu na walimu wa fasihi ilielezwa kuwa; ishara ya shetani, huwakilisha ukoloni mambo leo ambao upo katika jamii baada ya ukoloni mkongwe kuondoka jamii za kiasia ziliingia katika utawala wa ukoloni mambo leo ambapo anayetawala anakuwa haonekani kama vile ambavyo huwezi kumwona shetani. Hivyo shetani ametumika kiishara zaidi. Kazi hii inafaa kwa kuwa kutokana na maelezo ya vitabu teule ishara mbalimbali zinajitokeza kuashiria maana mbalimbali.

Ishara inajitokeza katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana anaona ishara mbalimbali kama vile mbingu inayogeuka uso unaofumbua mdomo. Anapokosa kuelewa vizuri ishara ile, panatokea ishara zaidi. Kwake yeye Nana ishara hiyo ni ya kitu kizuri. Anasema kuwa;

Nilipotazama mbingu, iligeuka uso uliofumbua mdomo kusema nami. Lugha niliisikia kwa mbali katika sikio langu la ndani, lakini maneno yenyewe sikuyaelewa. Baadaye uso wa mbingu ulipoona sielewi kitu, ulitabasamu kwa kukunjua rangi za mapambazuko. Je, kulikuwa na ishara njema kwangu zilizotoka kwenye uso huu wa maumbile? Baadaye madege ya pwani yalikuja kunizunguka mara saba. Yalinizunguka kwa kwenzi juu ya kichwa chake kama vile wakinizingua (Uk 129).

Kwa mara ya kwanza, Nana ametoroka kwao. Anakotorokea hajui. Yuko mikononi mwa Faisal-mpiga gita. Alikuwa rafiki wake wa kufana. Ndiye mtu mzuri aliyejua katika dunia ya nje mbali na kwao. Faisal anamtorosha hadi kwao, jiji la Sambejenge. Wamefika jijini. Hali ya hewa na mandhari yanamshutua Nana. Nana alizoea mandhari ya kifahari. Mandhari yenye utulivu bila kelele yoyote, mazingira yenye hewa safi na iwapo hewa ilikuwa mbaya, wangepukiza manukato. Barabara msongamano wa wachuuzi. Anahisi kuwa yupo pahala pabaya. Amesononeka. Faisal amekwenda kumtembeza ufukweni. Anahofu, ila anapotazama mbingu anapata nguvu fulani. Anahisi hiyo ni ishara ya kitu kizuri kitakachotendeka.

Maana ya ishara hujitokeza katika muktadha wa matumizi. Snowden (2006), anaeleza namna ishara hujitokeza katika fasihi. Snowden anaeleza wazi kuwa ishara hujitokeza katika vitu hai, visivyo hai na katika vitu dhahania na hivyo hujitokeza katika mazingira fulani. Zamora & Wendy (1995) wanaeleza jinsi mazingira ni sehemu muhimu katika fasihi na katika uhalisiajabu wanyama,

majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Katika riwaya ya *Nyuso za mwanamke* (2010), Nana yupo katika mazingira tofauti na alikozoea, lakini la kustaajibisha ni kuwa anapoangalia bingu anapata nguvu fulani na kuhisi ni ishara ya kitu kizuri kitakachotendeka. Kule kuangalia mbingu na kuwa na ishara tosha inathibitisha marejeleo ya nguvu za kiajabu ajabu katika mazingira fulani.

4.1.7 Kiumbe cha Kiajabuajabu

Kwa mujibu wa Zamora & Wendy (1995), katika uhalisiajabu, wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari, mazimwi na hata viumbe wa kiajabuajabu hurejelewa. Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana yupo chumbani, hajielewi, yumo ndotoni anapomwona mamake akijitokeza kama kiumbe cha ajabu. Akieleza ndoto, King'ei (2002) anasema kuwa ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu ambaye yuko macho au amelala na yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikra za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, malengo, matarajio na matamanio. Hivyo basi ndoto husafirisha tabia na sifa za mtu kwa sababu huambatana na matukio kadha wa kadha katika maisha ya anayeota na vilevile picha halisi ya mambo anayowaza. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), mawazo ya Nana yanaonekana kupitia ndoto, anasema kuwa;

We Nana! Ile ndoto yangu iliyopigisha rangi iliniita. Kwa sababu sikuitika, ilitoka kichwani kuja kuning'inia juu ya dari chumbani mwangu. Ilipoona nimeipuuza, ilichukua umbo la kiumbe cha ajabu ambacho sijapata kukiona. Kiumbe aliyechanganya rangi za ukole... 'We Nana!' Kiliita tena hicho kiumbe cha ajabu (Uk 133).

Nana alipokuwa akipumzika chumbani mwake, mle alikotorokea. Kiumbe huyu anajitokeza kwake kumkumbusha kuwa alitoka kuja kumtafuta mamake na kumkomboa mwanamke wa kitaarab, ilhali yeye yumo pale chumbani amekaa tu. Anamhoji na kumshurutisha awache kuwa mwoga na aondoke afuate kilichomleta pale. Nana anamwelezea kuwa yote haya yamekuwa magumu kwa sababu ya kukosa fedha. Anampa changamoto ya kuwa amekwisha mwelezea nani kuwa amekosa pesa? Amemweleza hata Faisal ambaye ndiye mwandani wake hapo alipo? Nana anapata nguvu na kujitokeza kwenda kutafuta riziki. Nana anajizungumzia. Anaeleza kuwa anazungumza na ndoto yake. Anapopuuza, linageuka kuwa kiumbe cha ajabu. Tukio hili ni la

ajabu sana. Ingawa inaweza kuonekana kuwa kawaida kwake Nana kwa kuwa kila mara viumbe tofauti vilimtokea, huwezi kuupinga uajabu au ukawaida wake.

Dhana ya uhusika wa kinjozi na usawiri wa wahusika ni pana mno na huweza kujumuisha bunilizi za kisayansi na kazi za kiuhalisiajabu. Unjozi huhusishwa na matukio yasiyo ya kawaida bila kutoa sababu za kutokea kwake. Ndoto ya Nana imeweza kuonyesha dhana ya utu ilivyojitokeza kupitia umbo la kiajabuajabu.

4.1.8 Jini

Kuna imani kuwa kuna kiumbe wa kiajabu ambaye anafahamika kama jini. Kiumbe jini ni kiumbe ambaye binadamu huhusishwa nacho kwa njia nyingi. Huweza kutumiwa kutimiza ahadi fulani alizo nazo binadamu. Binadamu huwa kama mkuu wake nacho kikawa mtumwa. Wakati mwingine huangaziwa kama ibilisi au hata malaika kulingana na matendo yaliyotendeka binadamu fulani. Wengi nao wannamini kuwa, jini huhusishwa na mabaya tu. Wengi wa wananchi walio katika nchi za kiislamu wana imani kuwa na uhusiano na jini. Mbiti (1991) akinukuu kitabu takatifu cha Quran anataja jini na kueleza kuwa limeumbwa kutokana na moto au moshi. Kitabu hiki kinaeleza kuwa, binadamu, jini, malaika na shetani ni viumbe wa Mungu. Pia inafafanua kuwa kama binadamu, jini huweza kuwa baya au zuri. Kutokana na mwandishi Said A.Mohamed, jini katika riwaya yake ni jini nzuri. Hili linajitokeza akija kumwonya K dhidi ya kujiingiza katika tabia za ukengeushi.

Mwandishi Said A. Mohammed katika riwaya yake ya *Babu Alipofufufka* (2001) anadhihirisha umbo la jini pale linapojitokeza kwa K. Anaeleza kuwa;

Mfu alikuja kuning'inia juu ya meza kwa mtindo wa jinni la Sinbad. Alijitokeza pale na ni K tu ndiye aliyemwona. K alikuwa akinena na yule jinni, hajamakinika kwa mazungumzo yake na marafiki zake kwa sababu ya yule jinni. Linalomsumbua Zaidi ni kuwa hajaamini kama tukio lile linamtokea kweli. Anaogopa kuwaeleza wenzake kwa kuwa kadhani ataitwa punguani. Hatimaye anasalimu amri na kukubali matukio yamfanye yanavyopenda (Uk 35).

Jini la Sinbad linapojitokeza kwa K, linajitokeza likiwa na sababu nzuri na wala si mbaya. Linajitokeza kwa K na marafiki zake wakiwa pale Neo-Casino katika harakati za kujifurahisha. Wanawake wako pale wa kuwafurahisha. Kuna mwanamke moja ambaye yupo pale na inaaminika asipokuwepo basi sherehe haiwezi kunoga. K hajamakinika, anasumbuliwa kifikra iwapo anaota, analiona jini lile kwa ukweli au amewehuka. Hili jini limekuja hapa kumtahadharisha K kutokana

na ukengeushi. K na wenzake wanakula vyakula vya kitamaduni za kimagharibi na kupotosha maadili yao kama waafrika.

Katika sehemu hii suala la umbo la viumbe linavyojitokeza wakidhihirisha utu umeshughulikiwa. Viumbe hawa wameonekana wakijitokeza katika maumbo mzuka, kivuli, sauti, malaika, jini, binadamu halisi na hata kwa umbo ambalo haliwezi kuelezwa bayana. Hata hivyo, sifa ya utu ilijitokeza katika viumbe hawa.

4.2 Udhihirishaji wa Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu

Utu ni hali ya kuwa na uadilifu. Utu huhusishwa na matendo mema kama vile: kulisha, kusaidia katika shughuli, kuongoza na hata kutahadharisha wengine kiasi cha kuwaathiri vyema kisaikolojia. Ni uzuri wenye nia ya kutia wengine mazuri na mema yaliyo na kifani. Utu ni kufanya mema unavyotarajiwa na wanajamii (Oruka, 1990). Ni muhimu kwa kila binadamu kuonyesha utu kwa binadamu wenzake (Palmer, 1992). Palmer anaendelea kutaja kuwa, binadamu mwenye utu na upendo huwa tegemeo zuri kwa mwenzake. Mara nyingi hupeana msaada panapohitajika na kila wakati huona kuwa ni wajibu wao kuwasaidia wenzao.

Matendo ya utu hujitokeza kwa njia mbalimbali; kwa mfano kusaidia mayatima, maskini, wazee na wajane. Watu hawa wanaweza kusaidiwa na makao mazuri, lische bora, nguo za kuvaa na hata elimu kwa wale wanaohitaji. Vilevile unaweza kulisha walio na njaa, kusaidia walio hatarini kama vile walionyang'anywa mali kwa njia mbalimbali, kutembelea wagonjwa hospitalini na kwa kuwasaidia kulipia ada za hospitalini na kununua dawa. Aidha unaweza kuwatembelea wafungwa ukawabebea mahitaji maalumu kama vile sabuni, sodo, mafuta ya kujipaka na mengineyo kwa kuwa pengine hukosa kuwatosha kila mfungwa kule korokoroni.

Katika riwaya teule, viumbe wa kihalisiajabu wamesawiriwa wakimiliki sifa ya utu kupitia njia zifuatazo; kuonyesha upendo, kuonyesha heshima, kutoa ushauri nasaha, kusema ukweli, kuwajibikia nafasi fulani, kusamehe, kupeana motisha kwa wengine, kuwa wakarimu na hata kuwaongoza kwa njia mbalimbali. Vijisehemu vifuatavyo vinawasilisha namna ambavyo viumbe wa kiuhalisiajabu walivyotumia mbinu mbalimbali na hisia tofauti kuonyesha utu kwa binadamu.

4.2.1 Upendo

Upendo ni sifa mojawapo aliyo nayo binadamu. Binadamu huonyesha upendo kwa njia mbalimbali. Anaweza kumwonyesha mwenzake upendo kwa kumsaidia nyakati za shida fulani kama vile; kumchangia pesa ili aweze kupata hela ya kujitibu au kulipa karo. Pia huweza kusaidiana kwa kumshughulikia rafiki yako akiwa hospitalini au mgonjwa nyumbani kwa kumwosha, kumlisha, kumsafishia nyumba na mengineyo. Wazazi huonyesha upendo kwa watoto wao wanapowatahadharisha na matendo yanayoweza kuathiri maisha yao. Aidha huwashinikiza watoto kusoma kwa bidii ili waweze kuwa na maisha mema. Mtu pia huweza kumwonyesha mwenzake upendo kwa kumpa wosia wakati ambapo mwenzake anapitia changamoto fulani maishani.

Upendo wa Mzuka kwa K unadhihirika mwandishi anapotumia motifu ya safari. Motifu ni kipengele radidi cha kijadi au kikaida cha kifani au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka (2010)* msanii ametumia motifu ya safari katika kuwasilisha na kujenga utu anaodhihirisha Babu kwa K. Hapa tunaona kuna motifu ya safari ya K na Mzuka. Matumizi ya motifu humfanya msanii kujenga visa na matukio kupitia safari za wahusika kwenye kazi za fasihi, kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Mathalani safari anayompeleka K kwa dunia yao Mzuka.

Upendo wa Babu kwa mjukuu wake K unajidhihirisha walipokuwa safarini aliposikia sauti ya K ikimwambia kuwa:

Watakuja, lakini usitaharaki. Watakwepuka tu madamu sasa umevaa nguo zangu... Hawawezi kukudhuru wala kukuibia..." alimsikia mzuka akinasihi. Hakumwona lakini. Wala hakuiona ishara yake yoyote. Alisikia sauti yake tu ikirindima (Uk 123).

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka (2001)*, Babu mzuka anapompeleka K katika dunia yao, dunia inayoitwa Amani, K ana hofu ya kuwa watu wa dunia hiyo watamwangamiza. Babu mzuka anamtolea hofu kwa kumhakikishia kuwa hatafanyiwa chochote na yeyote. Babu anamvisha K nguo zake ili watu wa dunia yao waweze kujinasibisha naye. Kwa sababu ya upendo wake kwa K, anamlinda. Babu alimtembeza K katika dunia yao akiwa na matumaini kwamba K ataweza kubadilika na kuwa mtu mwema anayejali wenzake. Anamwelezea kuwa anataka tu aione dunia

nyingine ili afahamu anachoambiwa kuwa yeye na wenzake wamebadilika sana kwa kukosa kuwaona wengine kama wenzao.

Mwanamke katika jamii za kiasia ametwikwa majukumu kadhaa yakiwemo kazi za kusafisha nyumba, kuangalia usafi wa mume na watoto na hata kupika na kuandaa chakula cha familia (Mbiti, 1990). Ingawaje ni majukumu anayopewa mwanamke, hudhihirika tu panapo upendo kwa familia. Katika riwaya ya *Dunia Yao (2006)*, upendo wa Bi. M kwa mumewe Ndi unadhihirika anapomshurutisha ale. Bi. M ananyanyuka kutoka kwenye alamu kumshughulikia mumewe, tendo hili linadhihirisha kama kiumbe wa kihalisiajabu.

Anasema kuwa;

Leo ya tatu hujakula kitu... Unataka kujiua? Wewe mja wa ki-Islamu unafanya hivi? Unataka kujiua na unajua Mungu hawi radhi (S.A.Mohamed 2006, Uk 21).

King'ei (2002), anayeleva kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamano. Maelezo haya yanadhihirika wazi Ndi anaponekana akiwa amechanganyikiwa. Hajui iwapo anaota au haoti. Ndi hana uhakika ikiwa aliuona picha ukinyanyuka au ni mwili wa Bi M. Hajui kama ni kuota anaota au ni fikira tu kutokana na athari ya video vya kutazamwa. Kisha tena anajihakikishia kuwa ni dhahiri amemwona Bi. M akinyanyuka akaemewa. Katika hali hii utu wa Bi. M unajitokeza anapomshurutisha mumewe kula chakula. Anafanya hivi kwa kuwa siku kadhaa amejifungia tu chumbani kwake hali. Hakuwa anakula kwa sababu alikuwa na aibu kula kilicholetwa kupitia bidii ya mwanamke. Alidhani kuwa chaula kile kilipatikana kutokana na kazi ya ukahaba. Kwa kuwa anampenda mumewe, anajali afya yake na kumlazimisha kula.

Vile vile upendo wa Bi. M kwa mumewe bado unadhihirika anapompelekea chakula na kumhakikishia kazi inayomsaidia kwa mapato ni kazi nzuri wala sio kazi haramu anavyofikiria mumewe. Anamwambia kuwa;

Nakuletea chakula hiki. Nimekichuma kwa jasho langu na kukipika mimi mwenyewe. Kama nilivyokwisha kueleza, siku hizi nafanya biashara ya kuuza vyakula ofisini (Uk 23).

Ndi hataki kujishughulisha na chakula kile kwa kuwa anafikiria kuwa ni ya kikahaba. Hakutaka mkewe kutoka kutafuta riziki kwa kuwa jukumu hilo lilikuwa lake. Mkewe hata hivyo anamhakikishia kwamba chakula hicho amekitafuta kwa jasho lake.

Katika tamthilia ya *Mama ee* (1997), mwenye nyumba, wanakoishi Mwavita na Kinaya, alifahamu kuwa Kinaya ndiye mpangaji wake lakini hakufahamu kuwa Kinaya alikuwa ameshamtwika mkewe Mwavita majukumu yote ya kuitunza na kuikuza familia yake. Kinaya hakuwa na habari jinsi kodi ilivyokuwa ikilipwa wala chakula kilivyokuwa kikitafutwa nyumbani. Kuna dhana miongoni mwa baadhi ya jamii ya kuwa ikiwa bwana yungali hai, mkewe hawezi kuwa mumiliki wala kuhesabiwa kuwa ana chochote. Mwavita alipenda kulalamika kwa sababu ya masaibu aliyokuwa akipitia katika ndoa yao. Wanapobarikiwa na mtoto Juma, Mwavita tu ndiye anayeshughulikia mtoto na vitu vya nymbani. Kupitia mapato yake anampeleka mtoto hospitaini na anapata huduma. Bila juhudi zake Mwavita, mtoto angeaga dunia. Kinaya anaporudi, ni vita tu na kumchapa mkewe. Mwavita alikuwa akimlalamikia Kinaya kila wakati. Wakati unafika ambapo Mwavita hakuweza kuvumilia akaomba talaka. Anakubali kuenda na kumwacha mtoto wake Juma. Tofauti na wanawake wenye hulka hii, Bi. M ni mwanamke mwenye mapenzi kwa mumewe na mwenye kuvumilia katika hali zote.

Upendo wake Bi. M kwake mumewe unafanya anamwonea mumewe huruma. Mapenzi ya Bi. M kwa mumewe yanampelekea kumtunza mumewe licha ya kwamba yeye ameasi majukumu yake ya kulisha na kuikinga familia yake kama vile mwanamume anapaswa kufanya. Kuna wanawake hasa wa kisasa ambao huasi majukumu yao wakati mumewe hana uwezo tena wa kuwajibika. Wengi hutoroka kutoka kwa ndoa zao, wengine wakipata chakula wanamyima mume, wengine wanamsuta kwa kutelekeza familia lakini hatumwoni Bi. M akifanya hivi. Inadhihirika wazi kuwa katika ulimwengu wa sasa, mwanamke tu ndiye hutwikwa mzigo mzito wa kuikimu familia. Wao huendesha shughuli hiyo vilivyo kwa moyo mkunjufu.

Utu wa Bi. M unaendelea kujitokeza anapomwonyesha mumewe heshima na mapenzi ya dhati. Anataka kuzingatia mambo fulani ndiposa ampe habari mumewe. Anamwambia mumewe Ndi kuwa:

Yungi hajarudi mpaka saa hizi.

Niliona niseme naye kwanza... Najua moyoni umejaa tafshani nyingi mno... Sikutaka kukutwika mzigo mwingine juu ya mzigo ulionao tayari.

Tena?

Aliniambia lazima afanye kazi. Wewe eti huwezi tena kuiendesha nyumba hii. Na mimi kizee cha Mungu, tena mwanamke. Alisema kwamba hii ni dunia yao. Dunia ya vijana.

Kazi gani anafanya?

Nilipomwuliza hakujibu... (Uk 24).

Kutokana na dondoo hili, imebainika kwamba Bi. M anamheshimu mumewe. Hataki tabia ya Yungi imwongeze mumewe mrundiko wa mawazo zaidi na kumrudi mwanawe kabla ya mumewe kujua. Anamtaka mumewe atulize akili kwanza. Yungi, hutoka nyumbani kuenda kwa biashara ila anahisi si biashara nzuri. Anajua litakuwa suala la kumhuzunisha mumewe kwa hivyo anatafuta wakati mwafaka wa kumwambia. Bi. M anayatekeleza majukumu yake kama mke pale nyumbani. Anahakikisha kuwa mumewe amekula na kupata pumziko baada ya kula. Baada ya hayo yote anatafuta muda mwafaka ambao atamtolea ujumbe mumewe. Anapopata muda mwafaka anamweleza mumewe Ndi yaliyotokea. Hii ni sifa ya mwanamke mzuri katika jamii nyingi za Kiafrika. Kwa kufanya hivyo, mwanamke huwa anaonyesha utu kwa mumewe. Hataki kumvuruga akili.

Kwa kawaida sio wanawake wote huwapa waume zao utulivu. Katika riwaya ya *Chizi la Heri* (2014), Naomi, mkewe Lunga tunaambiwa ni miongoni mwa wale ahali ambao hata wanapoolewa hawasahau uhusiano wao na nasaba zao. Hawatulii kuyapalilia maisha ya unyumba. Daima hujiona wageni katika familia za wakwe zao. Naomi anaishi akimkaza mumewe kuwa anataka awakimu kama familia yake. Anarejelea hadithi ya mzungu fulani aliyemjengea mpenziwe nyumba kubwa akasema ni kiota. Kisha anamwambia mumewe Lunga kuwa naye hataki nyumba aliyojengewa. Siku moja Lunga aliamka na kumkuta mkewe ametoroka. Aliamshwa na ujumbe wa simu, akaamka kusoma ujumbe. Ulikuwa umeandikwa; “Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kukimu familia. Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao. Kwaheri.” Naomi.

Vilevile, katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Shaib na Ndi wanapendana. Kutokana na upendo huu, tunamwona Shaib akimzuru rafikiye kwenye baraza yao akiwa mpweke. Mwandishi anataeleza kuwa;

Baada ya taaluma. Tulikuwa pekee yetu. Mimi na Shaib. Ndiye pekee niliyeweza kuzungumza naye hapa. Kivuli chake nakusudia. Siku hizi sisemi na mtu ila kivuli cha Shaib. Ye-, yaani Shaib, huzungumza nami ingawa simwoni. Alikuwa ameshakufa – kwa namna halisi ya kufa. Lakini bado alikuwa na uwezo wa kuniingia na kunining’inia

kichwani. Niliweza kumhisi ndani ya nafsi yangu wakati wowote. Lakini zaidi nilipokaa kwenye baraza hii ya taaluma (Uk 40).

Ndi na Shaib hukutana katika baraza ili kuzungumzia mambo mengi ambayo huwa yenye manufaa kwa Ndi. Huku kumzuru Ndi wakati akiwa mpweke unadhihirisha utu alionao kwake kupitia upendo. Upendo wa Shaib na Ndi ni upendo wa dhati. Wao ni marafiki wa dhati. Marafiki wa dhati hufaana wakati wa dhiki au wakati wowote ambapo rafikiyo huhitaji msaada wako. Shaib hujitokeza kumzuru Ndi wakati Ndi akiwa mpweke na kumsaidia kutatua mambo mengi. Hataki rafikiye ajizamishe katika fikira mengi mpaka apatwe na mzongo wa mawazo yanayoweza kusababisha magonjwa ya kiakili. Huku ni kumjali rafikiye. Hii ni sifa inayohusishwa na binadamu lakini kupitia dondoo hili, tunaona ya kwamba hata viumbe wa kialisiajabu wanaimiliki sifa ya utu.

Bori ametoka kwenye albamu. Anampenda na kumjali babake. Haya yanadhihirika anaposema kuwa;

Wapumbavu wote sisi... alipasuka ghafla.

Sisi watu wa nyumba hii... alijibu

Ati tumekuhasimu. Tumekugomea. Hatusemi nawe.” Alisema hivyo kwa kuyatafuta maneno. Alikuwa anapata shida kufululiza.

La, mimi ndiye niliyewahasimu. Mimi ndiye niliyewagomea na kutotaka kuwa nanyi kabisa “Aaaa, mimi nakupenda. Najua wewe baba yetu. Najua una hamaki nasi. Kuwa kabisa huwezi tena kutusaidia. Hata wewe mwenyewe huwezi kujisaidia. Na sisi hatuwezi kukusaidia. Si kazi ndogo! Lakini mimi nitakuwa injinia. Siku moja nitapata pesa nyingi za kuichukua nyumba hii (Uk 113).

Maneno haya ya Bori yanaonyesha kwamba yeye hapendezwi na jinsi watu katika familia yao wamemwasi babake. Anamwonea huruma babake kutokana na upweke uliogubika maisha yake japo ana familia. Anamwonea huruma jinsi ameshindwa kukimu familia. Yungi anaonekana kuwa mwenye matumaini kuwa atakuwa injinia na kuweza kumsaidia babake na familia yake. Hii ni sifa ya utu anavyodhihirisha Bori na inaonyesha kwamba yeye anamjali babake.

Familia ni muhimu katika maisha ya binadamu. Binadamu hasa huwa na familia yake ili asiwe anaishi maisha ya upweke. Panapo familia, mtu huweza kufanya mambo kadhaa ikiwemo kutangamana. Katika kutangamana huweza kujieleza na akasaidiwa kutatua mengi yanayomtatiza. Ndi ana familia ambayo imemwacha akiwa mpweke. Familia yake imemuasi kwa shutuma ya kuwa hawezi kuwakimu kama kiongozi pale nyumbani. Watoto wake nao wamemuasi. Yungi

anaingia katika ukahaba licha ya babake Ndi kumkanya. Anasimama kidete na kujibizana na babake mzazi. Kilua tu, kitinda mimba wake ndiye anayemjali. Katika dunia yao, vijana, wengi hawajali wala hawatii wazazi wao. Katika ulimwengu wa sasa vijana wamewaasi wazazi wao kwa sababu za tofauti za kiumri zinazoletwa haswa na teknolojia. Wengi wanaona kana kwamba wazazi wao hawaelewi mambo ya kiteknolojia na hivyo hawawezi katu kuwasaidia. Masuala kama haya yamewafanya vijana kujikuta wakiwatii tu marika zao. Matokeo yamekuwa mabaya kama kujiingiza katika shinikizo la marika, kutumia dawa za kulevya na hata kujiingiza katika wizi ili kujikimu na yale marika.

Upendo wa mama kwa mwanawe huwa dhahiri. Kwa kawaida, mzazi hasa mama, hujikaza awezavyo kuwakimu watoto wake. Chochote kitakachoweza kumdhuru mama na watoto wake, kina mama wengi hujitolea kuwanusuru watoto. Vile vile, katika bara la Afrika, (Mbiti 1991) anaeleza kuwa, Imani ya waafrika kwa wazazi wafu ilikuwa kwamba wanalinda watoto wao walioachwa nyuma hata wakiwa makaburini. Mbiti anaendelea kutaja kuwa wazazi wafu waliulizwa kuwaongoza wanao waliosalia wakiishi. Ungepata makaburi yao yanatembelewa pakiwapo na tatizo lolote. Aidha, hili linadhihirika katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) upendo alionao mamake Nana kwake Nana ulikuwa wa ajabu. Nana anaposema;

Nimekuwa nikimshuku uhalifu mama bure... ame... amenirehemu... ame... amenionyesha miujiza, amenivimbisha mapenzi moyoni mwangu... amenifanya nijute kujisusuika.

Miujiza gani Nana?

Nimeamka tajiri, alijibu Nana huku akicheka kicheko kipana na kinene kilichoibuka nyuma ya machozi. Alicheka mpaka kuta zikacheka naye. Faisal naye akaambukizwa kicheko. Wakacheka wote wawili huku wamekamatana mabega na kutazamana migongo. Hapo tena Nana akamwonyesha Faisal ile hundi ya shilingi milioni tisini na kibarua kidogo kilichokuwa kimefungamanishwa na hundi hiyo na kitabu cha benki kwenye bahasha maalum. (Uk 171).

Mamake Nana, Bi Mkubwa alipokuwa hai, aliweza kumwekea mwanawe akiba ya fedha na mali alizochuma. Hata baada ya kufa, upendo ule unamfanya amtokezee Nana na kumwelekeza kufikia zile fedha, baada ya kumwona Nana anateseka kwa kukosa fedha. Nana anafurahia. Haya tunayapata kupitia mazungumzo ya Nana na Faizal anapomwambia kilichotokea. Nana anafurahia kwa kupata zile pesa taslimu na zile zilizo kwenye benki. Anaona kama atatimiza ndoto zake zote kwa kutumia fedha zile. Nana alitarajia kuwa mwanataarab maarufu ambaye alikuwa na bendi yake. Kilichomkoshesha ndoto yake ni hela tu. Hivyo matumaini yake na furaha inazidi anapopokea

barua ile kutoka kwa marehemu mama. Ni kawaida kwa wazazi kuwapenda watoto wao na hata kuwapa urithi wa mali zao. Hapa tunamwona mamake Nana akimrithisha Nana mwanawe mali aliyomwekea kupitia kujinyima mapato yake. Wazazi huwarithisha wanao mali kama vile mashamba, nyumba, magari, mabiashara na hata pesa.

Katika bara la Afrika, wengi wanaamini ya kuwa mtoto wa kike hapaswi kurithishwa chochote (Tebbe, 2008). Tebbe anaeleza kuwa Waafrika waliamini fika kwamba mtoto wa kiume tu ndiye hurithishwa mali. Pia imeaminika hadi sasa katika jamii zingine kuwa yeyote asiye na mtoto wa kiume katika familia yake, basi ukoo wake umepotea. Hivi wengi hadi sasa bado hawataki kurithisha mtoto wa kike. Hata hivyo kufikia sasa, pana mabadiliko makubwa barani Afrika ikiwemo hapa nchini Kenya. Mbote (1995) anaeleza kuwa ni haki jinsi katiba imeweka usawa wa kurithi mali kwa watu wote; wa kiume na wa kike, haswa ikiwa ilikuwa mali ya wazazi wao. Mbote, anaendelea kutaja kuwa asilimia themanini ya wanawake nchini Kenya ni wenye bidii kuliko wanaume na hivyo haoni ubaya wao kurithi mali. Anasema kuwa, asilimia kubwa ya wanamke wakirithi mali, huitunza na kuilinda vizuri kuliko wanaume.

Vile vile barani Afrika, inaaminika kuwa wafu wangejitokeza kwa walio hai kuwasaidia katika njia mbalimbali (Mbiti, 1991). Hivi, wafu wangewasaidia wanaobaki wakiishi kwa kuwasaidia kutatua mambo memgi yaliyowaandama. Kivuli cha mamake Nana bado huja kumzuru. Marehemu mama bado anampenda na kumjali mwanaye. Hili linadhihirika kupitia dondoo lifuatalo:

Pengine aliambukizwa na kivuli cha mamake ambacho sasa kimekuwa kikifululiza kumzuru, kuziba mapengo ya ukiwa na utengano. Labda mama mtu alikuwa anajaribu kufidia wakati wote alioupoteza alipotengwa nab inti yake. Aliponyimwa haki ya kukitunza ki- Nana chake (Uk 174).

Marehemu mamake Nana alikuwa akimzuru Nana kila wakati ili kuondoa ukiwa na utengano uliokuwa ukimwumiza mwanaye. Inabainika kuwa, Nana alikuwa mpweke. Alijaliwa kuwa na mamake wa kambo na babake lakini alihisi bado yu mpweke. Marehemu mamake Nana naye alikuwa akihisi kuwa amefeli kama mzazi kwa kutokuwa karibu na mwanae alipokuwa yu hai. Hivyo hata baada ya kufa, anashinda akimzuru Nana ili aweze kuziba pengo la utengano kati ya mzazi na mwanae. Hii ni sifa ya mapenzi ya mama kwa mwanawe.

Upendo wa nyanya kwa kitukuu wake unajitokeza katika *Nyuso za Mwanamke* (2010), Bi Mau, anapomwona mjukuu ake Bi Mkubwa pale nyumbani akimtunza kitukuu wake Nana. Bi Mau haamini kuwa mjukuu wake Bi Mkubwa alikwisha aga dunia kwa kujinyonga. Ana Imani kuwa hakufa ila alienda tu kupumzika na hivyo huja kwao kukilea kibinti chake. Mwandishi anaeleza kuwa:

Licha ya hayo, mpaka leo Bi Mau haamini kwamba mjukuu wake Bi Mkubwa amejinyonga. Hakufa Bi Mkubwa. Amekwenda tu kupumzika huko jongomeo. Kuwa Bi Mkubwa yumo mumo humo anaishi na watu wake ingawa haonekani. Yumo mwao akijaribu kukilea kibinti chake ambacho pia kimekuja kwao hivi karibuni. Yumo humo kumpa Nana mapenzi ambayo ameyakosa muda wote wa zamani. Anamwona akimbembeleza Nana huku akimpiga vikofi begani anapokuwa karibu kuchukuliwa na usingizi kila siku (Uk 175).

Hisia za mapenzi alizo nazo Bi Mau zinadhihirika kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Bi Mau alimpenda sana mjukuu wake Bi Mkubwa. Mapenzi yake nayo yanadhihirika kwa kitukuu wake Nana pia. Hivyo naye anafikiria kuwa Bi Mkubwa anampenda Nana, kitukuu wake na hivyo hawezi kumwacha kamwe. Anahisi kuwa hata baada ya kifo, Bi Mkubwa bado huja kumlea Nana.

4.2.2 Ushauri

Kumtolea mtu ushauri nasaha ni kumwonyesha utu. Unapotoa ushauri unaweza kuonya mtu, kumsihi afanye vitu kwa njia fulani au pia kumwelekeza katika njia mbalimbali. Kushauri mtu ni kumweleza kuhusu mambo mbalimbali anayostahili kuzingatia katika maisha yake ili ajiepushe na shida zinazoweza kumkumba katika maisha yake. Mtu aliyeonywa kisha akayapuuza aliyoambiwa huweza kujitumbukiza katika shida ambazo angeziepuka kwa kufuata ushauri nasaha aliotolewa. Binadamu anayekosa utu hutenda vitendo ambavyo ni vya kinyama kama kuiba, kupiga wenzake, kunyima mtu chakula, kumfukuza mtu aliyekuja kuomba msaada miongoni mwa matendo mengine mabaya.

K, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), anatembelewa na babu yake kumkosoa kuhusu tabia zake mbovu. Kwanza kabisa K ameishi kwa kasri kubwa, anamiliki kila kitu cha kifahari katika kasri lake. Mkabala wa kasri la K kuna watu maskini hohehehe. Watu hawa wanakosa chakula cha kutosha. K anaonekana kupitia wafanyikazi wake wakimpikia mbwa wake chakula ambacho binadamu anaweza kula. anakuja kumshauri K. K naye anasikika akiunga mkono marafiki zake waliotaka kujenga klabu moja mashuhuri ambayo yeyote anayeburudika mle ndani hangekubaliwa kuvaa vazi lolote bali wawe tu uchi wa kuzaliwa. Mawazo haya si mema kwa kuwa unapotosha

utu na hadhi ya binadamu. Tabia hizi mbaya zinamfanya mzuka wa babu kutotaka kumwingilia moja kwa moja. Babu anamweleza K kuwa;

Sikuweza kuingia kwa sababu ya farakano baina ya maisha yako yanayokimbilia upande mmoja tofauti na wanaokimbilia wengi maitikwenenda kama sisi. Dereva wako yuko karibu na mimi kuweza kumwingia kwa urahisi. Ingawa wewe na mimi ni damu moja, umebadilika mno na kuwa mgumu kufikika kwa mwanya mkubwa unaokukuza makusudi kila siku...Nikwambie tena, mimi ni babu yako; na kisha niongeze kuwa mimi ni dhahiri kwa kiasi kikubwa hata kuliko wewe kwa sababu sina farakano na watu. Wala sina makiwa na utawa kama ulionao wewe. Sihofu wala siogopi kama uogopavyo wewe. Nakwenda nipendapo. Nakutana na nimpendaye. Ufunguo wa kasi yangu ninao mwenyewe. Hakuna niliyemkera, hakuna niliyemdhulumu... (Uk 22).

Anamshauri ili aweze kutazama mambo kwa mtazamo mpevu. Anamshauri dhidi ya mabadiliko yake ya kitabia ambayo yamekuwa mabaya kwa kiwango cha kumtenganisha na babu yake ingawa ni wa damu moja. Hivyo, anajitokeza kupitia kiwiliwili cha dereva wake, Mzula ambaye tabia zao zinahusiana. Babu anamzindua K kuwa tabia zake mbovu za kuwakera na kuwadhulumu watu ndizo zinazoyafanya maisha yake yawe magumu. Hawezi kuenda kila pahali na pia anaishi akiogopa kila wakati. Ni kutokana na utu alio nao babu kwa K, ndiposa akamzindua ili aeweze kubadilisha tabia yake. Babu hapendi binadamu akimpapura mwenzake. Hapendi kero na dhuluma zozote. Hapendi kujitanua. Hana kiburi, yuko huru na hana faragano na mtu. Maisha ya K akilinganisha na maisha yao, anaona kuna tofauti kubwa ambayo ni ya tabia mbovu. Akimsuta K, K anakesha kumwambia kuwa hiyo ni dunia yao. Utu unaonyeshwa na babu kupitia mtazamo wake alionao kuhusu maisha ya binadamu.

K na babu yake bado wanaendelea na mazungumzo. Yuko kwenye limonsin yake. Babu bado amejitokeza kupitia dereva wake K, Mzula. Anamkumbusha K kuwa sasa amempata kupitia kwa dereva wake na ataganda pale hadi atakapomaliza kazi yake. K anaamini kuwa huo ni upuzi tu na ndoto ya muda ambao utakuja kupotea tu. Anataka amwone babu yake kwa kina na hivyo kumweleza kuwa anataka kumwona. Babu anamweleza asiwe na haraka ya kumwona. Kutotangamana kwa mzuka wa babu na K ni kwa sababu ya hulka mbovu ya K. K hana sifa za utu ila ni mzuka wa babu ndiye anadhihirisha matendo na maneno ya utu. Mazungumzo yao yanadhihirika hivi;

Kwa kweli nimekuja kukutatulia mambo si kukutilia tata mambo. Ndiyo maana sura yangu si muhimu kuliko kauli yangu...
Unataka kuniambia nini?

Usinikatie kutoweza mpaka ushuhudie kushindwa kwangu. Kama nikwambiavyo, dunia yetu si hai. Haidhuru hata kwamba unakoga katika mabafu ya maziwa na asali. Zaidi ya hapo, dunia iliyokuzunguka imejaa udhia! Nitakuonyesha mifano hatua kwa hatua. Kwanza furahia kishindo, kitetemeshi na msukosuko wa barabara. Kwa nini unajiachia kumezwa katika giza la vioo vyeusi vya gari visivyopenya mwangaza wala risasi? Ivue miwani ya jua uione dunia. Kwa nini unaogopa kuyaona mazingira katika kutokuwa na kuwa na hatia? Raha gani hiyo? Uhai gani huo? Wakati wa uhai wetu hata wale wabaya hawakuwa na sababu ya kujificha au kujitenga au kukimbia au kulindwa; kwa sababu walikuwa, kwa namna fulani sehemu ya watu wetu-lakini nyi... (Uk 23).

Hapa babu anaonyesha utu kwa kumweleza K kuwa maisha yake yana matatizo chungu nzima. Ila yeye, babu, amekuja kumsaidia K kutatua mambo yale. Babu anaendelea kumueleza ukweli kuhusu dunia yake. Dunia ambayo anaogopa. Anaishi duniani ila hawezi fanya chochote akiwa huru. Kila mara huhisi kuwa adui wake wanamfuata na kutaka kummaliza. Babu anamsuta ili aweze kubadilisha tabia na mienendo yake awe mtu mwema. Babu anahisi kuwa K ameishi maisha ya kujificha nyuma ya vioo vyeusi vya magari na nyuma ya miwani ya kuinga jua. Anahisi K hataki kuuchukua mwelekeo wa dunia ulivyo. Anahisi kwamba wakati wao katika dunia yao, wabaya walikuwa wabaya kwa kiasi cha kuweza kupata fursa ya kutangamana na wenzao.

Babu anakerwa na maisha ya K yaliyobadilika. Amekuwa katika tabaka ambalo kwalo hawezi tena kupatikana kwa urahisi. Anamtumia tu Mzula, dereva wa K ambaye ndiye sasa wa kiwango chake kumfikia K. Hapendi jinsi K ameishi maisha ya woga na ukiwa. Anamweleza K uhuru wa maisha yake ulivyo kwa kuwa yeye hajakosea watu.

Binadamu wakati mwingine huwa mnafiki. Huweza kukudanganya tu kuhusu mengi iwapo anafaidika kutoka kwako. Unapohitaji ukweli wa kukusaidia maishani, huweza kukufichia ukweli na ukaishia kuangamia. Kwa kawaida ukweli nao humdunga moyo binadamu kama mkuki. Mzuka hapa anamwambia K ukweli wote bila pingamizi yoyote. Mzuka, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), anamshauri K kuhusiana na mambo kadhaa. Babu, mzuka hana unafiki kama binadamu halisi. Anamshauri K kuepukana na mambo mengine. Anamwambia kuwa;

Fikiri K,” Sauti la mzuka sasa lilikuwa la kushawishi vya kutosha, “fikiri vipi ingekuwa kama vyakula hivi vina asili ya Kiafrika. Bila ya shaka ingekuwa hadithi ya kima na tumbili wa Zaire. Nadhani kila uzuri na ubaya wa kitu fulani katika dunia hii unatokana na msingi wa utajiri na umaskini wa watu wa asili fulani... Ukiwa na uwezo unaweza kukigeuza kitu chochote kibaya kuwa kizuri na dunia nzima itakuitikia hewalla, na tena kukufuata kuhalalisha visivyohalalishika...tena kukufwata kwa shangwe na gharama! (Uk 38).

Anamshauri K, kuepukana na tabia ya raha na wenzake na kutumia pesa kwa vitu vyenye thamani ilhali wengine wanaumia. Anamwambia K ajijali kwa yale watakayosema watu kumhusu. K na wenzake wapo kwenye Neo-Casino. Vyakula walivyoletewa ni kama Chatu wa kutokosa, nyoka wa kukausha, kijibwa kilichichomwa miongoni mwa mengine. Mzuka anakasirishwa na mambo haya na kumzungumzia K kwa hamaki.

Babu anamwonyesha K utu kwa kumshauri kubadilisha mienendo yake. Hataki mabaya yamtendekee K. Mzuka ni mhusika wa kiuhalisiajabu ambaye ana uwezo wa kuingilia maisha ya walio hai ili kuwaonya, kuwaelekeza na kuwaelimisha. Anamkumbusha K alivyobadilika kitabia, kihadhi na kifalsafa, kwani zamani aliwachukia matajiri na kuwaita mazimwi. Mzuka anamkumbusha K alivyoahidi kutumikia raia lakini ni msahaulifu na amebadilika hivi kwamba leo ni ‘msitu mpya na komba wapya’.

Mzuka anamshauri K kuwa anaweza kubadilisha mabaya yawe mazuri kwa kuwa ana uwezo. Anawaonea maskini huruma kwa madhila wanayoyapitia. Anaendelea kumweleza kuwa tabia yake njema itaweza kufanya watu wampende na wamfurahie.

Mzuka bado anamfuata K popote aendapo. Hachoki kumpa ushauri kama alivyochooka kumwona yeye K. Katika maisha ya binadamu, mtu hupewa ushauri na akachagua kwa hiari kama ataufuata ushauri huo au la. Wakati mwingine, anayepeana ushauri naye hufa moyo kuendelea na ushauri iwapo haoni mabadiliko yoyote ya mtu huyo. Mzuka hakati tamaa na anaendelea kumwandama K kumpa ushauri. Bado anamwonya kuwa;

Nimeshakwambia ... kukuasa, kukuonya na kukuonyesha yanayokuelekeeni, kama nyinyi ni waja wa kuonyeka na kusikia ... Pimeni m’nyofanya...

Sikatai... lakini usidhani unaweza kuachiwa milele kuchukua nyundo kuwagonga wengine, ati kwa sababu unataka kuridhisha utashi wako na kujimudu... Unaweza wakati kukuacha ujimudu hata maisha yako yote, lakini vizazi vyako havitadiriki kuendeleza uliyoyaanza wewe; na hasira za unaowafunda nyundo zitakuja kuwaangukia wao...(Uk 49).

Hapa K ameshatoka kwenye Neo-Casino. Yupo kwenye limonsin yake. Anafikiria kwenda kujiliwaza kwa Zuhura Mapozi ili aweze kumwepuka Mzuka. Babu mzuka mara tena anajigeuza kuwa dereva wake, Mzula. K anasinyika na kusonya anapomwona. Babu mzuka anamhakikishia kwamba hata asonye, hatomwamwacha katu hadi akamilishe kazi yake. Wanaingia katika

mazungumzo na K; mzuka bado anamshauri K kufikiria kuhusu vizazi vyake vya baadaye vitakavyoathiriwa na vitendo vyake pamoja na wengine wenye matendo kama yake.

Mzuka anamtembeza K katika dunia yao. Anampa ushauri jinsi enzi zao, watu walikuwa na moyo wa huruma kuliko enzi hizi za kina K. Kupitia ushauri huu, tunaona utu alionao kwa watu wa dunia hii, ya kina K. Mazungumzo yao yanabainisha utu kwa njia ifuatayo;

Dunia yenu ya dhulumu tupu K...

Kweli, sauti ya mzuka ilionyesha wazi hamu ya kuendeleza ulinganifu wake; wakati wetu ulikuwa na dhulumu pia... lakini wezi walikuwa na haya ya kujificha angalau nyuso zao. Siku hizi hakuna kujificha. Watu wanavikaukia vitu vya watu kwa mabavu. Desturi ya kistaarabu haipo tena, ile hisia ya mtu mmoja kwa mwingine. Kwamba uso umeumbwa na haya na kuna Imani na huruma. Madamu mtu ana nguvu sasa, anafanya apendavyo. Ndivyo ulimwengu wenu wote ulivyo. Kila mwenye nguvu husema kinywa kipana... Mnaniona? N'mependeza? N'nachukua ndiyo, liwalo na liwe- kwa jeuri! Wakati wetu watu wenye nguvu walijitahidi kujizuia kutochukua vile vitu pekee watu wengine walivyokuwa na'vyo. Hata wafalme walikuwa na adabu zao katika jambo hili (Uk 100).

Mzuka anaghadhabishwa na jinsi watu siku hizi wanatenda matendo hadharani bila kujali. Anaghadhabishwa na jinsi wenye uwezo, matajiri wanawanyasya maskini waso uwezo. Mzuka anashangazwa na jinsi binadamu amekosa utu kwa wenzake. Jambo hili si la kawaida. Ni kinaya kuwa mzuka ana utu kwa binadamu ilhali binadamu mwenyewe hana utu kwa wenzake.

Kutokana na mifano iliyojitokeza, Mzuka anadhihirika kuwa mfu anayetenda matendo yafanywayo tu na binadamu halisi. Mhimili mojawapo wa nadharia ya uhalisiajabu unaeleza kuwa sifa za uhalisia hukiukwa kama zilivyo zoeleka. Matukio yasiyoaminika na ya kifantasia husawiriwa, mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja kuonekana kana kwamba ni ya kawaida. Wanjiru (2013) anasema kwamba, katika jamii za Kiafrika, wazee wetu wakiwemo mababu zetu na nyanya zetu walikuwa na muda wa kukaa na wajukuu na wanao na kuwapa nasaha kuhusiana na mambo mbalimbali. Wajukuu wa kike walijiunga na nyanya zao na wa kiume wakaungana na babu zao. Inaaminika kuwa walikuwa na maarifa. Basi Mzuka, ambaye ni babu yake K, anatekeleza wajibu huo wa kutoa ushauri japo ni mfu.

Tabia ya kutoa ushauri kama sifa ya binadamu aliye na utu tunaipata pia katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Shaib na Ndi wamo barazani. Wanazungumza kuhusu hali ya dunia ilivyo. Shaib ni marehemu rafikiye Ndi, humzuru bado na huwa na mazungumzo ya mara kwa mara.

Shaib anasema kuwa:

Lakini watu hawatarajiwi kukaa tu na kufunga mikono... Shaib aliniambia Hakuna njia ya kuzuia nguvu hizi? Inaelekea hivyo, ingawa mwanadamu hapaswi kuketi na kukamata mikono tu kutazama ulimwengu unavyoangamia (Uk 48).

Wanazungumzia teknolojia na utandawazi ulivyoathiri dunia. Wanajadili jinsi vita vya dunia vya kwanza na vya pili vilivyoathiri dunia. Jinsi mataifa ya kimagharibi yalivyodharau Afrika. Wanazungumzia Afrika ilivyokosa uhuru wao kwa mikopo ya hela, misaada ya vyakula na vitu vingine, ingawa wao wanaona wana uhuru. Wanakasirika kutokana na jinsi mataifa hayo yanawatumia waafrika vibaya kisha kuwatema kuwa ni washenzi na hawana akili. Waafrika wanakuwa watumwa katika viwanda vyao. Wanatengeneza zana za vita zenye hatari kubwa kwa maisha ya binadamu. Wanahofu jinsi dunia siku hizi imetawaliwa tu na wenye uwezo na nguvu za kiutawala na sio na wenye akili tena. Hao ndio wanaohodhi utaratibu wa maisha, nyenzo za mawasiliano, elimu, sayansi, teknolojia, dini, usafi na uchafu wa mazingira yetu. Shaib, kupitia mazungumzo yake, anawatetea wanadamu haki yao. Anawazindua kwa kuwahamasisha wasikae tu wakingoja kudhulumiwa na wengine.

Ndi na Shaib wanashikilia kuwa ni makosa binadamu kuona jinsi ulimwengu unaangamia ilhali hakuna lolote awezalo kufanya. Kwao, binadamu anapaswa kujitahidi kukomboa dunia kutokana na maovu yake. Oruka (1990) anaeleza uovu kama hali ya kutokuwa na uadilifu. Uovu huhusishwa na matendo mabaya kama vile: ubaguzi, kuwaumiza au hata kuwadhulumu wengine kiasi cha kuwaathiri kisaikolojia. Ni uharibifu wenye nia ya kutia wengine machungu na mateso yasiyo na kifani. Uovu ni kufanya mambo kinyume na matarajio ya wanajamii. Dunia imejaa maovu chungu nzima. Kila uchao mwanadamu anamwangamiza mwanadamu mwenzake kupitia mikono yake mwenyewe, silaha butu, silaha za vita, teknolojia na mengineyo. Kila siku kwenye habari matukio yanatangazwa ya kusikitisha, wazazi kuua watoto, wachumba kuuana, wanafunzi kuumiza walimu shuleni, vita vya kikabila na hata vita vya mali. Mambo haya kwa kweli yanafaa kukomeshwa na ni binadamu mwenyewe aweza kuyakomesha.

Mara kwa mara mzazi hujitokeza kumpa mwanawe nasaha popote ahitajipo. Nasaha haswa hutolewa kwa binadamu anapoonekana kuenda kinyume na matarajio au anaposumbuliwa na mawazo Fulani ambayo huweza kubadilisha tabia zake. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*

(2010), Mamake Nana hujitokeza kwake mara kwa mara. Huja kumpa nasaha ajitayarishe kuhusu maisha yake ya mbele. Nana anaeleza kuwa;

Sherehe ya leo ililazimishwa kama zilivyolazimishwa sherehe zangu zote. Hasa kwa vile ilichanganyawa na kuwa kwangu mtu mzima. Ingawa hilo halikutangazwa, maana ilikuwa siri ya familia yetu. Isitoshe, mama Bi Mkubwa alinijia usiku (siku hizi anafululiza kunijia) kunambia kwamba mkusanyiko wa watu ni mafunzo ya kujilinda. Basi ningewezaje kuipinga sherehe hii? Labda ningesoma mambo zaidi ambayo yangenisaidia baadaye nikiishi pekeyangu (Uk 32).

Nana hapendi sherehe nyingi zinazofanywa na babake. Sherehe za walala hai tu. Sherehe kubwa iliyo na kila aina ya chakula ilhali majirani tu walio karibu nao, waliowauzia kipande cha ardhi wanakosa chakula. Sherehe sasa inataka kuandaliwa kwa sababu Nana alivunja ungo na sasa amekuwa mtu mkubwa. Nana hapendezwi na jambo hilo. Mamake anamtokezea na kumweleza kuwa mkusanyiko wa watu ni mafunzo ya kujilinda.

Wazazi huweza kukasirikia watoto wao baada ya watoto kufanya maamuzi fulani. Haya hutokea haswa kama ulishauriwa kufanya hivi ukafanya vile. Aidha, huweza kuendelea kupeana nasaha kwa wanao hata baada ya maamuzi mbovu kufanywa ili aghalabu pawepo na mabadiliko. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), marehemu mamake Nana anajitokeza kwa Nana. Amekasirika na uamuzi wa Nana kuolewa. Anamgombeza kwa kusema;

Kwa nini hutaki kunisikia? Kwa nini enh? Kwa nini wewe huambukizi? Ni mkaidi kama babako ...Unataka kuolewa, hujui kwamba kuolewa ni kudhibitiwa na mwanaume? Umetoka kwa balaa la babako kukudhibiti kama alivyotaka kunidhibiti mimi, sasa umeingia katika mikono ya dhibiti ya mwanamume mwingine asiye babako wala mtu wako? (Uk 287).

Kwa kutotaka mtoto wake Nana ajiingize katika asasi ya ndoa, mamake anaonyesha kumjali mwanawe kwani hataki akijitosa katika matatizo yanayotokana na ndoa. Alipojitokeza, alikuwa amekasirika sana. Anamzungumzia Nana kwa ukali sana. Amekuja kumnasihi Nana aachane na mahusiano ya ndoa. Hii ni kwa sababu alipitia mengi katika maisha ya ndoa. Marehemu mamake Nana, anamsihi aachane na mambo ya ndoa kwa kuwa yeye aliteseka mikononi mwa mwanamme. Anamwelezea kuwa hata huyo Faisal aliweza kumtoroka alipojua kwao. Anahisi kuwa mwanee Nana hajui chochote kuhusu wanaume ama ndoa. Kumjia mwanaye na kumpa ushauri na maarifa

kuhusu ndoa ni kitendo cha utu kama anavyoeleza Gilbert (2010) kuwa sifa za utu ni pamoja na maarifa.

Jamii imekuwa, ikiendeleza elimu ya jadi ya kwa kutoa maonyo, kutoa nasaha au kutahadharisha kuhusu masuala yenye madhara. Vile vile, hutumia mbinu mbalimbali kama nyimbo, zenye dhima ya kuelekeza mambo mema yafaayo kutendwa na mambo maovu yanayopaswa kuachwa. Nasaha hutolewa kwenye maisha ya kila siku ili kupata jamii iliyo bora. Maisha yanaongozwa na maneno yenye hekima kwa kuonya, kutahadharisha na kuelekeza.

Mzazi kila mara humpa mtoto wake nasaha na ushauri utakaomsaidia katika maisha yake ya hapo usoni. Anamfunza Nana jinsi ya kuishi na wenzake. Hapo mbeleni Nana anakuwa na ujasiri wa kuimba na kucheza densi mbele ya umati mkubwa wa watu.

4.2.3 Kupenda Amani

Kupenda amani ni sifa nzuri sana katika maisha ya binadamu. Binadamu anapoishi kwa amani na wenzake, huishi vizuri. Hii ni ina maana kuwa huweza kupata msaada wa aina yoyote ile kutoka kwa wenzake. Bila Amani, watu huishi tu kwa vita na ugomvi vya kila wakati. Huleta madhara mengi ikiwemo kujeruhi watu, vifo vya watu, kupoteza mali na hata kufanya watu wahame walikoathiriwa. Kupenda amani na kuishi kwa amani huwa na athari chanya katika jamii.

Babu ni mpenda amani. Katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), babu anaishi katika dunia iitwayo amani. Anapenda dunia yao akikumbuka walivyoishi kwa amani, tofauti na sasa ambapo dunia yao haina Amani. K hana Amani maishani mwake kutokana na tabia zake mbovu za mabwenyenye alio nao. Kila anapoenda mahali anafikiri tu anafuatwa na adui. K na wenzake wako kwenye Neo-Casino. Mle ndani mazingira yanadhihirisha hali ya ufahari. Wale wateja wanaozuru hapo si wateja tu wa kawaida, ni wateja wenye mali na wenye kuishi maisha ya kifahari. Wenzake K wanamsubiri aje, anapofika mle, wanamlaki kwa kushangilia na kumpigia makofi. Anajilazimisha kucheka kwa kuwa anapitia wakati mgumu na mzuka wa babu yake ambaye kila mara anamkosoa kuhusu tabia yake na maisha yake anavyoishi. Kwa sababu ya utu alionao kwa kilembwekeza wake, ndio maana akamshauri kuhusu maisha mabaya ambayo amechagua kuishi. Si kama walivyo ishi wao. Anamwambia kuwa:

Haya tu ndiyo yanayokukausha roho na kutaka kuendelea na kiu yako milele...haya tu ndiyo yanayokausha kila punji ya ubinadamu wako, pesa...fahari...ulwa...nguvu...! (Uk 30).

Babu anasikitika jinsi maisha ya K na rafikize ya kifahari yamemfanya abadilike na kutokuwa na ubinadamu. Tabia za K zimebadilika kwa sababu ya maisha ya kifahari anayoishi. Kwake yeye, maisha aliyokuwemo K, ilikuwa maisha ya kuwasaidia wale ambao hawajiwezi kwa njia mbalimbali.

K na mzuka wapo kwenye dunia inayoitwa Amani. Mzuka ameamua kumtembeza K katika dunia hiyo ili aone jinsi watu wanavyoishi bila amani licha ya nchi hii kuitwa Amani. K analalamika. Mzuka anatomika ili kumshauri K ili aepukane na maisha ya kibinafsi kama anavyoeleza (Faris, 2004) kuwa, uhalisiajabu inahusishwa na visasili vya utamaduni wa wazawa na hivyo kuepukana na utamaduni wa kimagharibi wenye kumakinikia ubinafsi. Babu anamkemea kwa kumwambia kuwa;

Wewe unaogopa kufa kwa siku moja, huku kuna kufa kila siku... kama si kisu, panga; kama si rungu, risasi; kama si kupigwa dafrau na gari hata kabari... au hata dhii ya maisha... Alimaka mzuka.

Sawa, kila mtu ana haki ya uchaguzi... alijibu K kwa puruzai na jeuri.

Wewe una haki, wengine hawana... wewe una uchaguzi, wengine wana upaguzi tu... Aaa! Nilitaka uone tu, sasa twen'zetu (Uk 133).

K anataka kurudi nyumbani baada ya kutembea na kushuhudia matukio ambayo yalitisha maisha yake. Anaona jinsi watu wanavyouana kwa njia nyingi. Anaogopa kifo. Mzuka anamshutumu kuwa yeye anaogopa kifo ilhali haogopi wengine wakifa kwa ajili yake. Haya yote anayomfanyia K, yalipasa kumsaidia K kujibadilisha kitabia na kuwa mtu mwema.

Amani ni muhimu katika maisha ya binadamu. Hata watoto hutambua panapo amani au vurugu nyumbani. Kila mtu hufurahia kukaa katika mazingira ya amani. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006) Kilua, mtoto wa Ndi anaonyesha kutoridhika kwa suala la babake kunyamazia watoto wake. Anataka amani iwe kati yao na babake. Anauliza;

“Kwa nini baba siku hizi hutaki kusema na mimi? Hutaki kusema na mama, na dada Yungi, na kaka Bori na Kaka Jitu na kaka Dubwa... husemi na yeyote,” aliendelea “Nilishindwa kumjibu. Nilitaka lakini kauli haikunitoka.” (Uk 59).

Kilua ametambua kuwa hapana amani kati yao na babake. Anajaribu kutatua kilichotokea kati ya babake na wao. Kilua anatambua kuwa babake hana jibu na hivyo anabadilisha mada. Ni mpenda amani. Anataka amani iwe kati ya babake na familia yao. Anaomba awe karibu na babake alivyokuwa zamani.

Vilevile, Bi M, mkewe Ndi, anapenda Amani katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006). Anataka kumweleza Ndi kuwa Kazi afanyayo Yungi mwanawe si nzuri mno.

... Niliona niseme naye kwanza... Najua moyoni umejaa tashfani nyingi mno. Sikutaka kukutwika mzigo mwingine juu ya mzigo ulio nao tayari (Uk 23).

Bi M anamjulisha Ndi kuhusu kazi ya Yungi. Hakutaka kumweleza tu bila ya kusikiza kutoka kwa Yungi. Baada ya kuhakikisha kazi afanyayo Yungi, ndiposa akaweza kumwelezea mumewe Ndi. Ndi anaamua kumsubiri Yungi. Yungi anaporudi panatokea mzozo na Bi M anajaribu kutatua mzozo huo. Anasema kwamba;

Hakuna cha mila au desturi. Hakuna mswalie mtume wala mswalie nini. Alisita.
We Yungi, Bi M alibwata “Unamjibu nani maneno hayo?”
Nyamaza nawe, alimgeukia mamake
Kibao kilialika katika kimya ya alfajiri na kuamsha wote waliokuwa wamelala ndani...
(Uk 27).

Bi M anamzaba Yungi kofi kama mamake mzazi. Yeye kama mzazi anataka amani iwe kati ya baba na mwanawe. Anakasirika na kumhukumu Yungi na kumkemea kwa kumwambia amekosa heshima kwa babake.

Ingawa sifa ya amani na utulivu huhusishwa tu na binadamu hai, viumbe wa kiuhalisiajabu pia wanapenda amani. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Bi Mkubwa, marehemu mamake Nana ana penda amani. Anapomtokea Nana, anamhadithia alivyotoroka mumewe wa pili. Anamhadithia kuwa;

Baada ya muda mfupi tu wa kuolewa na Simai, Bi Mkubwa alitambua amekutana na mpenda-kupiga-wanawake. Mara leo Bi Mkubwa alipigwa kibao akavimba uso kwa sababu kachelewa kupika. Kesho alivimba mdomo kwa kibao alichozabwa nacho bila hisi wala huruma. Mara kesho kutwa alivunjwa mkono kwa dhoruba ya mwanamume huyo asiye na uonelevu wa aina yoyote (Uk 288).

Kutokana na dondoo hili, Bi Mkubwa, alipofukuzwa na babake Nana, alimpata Simai, mchuuzi wa samaki. Mwanamme aliyependeza. Walikutana pale mnadani. Alikwenda kuishi naye na

akajikuta ameishi na mpiga wanawake. Alikesha kupigwa siku nenda siku rudi. Bi Mkubwa aliamua kutoroka na kuenda kuishi mbali na huyo Simai. Alitoroka kutafuta Amani maishani mwake.

4.2.4 Heshima

Heshima ni staha, adabu, nidhamu aliyonayo mtu kwa mwingine (TUKI, 2013). Katika maisha ya binadamu heshima ni tabia muhimu zaidi. Kila binadamu anapaswa kumheshimu mwenzake, wadogo kwa wakubwa, wazee kwa vijana, wake kwa waume na yeyote yule anayehusiana na binadamu mwenzake. Ili uweze kupokea heshima kutoka kwa mtu fulani, ni sharti nawe pia uwe unamheshimu.

Heshima ni nzuri kwa kiumbe yeyote yule. Si kwa wazee si kwa vijana, si kwa watoto si kwa watu wazima, heshima ni nzuri ikiwepo. Mzuka katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), anampa K heshima zake. Anamwambia kuwa;

La, sitakuharibia usiku wako, alimsikia yule mzuka akisema (Uk 35).

Hataki kumharibia usiku wake wa raha na rafikize. K anakaribia kukata tamaa kutokana na yale matukio. Anahisi ayaache tu yatendeke kama yanavyotaka ila tu yasiharibu usiku wake. K anapofikiria hivi, mzuka naye anamhakikishia kuwa, hataharibu usiku wake. Mzuka anampa K muda wake wa kulala. Anajua uzuri wa kumpa mtu heshima zake. Kutomharibia K usingizi unaashiria heshima zake.

Katika jamii ya Waafrika, (Mbiti, 1990) anaeleza kuwa kazi zilikuwa zimegawiwa kulingana na jinsia. Palikuwepo na kazi za kulinda boma, kuleta chakula, kuwaelekeza watoto wa kiume, kuchunga mifugo na hata kupasua kuni ambayo yaliachiwa watoto wa kiume. Kazi kama kusafisha nyumba na mazingira yake, kuosha vyombo, kuteka maji, kupika vyakula kutunza watoto na mengineyo yalikuwa kazi ya watoto wa kike. Hili linadhihirika wazi wakati Yungi na babake katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), wanazozana kuhusu kazi za wake kwa waume. Bi M anaingilia kati kudumisha amani. Mazungumzo hayo yanadhihirika hivi;

Mimi nimepevuka kidogo kwa sababu nimejifunza. Ni kijana kwa sababu sehemu yangu kubwa ina vitu ambavyo watu waliopevuka Zaidi kuliko mimi wamenifunza. Zile tope machakavu zilizoganda kwenye kiatu mimi.

We Yungi, unamjibu nani maneno hayo? Alimaka Bi M.

Nyamaza na wewe, alikuwa kapandwa na pepo alipomgeukia mamake, kama miaka yote hii umeshindwa kumzuia bwana huyu kuwa mwamba katika nyumba hii... (Uk 27).

Yungi, Ndi na babake katika dondoo, wanazozana kuhusu kutafuta riziki kwa njia isiyo halali. Ndi, babake Yungi anaona si njia halali kwa kuwa anajikimu kwa njia ya ukahaba. Yungi anafikiria kuwa kazi ni kazi, haidhuru ni kazi gani. Anahisi kuwa wakati umefika ambapo dunia imebadilika na mwanamke hapaswi kumngoja mwanamme kutafuta riziki. Kuzozana huku kunadhihirisha utovu wa heshima ya watoto kwa wazazi. Kupitia heshima ya Bi M kwa mumewe, utu unajitokeza. Hataki mtoto kumkosea heshima babake. Heshima hii inajitokeza Yungi anapomkosea heshima babake kwa kumjibu kwa maneno makali kasha Bi M anamkataza kwa sauti ya juu.

Ni jukumu la wazazi kuhakikisha kuwa wanao huwa na heshima kwao na kwa wakubwa wao. Hivi tunamwona Bi M akichukua jukumu lake kama mama mzazi kumkaripia mwanao Yungi anapozungumza na babake vibaya.

Wanajamii pia wanapaswa kuwa na heshima ya mtu kwa mwenzake. Katika riwaya ya *Nyuso za mwanamke* (2010), Bi Mkubwa, marehemu mamake Nana alikuwa akimheshimu Faisal. Kupitia barua yake Bi, Mkubwa kwa Nana, heshima yake Faisal inajitokeza kama tunavyoona katika dondoo lifuatavyo:

Mwanamme huyu alikuwa mfano wa binadamu... Niligundua kuwa ni tofauti na wanaume wengine. Hakusoma tu bali amelimika kuhusu uhusiano unaotakiwa uwepo baina ya mtu na mtu- mwanamke na mwanamme, mwanamke na mwanamke, na mwanamme na mwanamme (Uk 173).

Bi Mkubwa ana heshima kwa Faisal kwa kuwa tabia zake hazikufanana na za wanaume wengine. Alikuwa mwanamme aliyependa kwa dhati. Bi Mkubwa anaeleza kuwa alikuwa na elimu hadi ya kihusiano. Mapenzi ya Faisal kwa Bi Mkubwa hayakuwa na mpaka. Bado alimtumia vijipesa ambavyo aliweka kwenye benki na ndizo zinamsaidia Nana kwa sasa.

4.2.5 Hekima

Binadamu ana hekima. Hii ni hulka mojawapo aliozawadiwa na Maulana. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), Babu ana hekima. Kama mzee aliyeishi miaka mingi anaelekeza kwa kusema hatari itakayotokea. Ana uwezo wa kutafakari na kuona yatakayotokea hapo mbeleni. Anatomia hekima yake kumwonya K kuhusu mradi wao wa burudani. Anasema:

Lo, lo, lo...” alimaka babu mzuka, “unaingia huko tena K? Ama kweli... ubuku umekushika kiasi hicho... Basi itafaa klabu yenu muipe jina la kienyeji...Iteni ‘Giningi’ au ‘Uchawini’ badala ya FKK... Hata nyinyi wengine mliofyodoka matumbo na vitambi vilivyosokotana mtakuwa upeo wa sanaa? Mtakuwa na haki kuwaonyesha kuchusha kwenu watu wengine? ... Basi m’naonekana m’ko tayari kuzipokea haki zote hizo taratibu katika unyamavu, maadamu tu zinakamatana na pesa... shabash! (Uk 44).

Babu mzuka katika kuonyesha kuwa kutoa nguo hadharani si ustaarabu. Kulingana na Babu, kutembea uchi ni unyama. Ni wachawi tu au wenye akili tahira ambao hutembea uchi. Binadamu aliye na akili timamu hapaswi kuonekana uchi. Ni hekima aliyo nayo babu ndio inafanya awe na mtazamo huu.

Ni jambo la kawaida kina babu kuwa na utu kwa mjukuu wake. Ingawa ni sifa inayopatikana tu kwa watu wachache, wengine huidhihirisha sifa hii ya utu. Kwa sababu hii babu anatomia hekima zake kumwonya K, dhidi ya mabaya yatayomtokea hapo mbeleni. Anamtakia mema maishani na hivyo kumsaidia kwa mawazo mapana.

K na wenzake bado wanaendelea kujadiliana kuhusu miradi mbalimbali wanavyofaa kutekeleza, mengi yanajadiliwa lakini ule wa mradi wa FKK ndio unashika kani. Wanataka kuanzisha klabu ya FKK ya burudani ambayo watakaozuru watakuwa wakiingia huko uchi. Babu anamtahadharisha K. Anasema kuwa:

K mengi yanakuja; inafaa mjitayarisha. Msiwe tu mnavaa miwani ya kutoona kesho. Kesho vitukuu na vinying’inya vyenu vitavyozama katika mashakili makubwa... Kutakuja tupwa takataka za sumu... Ardhi na viwanja vyenu vtauzwa na jambo hilo litaleta matatizo makubwa. Vijana wenu watakoga na kujitapakaza unga na mtakosa mabarubaru wa kufanya kazi. Jambo hilo litaleta msiba mkubwa. Watoto watakaokuja zaliwa wakati huo watakamatwa kuenda kucheleshwa unyago wa kinyama huko ng’ambo. Nyinyi mu dhaifu hivi mlivyo sasa, na mtakuwa dhaifu zaidi kesho. Na bila ya shaka mtakuwa ngawira rahisi.” Alisita hapo na ukimya ukatawala (Uk 51).

Katika dondoo hili, maneno ya Babu yanaonyesha hekima aliyonayo. Anampa K ushauri kuhusiana na umuhimu wa kuwa na akili tambuzi kuhusiana na maisha. Anamwelezea kuwa awe mtu wa kufikiria maisha ya mbele. Anawaonea vizazi vya baadaye huruma kwa watakayoteseka kutokana na dhambi za wazazi wao. Anamwambia K kuwa wasipochunga, sasa watafurahia lakini baada ya muda watalia.Mzuka anaendelea kumtahadharisha K. Anamtahadharisha kutokana na tabia mbaya ya ukengeushi na mabadiliko waliyonayo. Mzuka anamwelezea K kuwa watu kama yeye wamekengeuka wakawa wanawadhulumu watu wenye rangi kama wao. Watu wamekengeuka kiasi cha kutaka kubadilisha maumbo yao na vipodozi. Mabadiliko yamekuwa ya

watu fulani kutumia wenzao na akili za wenzao kujitajirisha bila kujali maslahi ya wengine. Mzuka anahisi vibaya kwa kuwa mabadiliko yamekuwapo tu ila ni ya kuwadhalilisha wengine.

Hekima kwa kawaida ni sifa inayohusishwa na binadamu. Sifa hii aidha, inapatikana kwa sauti ikimwonya Ndi. Ndi katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), alipokuwa pale msituni, kila mara alisikia sauti likimwonya na kumwongoza bila kuona ni ya nani au nini. Hivi, hangeweza kuangamizwa pale msituni. Sauti inasikika ikisema:

Ndi- mbele yako kunakuja dhoruba na vumbi, fumba macho. Kimbia! Usirudi nyuma!” Nami nilifumba macho na kukimbilia mbele. Mara kwa mara nilijikwaa au kugongana na mpitanjia au baiskeli iliyokata vichochocho pasi na mwendeshaji. Mara nyingine nilihisi alikuja mtu aliyeniongelesha nifanye hivi au kunionya nisifanye vile. Nilipomtafuta, sikumwona. Sikumjua mtu gani wala sikuweza kutambua kama alikuwa mtu kweli au la (Uk 70).

Hekima iliyoko katika lile sauti linalomwonya Ndi, linalisaidia kuongoza Ndi kutokana na mabaya atakayoyakumba. Sauti lile Ndi analifuata bila shaka na kunusurika.

Vilevile, hekima inadhihirika vilivyo katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, (2010) Marehemu mamake Nana humtahadharisha wakati mwingi jambo mbaya linapomkabili. Ingawa husonya na kulalama, mwishowe husaidika kwa kuuepuka hatari hiyo. Kutokana na utu na upendo alionao kwa mwanawake Nana, anamtahadharisha ili kuepuka hatari yoyote maishani mwake.

Mara nyingine wewe huja ghafla kunigutua kwa jambo la hatari ninalolikabili – name hushukuru. Mara ngapi umenivuta bega kwa haraka ninapopigwa na bumbuwazi huku gari liko mbele yangu tayari kunimaliza? Au pale mpanda baiskeli alipokosea kunizoa na kunitupa chini kunionya mauti na baadaye kunikaripia... Mara nyingi hukumbuka pale unapofurutu ada. Pale unapokuja kuninyukua au kunizaba kibao ili kunizindua na hatari inayonikabili. Nami hujua ni wewe, kwani hapana mwingine ambaye angethubutu kunikamata mkono kunivusha barabara ya hatari. Na ingawa hulalama na kulaani huku nasugua mchonoto pajani au shavuni, hujikuta hatimaye nimeonyeka. Nimenusurika. Nimeepuka hatari (Uk 18).

Kutokana na miaka aliyoishi humu duniani marehemu mamake Nana ana hekima. Anaweza kuashiria kile kitakachotokea hapo mbeleni na kumwonya mwanake Nana.

Marehemu mamake Nana anaendelea kutumia hekima yake kumtahadharisha Nana katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), anajitokeza kwa sura ya kigeni kumwonya kuhusu mwanamme. Anamweleza jinsi mwanamume ndiye kiumbe mbaya kabisa humu duniani kulingana na maneno yake yafuatayo:

Kwa nini hutaki kunisikia? Kwa nini enh? Kwa nini wewe huambiziki? Ni mkaidi kama babako ... Unataka kuolewa, hujui kuwa kuolewa ni kudhibitiwa na mwanamume? Umetoka kwenye balaa la babako kukudhibiti kama alivyotaka kunidhibiti mimi, sasa umeingia katika mikono ya dhibiti ya mwanamume mwingine ambaye si babako wala mtu wako. Umeingia katika dhibiti ya mwanawe Faisal, wewe unamjua Faisal au huyo mwanawe? Faisal alinikimbia pale alipojua kwao. Alihalifu miadi tuliyoweka... Enh, wewe unajua nini kuhusu wanaume? Unajua nini kuhusu ndoa... ngoja mimi nikwambie (Uk 287).

Anapojitokeza kwa sura ya kigeni, mambo huwa mabaya. Anapojitokeza kwa sura ya kienyeji mambo huwa mazuri. Anapojitokeza kwa sura ya kigeni, alimsukuma Nana, akatokatoka na kuingiaingia chumbani mwa Nana, akaanza kuhaha pumzi zikimtoka midomoni, macho yake yakawa mekundu, akasema maneno yasiyofahamika. Alisema lugha ya kuzimu. Akaanza kugwara alichokutana nacho kwa kucha zake ndefu, kisha akatoa ukwenzi wa kishetani. Alipomaliza haya, sasa angeweza kusema maneno kwa lugha inayofahamika. Mamake Nana anamwonya kuhusu mwanamme. Anamweleza alivyotawaliwa na wanaume maishani mwake na kuishia kuwachukia milele. Makumbusho haya yanaafikiana na mawazo ya (Zamora & Wendy, 1995), akieleza mojawapo ya mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu inayosema kuwa; Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Jambo hili hufanywa kwa kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Mwandishi hutumia mbinu rejeshi kuvunja mtiririko wa vitushi Utafiti hivyo imeweza kurejelea matukio rejeshi.

Kutokana na maisha aliyopitia mikononi mwa mwanamme, hataki mwanae Nana apitie maisha kama hayo tena. Anamwonya Nana kutokana na kuolewa, hii ni hekima inayojitokeza kutokana na maisha mengi aliyojifunza kwa wakati wake. Mojawapo ya methali za Kiswahili ambayo hurejelea hekima ya mtu huwa 'Kuishi kwingi ndiko kuona mengi'. Kutokana na methali hii, hekima ya Mzuka, babuye K na marehemu mamake Nana unadhahirika wazi katika madondoo yaliyoendelezwa.

4.2.6 Msamaha

Binadamu huhitaji kusamehe mwenzake. Katika Bibilia takatifu, tunaelezewa kuwa msamaha ni kitu muhimu sana. Hata Yesu anapowafunza wanafunzi wake kuhusu maombi, anasema tuwasamehe watu kama walivyotusamehe. Bibilia inatuhimiza tuweze kuwasamehe wenzetu kabla Mwenyezi Mungu hajatusamehe.

Ni jambo bora katika maisha ya binadamu, binadamu kumsamehe mwenzake. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Dubwa, anamsamehe babake kwa kutenga familia yake. Anamsamehe kwa kuona kuwa anaikimbia makusudi jukumu lake. Dubwa anamwambia;

Kwani hujasikia kulaumiwa wewe? Dunia nzima inakusema kwamba umeitenga nafsi yako. Kisha ukatenga nafsi ya mama watoto wako. Wanaona unajitia wendawazimu wa makusudi kukimbia dhamana na jukumu lako. Tutubu kwa Mwenyezi Mungu wetu (Uk 139).

Dubwa anamsihi babake atubu kwa Mwenyezi Mungu. Ili kupata msamaha, mtu hupaswa kutubu matendo yake. Hivi, naye anamsamehe babake. Ni vyema kuwa na moyo wa msamaha.

Bori pia anamsamehe babake Ndi. Anamkumbusha nafasi alizopaswa kupewa ila hakupewa. Anamwambia kuwa;

Hukunipa nafasi. Na kwa sababu hukunipa nafasi, nilichukia masomo. Ndiyo maana sikufanya vizuri. Sikulaumu lakini. Nyinyi wazee mmekulia dunia yenu na sisi nyingine (Uk 115).

Hataki kumlaumu babake kwa kuteseka kwake. Anajilaumu kwa kuwa hakusoma alivyotakikana kusoma. Anajiambia ya kwamba angesoma angefaidika kwa sasa. Anamaliza kuzungumza na babake kasha anaruka na kurejea kwenye albamu.

Msamaha katika jamii hujitokeza kwa njia mbili. Mtu huweza tu kuamua kumsamehe mwenzake au aliyekosea kumwomba aliyekosewa msamaha. Hivi, katika riwaya ya *Nyuso za mwanamke* (2010), Nana anaomba msamaha kwa Faisal. Hii ni kwa kuwa wamekosa kuelewana na Faisal kuhusu marehemu mamake Nana. Nana anasema;

Nimekuja kukutaka samahani ... Nisamehe...nisamehe sana kwani sikukusudia hivyo (Uk 254).

Nana alikuwa akimwelezea Faisal kuhusu kumwona marehemu mamake katika harakati zake. Alikasirika Faisal alipomwambia kuwa yeye hamwoni mtu yeyote ilhali yeye Nana alikuwa akimwona marehemu mamake akijitokeza kila wakati.

4.2.7 Utoaji Msaada

Kutoa msaada ni muhali kwa binadamu. Aghalabu kila binadamu kwa wakati fulani huhitaji msaada wa mwenzake. Binadamu humnusuru mwenzake kutoka katika hali fulani akiwa

amekwama. Huweza kunusuriwa kwa njia tofauti. Kwa mfano kumsaidia mtu na hela anapofungiwa hospitalini kwa kukosa kulipa ada ya hospitalini, kumwoko a anayezama majini au hata kumwoko a jambazi kutokana na umati wanaotaka kumuua

Akichangia kuhusu falsafa ya Ubuntu, Mugumbate (2013) anaeleza kuwa, mtu huweza tu kuongeza mibaraka yake kwa kusaidia wenzake katika jamii na hivyo hata kuinua hadhi miongoni mwa jamaa, (Mugumbate, 2013). Mugumbate anaendelea kusema kuwa, matendo ya Ubuntu hujitokeza kama vile kuenda kuwaona wagonjwa ambao hata si jamaa yako, kutuma rambirambi kwa waliofiwa, kupeana chakula kwa wasioweza kupata, kuwasaidia wazee na hata kusalimia watu kwa njia ya upole. Mawazo haya yaliweza kufaa utafiti kwa kuwa, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), K anapata usaidizi wa kufika dunia nyingine. Dunia ya kina babu mzuka. K hakuweza kufika peke yake, lakini kwa usaidizi wa babu mzuka, aliweza kufika katika dunia hiyo. Msaada huo unadhihirika hivi;

Twende...

Wapi?

Mzuka hakujibu, wala K hakumaizi. Alijikuta tu akikamatwa mkono na'ye na kutokuwa na budi kufuata.

Kwanza, nataka uvue miwani yako ya jua ... Kisha nataka uvae figu hili mpaka n'takapo kwambia ulivue. Tatu, nataka ujiue. K alijikaba roho na kujiua.

Sasa twende, mbele ya safari utaona mengi. Unapoona chochote, kile usije ukavua figu lako mpaka nikwambie ...

Sawa K alijibu (Uk 83).

Maelezo haya yote anayopewa K ni kwa manufaa yake. Mzuka anamsaidia kwa kumwongoza safarini kote. Mzuka anamsaidia katika dunia ya ugenini. Hataki K aathiriwe kwa njia yoyote ile katika dunia yao. K na mzuka wanazuru dunia ya kina mzuka hadi wakati ambapo ziara inaisha. Kutokana na usaidizi wa mzuka, anamaliza ziara bila tatizo lolote.

Usaidizi hujitokeza katika sehemu nyingi ikiwemo, nyumbani, barabarani, hospitalini, shuleni, baharini na mahali popote mle. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi amekwenda matembezi pale baharini. Alipokuwa pale akahisi kupiga mbizi mle baharini. Aliingia baharini na baada ya muda akalemewa kupiga mbizi. Akaamua kuomba usaidizi. Bi Muse tena anajitokeza kumwoko a kutokana na mawimbi yale makali.

Nazama?

Hapana!

La! Siendi juu wala chini kamwe. Siendi nyuma wala mbele. Nimo tu naelea ndani ya maji. Ghafila lakini mkono wangu unashikwa. Hisia. Ujomnyosi. Mkono wenye nguvu za raha, unanivuta juu huku muziki wa tango unanitumbuiza. Muziki wa piano. Je, Bibi wa Bucarest, Dana Protopopescu mwenyewe? La, Siye! Alikuwa Muse- Mize!” (Uk 169).

Ndi anaingia baharini na kukutana na pandikizi la mtu. Mtu yule amewafunga samaki-mtu ambao wanalalamika kuwa wameshikwa bure. Katika harakati ile, jitu lile tena linashika samaki-mtu mkubwa kwenye nyavu. Mvuvi huyu anakazana kumkamata samaki-mtu ambaye anauka juu na kusababisha dhoruba. Samaki yule anaposhikwa, wengine wao wanafurahia kwa kurukaruka na kusababisha mawimbi. Mawimbi yale yanamwelekea Ndi, anajaribu kila awezalo kufika ng’ambo ya pili. Anashindwa, anachoka, anaishiwa pumzi na hatimaye fahamu zinampungua. Bi. Muse anamsaidia Ndi anayezama. Ndi anazama kimawazo na kitaaluma. Bi. Muse anakuja kumsaidia kujilimbikiza katika ulimwengu wa uandishi wa kiuhalisiajabu. Ni vyema kumsaidia mwenzako.

Vile vile, usaidizi huweza kutokea kwa kiumbe yeyote yule akiwemo binadamu au mnyama. Nyakati zingine, wanyama kama mbwa wamesikika wakisaidia kwa kutambua alipotupwa kijusi, au hata husaidia kulinda watu usiku. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Kitoto cha miujiza kinamwonea babake huruma kwa kufungwa na kusingiziwa kuwa na wazimu bure. Anasema fika kwamba, siku moja atamkomboa babake na kilamtu. Ukombozi huu utajitokeza tu kwa kusaidiwa. Kinadhihirika hivi;

Wallahi’ adhimu hivyo, usidhani nakizulia kimalaika cha Mungu... juzi, juzi ya kijomba, niliskia kama kinaniita- ‘Mama, mama, yu wapi baba?’ Nikashtuka. Kitoto cha miezi mitatu kitawezaje kusema? Kitawezaje kuuliza na kumtaka babake? Lakini usiku nilipokuwa nikilaza tena kikaongeza, ‘Najua baba kafungwa. Najua kasingiziwa kua na wazimu bure, lakini mimi nitakuja kumkomboa siku moja. Nitakomboa kila mtu! (Uk 197).

Kitoto hapa kama binadamu pia ana hisia ya utu. Kitoto kile kinataka kumsaidia babake, ana imani ya kumkomboa babake kutoka kwenye jela ya kusingiziwa. Kila mtu pale kijijini anasema kuwa Ndi amekuwa mwendawazimu. Hii ni kwa sababu amekuwa akiishi maisha ya upweke bila familia yake. Jambo hili linaonyesha uhusiano wa dhati kati ya baba na kile kitoto. Kezilahabi (1976) anasema kuwa waandishi wengi wa Kiswahili hujishughulisha na Utunzi wa kazi za fasihi kufuatana na matatizo au ufunuo uliowafikia wakati huo, au kufuatana-na mkondo wa wakati na mabadiliko yake. Hivi ni kumaanisha kwamba mwandishi hutunga kwa kuongozwa na mambo yanayotendeka katika jamii yake wakati wa utunzi au mabadiliko yanayoikumba jamii anayoishi. Inadhihirika wazi hapa kuwa Ndi alikuwa akipata ufunuo wa utunzi wake kutoka kwa Bi Muse.

Binadamu hutafuta usaidizi kokote, kutoka kwa waganga, wanasayansi, wahubiri na hata miungu ambayo wao huamini wanaweza kuwasaidia. Ndi katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), anajikuta katika dunia ya wafu. Mle ndani anapelekwa na rafikiye Uledi. Anataka kupata tiba ya uandishi. Tiba ya kuwahusisha wanawake na kuwapa nguvu katika maandishi yake. Anakutana na mkewe Bi M, Mwanawe Yungi, Bi Mize na Jabu. Wale wanawake wanampokea na kumtunza vizuri. Bi M anasema:

Tunataka kukutibu donda uliojipa mwenyewe, aliniambia Bi M. Sasa keshafika karibu name, ananitazama kifuani pangu pale nilipogunyuka jeraha. Lo! Alimaka, Tazama donda kubwa kumbe! Nasikia ulikuwa ukiogelea nchi kavu badala ya baharini... Usiwe na hofu, utapona tu bwanamkubwa... Alikuwa akitabasamu kwa ileile namna yake ya zamani ya ujanajari.

Sasa tumwoshe mara nyingine, joshu kubwa zaidi kuliko lile la Mpigaduri, aliamrisha tena Bi M...

Tunakuosha nje na ndani kwani donda lako si la juujuu tu, limezama ndani mno, alisema hivyo mara zisizo idadi. Kisha akamwita Bi Mize. Njoo, umkafini msanii wako, umtoe uchafu wa fikra. (Uk 182).

Bi Mize anamsaidia Ndi kama msanii. Anaeleza kuwa wanataka kumtolea uchafu wa fikra. Ndi ni mwandishi wa uhalisia, ingawa anataka kuingia kwenye tapo la uandishi wa uhalisiajabu, hajui vipi. Hivi Bi Mize yupo pale kumsaidia katika safari hiyo ya uandishi.

Usaidizi hujitokeza kwa njia mbalimbali ikiwemo hata kutoka kwa mizimu. Katika riwaya ya *Nyuso za mwanamke* (2010) usaidizi unajitokeza kutoka kwa marehemu mamake Nana. Anamwandikia barua akiwelezea kuwa;

Nimekuhakikishia kwamba nilikutengenezea msingi wa kujitegemea kwa maisha yako ya baadaye, kwani mwanamke hawezi kuwa huru kama hana msingi wa kujitegemea kiuchumi (Uk 172).

Marehemu mamake Nana amemsaidia na pesa nyingi sana. Sababu ni kuwa alimengenezea msingi wa kujitegemea maishani mwake anapokuwa mtu mzima. Kupitia barua aliyoundikiwa Nana na marehemu mamake, inaeleza kuwa mamake Nana alimwachia kiasi cha pesa kwenye benki zilizoweza kumsaidia kujikimu alipokuwa akianza maisha. Marehemu mamake aliamini kuwa mwanamke huwa huru tu akiweza kujikimu kivyake. Hakutaka mwanae Nana aishi alivyoishi yeye kwa kuteseka mikononi mwa mwanamme.

4.2.8 Uwajibikaji

Kuwajibika ni kuchukua jukumu lako kufanya kazi ulilostahili kufanya. Ni vizuri kila mtu akiwajibika ili mengi yaweze kutendeka katika jamii. Uwajibikaji haswa hujitokeza panapo kazi fulani ya kufanywa iliyo tengewa mtu. Uwajibikaji huwasisitizia watu kufanya kazi kwa juhudi na maarifa yao yote ili kupata maendeleo. Mtu anapowajibika, huepuka uvivu ambao ni sumu ya maendeleo;

Ni jukumu la kila mtu kuwajibika katika lolote lile. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), Babu amewajibika. Anamtolea K hukumu. Hukumu hizo zinadhihirisha kutowajibika kwa K na kuwajibika kwa Babu. Anamweleza ya kwamba;

Shtaka la kwanza; kuwageuza watu panya wa majaribio katika maisha yao...

Shtaka la pili linadai kwamba wale matajiri walionyang'anywa mashamba yao yaliyokaa bure tu bila kuoteshwa kitu miaka yote hii, sasa wanadai mashamba na ardhi zao...

Mashtaka yanaendelea kudai kwamba nyumba za wananchi zilizovunjwa burebure mjini na vijijini lazima zilipwe fidia... Nliona kwa macho yangu buldoza lilipokuwa...

Shtaka jengine ni la watu walio wengi... wanataka kujua asili ya watoto wao kupewa elimu ya jembe miaka yote hii, huku wenu nyinyi...

Suala hilo si langu pia... alimkata kauli mzuka asiwahi kumaliza maneno yake (Uk 70).

K yupo afisini mwake. Sekretari wake anamletea faili anazopaswa kuziangalia. Mara anajihisi kuregea na hali ya usingizi unamkwea. Kisha anatambua kuwa ni mzuka anataka kumzuru. Mzuka anafika na kukaa mbele yake, anamshurutisha afungue majalada. Anamkumbusha awajibike kazini kwa kumwambia ofisi yake ni ya kutatua matatizo na si kulimbikiza matatizo. K, kwa lazima anaanza kukagua majalada kwenye treya. Mzuka anatanguliza kwa kumwambia yaliyomo kwenye majalada hayo. Mzuka anamhukumu kwa mashtaka mbalimbali. Hajapendelea jinsi K na wenzake matajiri wanawadhulumu maskini. Kupitia kwa mashtaka yake, tunaona akiwa na huruma kwa wale wanaodhulumiwa na kuteseka. Hivyo anataka K, kwa kiwango chake cha kazi, awasaidie.

Mzuka anamjia K wakati wowote mahali popote. Limekuwa jambo la kawaida kwake K ingawa ni matukio ya ajabu. Matukio haya yanadhihirisha wazi ukweli wa mhimili wa nadharia ya uhalisiajabu inayosema kuwa; kazi za fasihi za uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida. Hivi katika matini ya uhalisiajabu jambo lolote

huweza kujiri wakati wowote (Zamora, 1995). Mwandishi huyu anatukumbusha kuwa, pamoja na kuwa tunaishi maisha ya kawaida yapo upande wa pili yaliyosheheni wazimu na maajabu. Kwa kuwa matokeo ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, hushangaza, huduwaza na huogofya.

Mashtaka hutolewa kwa watu wanaoshukiwa kutenda makosa fulani. Babu anamtolea Ndi mashtaka mengi kuhusu tabia zake mbaya kwa binadamu wenzake. K amekuwa tajiri na sasa yeye na wenzake wanawanyanyasa wasiojiweza. K anakataa mashtaka mengi anayoshtakiwa kutenda.

Mzuka, kama hakimu anamsomea K mashtaka yake. Mashtaka ya K yanadhihirisha fika kwamba K na matajiri wenzake waliwanyanyasa wengine. K anaelezewa jinsi wao waliwapeleka watoto kusoma ng'ambo ilhali walala hoi mle jijini mwao watoto wao walisomeshwa tu masomo ya jembe. Hii ilikuwa na athari kwa wananchi wale kwa kuwa bila elimu nzuri hawakupata kazi nzuri za kuweza kuwasaidia kujikimu. Pia anatolewa shtaka la kuwageuza watu panya wa majaribio katika maisha yao. K na wenzake wanapanga kufungua kilabu cha FKK, ambapo kitakuwa cha watu kujiburudisha sana hasa wenye mali. Pia wanakisia kwamba, mle ndani ya FKK itakuwa ni vizuri watu wakiingia huko uchi bila nguo ndio waweze kujiburudisha vilivyo. Babu anamkashifu kuwa hawaoni kama itakuwa ni kinyume na maadili ya binadamu. Shtaka la kubomoa nyumba za watu bila kulipa fidia pia ni swala ambalo lilikuwa likiwasumbua wananchi. Wananchi wa kawaida walikosa pahala pa kuishi kwa kuwa makao yao yalibomolewa na kunyakuliwa na matajiri ambao hawakujali dhiki yao.

Mzuka anampeleka K katika safari ili aelimike. Ni mvumilivu na ni mwenye msimamo mkali. Anamuahidi K hatamtoka mpaka akamilishe kazi yake. Anambadilisha K akawa mchwa na kumpeleka alimokulia akiwa kiumbe wa kiajabu. Mwishowe anampeleka kwa mahakimu wa wakati ili ahukumiwe kwa maovu aliyoyatenda, kisha anamwambia amemaliza kazi yake, kwani anajua kuwa sasa haki itatendeka. K analishwa kiapo cha Wamasai na Kikamba na anapoachwa na Mzuka, anaona maovu aliyoyatenda na anajinyonga.

Wazazi huwajibika. Huwajibika kuhakikisha kuwa wamejikimu vizuri na watoto wao. Wazazi hutaka kuhakikisha kuwa watoto wamekula, wamevaa na wamepata masomo na hatimaye kuwa na maisha mema. Bi Mkubwa, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), amewajibika kama mama mzazi. Alipokuwa akiishi. Pesa alizotumiwa na mpenzi wake Faisal, ambaye alitaka kuishi

naye ila wazee walimkataza, alikuwa akiwekeza akiba. Mwandishi anatueleza kupitia barua yake kwa Nana kuwa;

Nimehakikisha kwamba nimekutengenezea msingi wa kujitegemea kwa maisha yako ya baadaye, kwani mwanamke hawezi kuwa huru kama hana msingi wa kujitegemea kiuchumu... Humu ndani nimeweka uthibitisho wa kisheria kwamba hii ni mirathi yako (Uk 172).

Alijua fika kwamba mwanake Nana siku moja atataka uhuru wake na uhuru wa mwanamke hauwezi kupatikana bila kuwa na hela. Anamwandikia Nana kwenye barua kuwa alimwekea pesa atakazohitaji kuanzisha maisha yake na kuuendeleza taaluma yake ya nyimbo. Nana anafurahia kwa kuwa alihitaji pesa nyingi kuuendeleza miradi yake.

4.2.9 Usemaji Ukweli

Kusema ukweli ni kitu muhimu maishani, ni vizuri kumwambia mtu ukweli bila kuficha jambo lolote. Hii huweza kumsaidia mtu kubadilisha matendo au msimamo fulani.

Mtu akiambiwa ukweli kuhusu jambo fulani, hubadilisha mtazamo wake. Wengine huchukua mtazamo hasi na wengine chanya. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), mzuka anamwambia K ukweli wa mambo bila kuficha lolote. Anasema kuwa:

Mbona mimi nimeona kama tumechukua miaka elfu moja?

Ndiyo, alijibu mzuka kwa kukenua; ndani ya nyoyo zenu mnalazimisha kuwepo kwa utengano mkubwa namna hiyo, ili muweze kujisikia. Na ni kujisikia kuliko jambo jengine lolote. Na kwa sababu hiyo ndiyo maana umehisi safari ndefu. Ukweli wa mambo ni kwamba pamoja na kutengana nao kwa makasri, mabustani, magari na starehe kemkem, mmepakana na dunia yao inayonuka. Harufu mnazisikia lakini mnaziba pua... Isitoshe, hamtaki kukumbuka nyuma yenu ilivyo chafu na inavyonuka pia. Mnang'ang'ania kuwepo na kupulizia tarabizuna, kwani mkiwa hampo uvundo wenu utasikika na kuibua hatari inayojilimbikiza kwenu (Uk 88).

Mzuka anamwelezea K jinsi wachochole wanavyoteseka kwa mikono ya matajiri. Mara hii, K anaweza kumwelewa kwa kuwa amembadilisha umbo na kumpeleka katika 'Dunia yao', dunia ya wafu. K anaona kuwa wamechukua muda mwingi kutoka katika dunia yake hadi dunia ya mzuka. Anamweleza K kuwa anavyoona tofauti ya dunia hizo mbili, ndivyo kulivyo na tofauti na utengano kati ya wao matajiri na wale masikini. Babu anamweleza kuwa wamelazimisha utengano baina

yao na wale ambao hawajiwezi. Anamueleza kwa mapana jinsi wamejenga ukuta baina yao na watu wengine. Wameishi maisha ya kifahari na kupuuza wenzao.

Mzuka anakashifu maovu yanayotekelezwa na viongozi kama K. Mzuka haoni ni kwa nini mtu mmoja awe na majumba mia moja yenye vyumba milioni na akijaliwa maisha yake ni miaka themanini tu. Mzuka anawashawishi viongozi wasiwe wabinafsi na wajali maskini wanaoishi katika makazi duni na yenye umaskini mwingi.

4.2.10 Ukarimu

Kuwa na sifa ya ukarimu ni kuwa na tabia ya kupenda sana kutoa au kusaidia kwa hali au mali. Katika ulimwengu huu ni bayana kuwa watu hawatoshani. Kuna wale wenye uwezo kuliko wenzao. Tunapaswa tuwe wenye moyo mkunjufu ili tuweze kuwasaidia wale ambao hawajiwezi. Ingawa si kila mtu aliye na uwezo wa kupata mahitaji yake yote na kwa wingi, huwa na moyo wa kupeana. Wengine huwa wenye mioyo ya uchoyo. Ni binadamu huwa na moyo wa ukarimu. Babu Mzuka ni mkarimu. Zamora & Wendy (1995) anaeleza kuwa matokeo ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida.

Mwanadamu huweza kujitolea kusaidia wenzake chakula, nguo, fedha, makazi ya kuishi na kwa njia zingine mbalimbali. Babuye K, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), ambaye ni mfu aliyefufuka anajitokeza kuonyesha hisia za utu. Utu wake unajitokeza anaponyesha upendo kwa watu maskini wanaokosa chakula ilhali K anampa mbwa wake chakula halisi wala sio hata mabaki. Anasema kuwa;

Niliitikiwa na ombwe, sauti yangu ikatuama huko mbali. Nilitaka kumwambia. La, nilitaka kumtanabahisha kinywa kipana kwamba sahani za vyakula anazoamrisha kuwekewa jibwa lake siku hizi naziondoa. Kwa sababu naona si halali. Nafanya hivyo kwa sababu nimejiaminisha kwamba mimi ni babu yake. Tena isitoshe, najaribu kumkumbusha K, kilembwekeza changu, kwamba wakati wetu mbwa walipewa chakula baada ya watu wote kushiba. Kwa hivyo vyakula K anavyoamrisha vipelekewe jibwa lake, naviondoshwa na kuwapa majirani wanaolala njaa. Nataka kumwambia K asikasirike, kwani kufanya hivyo ni wajibu wangu... (Uk 2).

Utu humsukuma mtu kumsaidia mwenzake mwenye maumivu ya kimwili, kifikra na hata ya kiakili. Kwa mujibu wa Gilbert (2010) anaeleza kuwa utu una sifa za upole, unyenyekevu, maarifa na uvumilivu hivi kwamba, mtu aliye na sifa hizi ni rahisi awe na utu kwa wenzake. Hivyo maelezo haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa, kutokana na upendo wa dhati alionao babu na livyokuwa akiona

watu wakijumuika kwa pamoja kusaidiana katika jamii, anawaonea huruma jirani wake ambao wanakosa chakula na kuwasaidia. Anachukua chakula cha doggy katika hali ya kiajabu ajabu na kutoweka nacho.

Ukarimu hujitokeza hata kwa kumpa mtu fedha za kujisaidia kukimu mahitaji yake mengine. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi anachelewa nyumbani kwake. Alikuwa akitafuta usaidizi. Anaeleza kwamba;

Leo nilichelewa kurudi. Si kwa kukimbia jikumu langu, lakini Zaidi kwa sababu ujanadume wangu wote uliishia shilingi hamsini na tano mfukoni nilizogawiwa na Shaib, majinuni mwenzangu. Nilijikuta tu napiga teke kipochi na nilipokiokota nikaona shilingi hamsini na tano. Ulikuwa usiku mkubwa nilipokiokota. Huu ukawa muujiza kwangu, na nilipokuwa nikijiuliza ilikuwaje mtu kuangusha kipochi cha pesa katika dunia hii, Shaib alinjia kichwani na kung'ang'ania kwamba pesa hizo alizidondosha yeye, baada ya kuona nimekwama! Na shilingi hamsini na tano zifanye nini siku hizi? Hazinunui hata kijiko cha bizari. Baada ya kutamba mchana kutwa na kutumia ulaghai wote nilioweza kutengeneza, nilikutana na Shaib dakika ya mwisho ya kukaribia kukata tamaa (Uk 19).

Ndi anatueleza kuwa kachelewa siku hiyo kwa sababu ya kukosa hela ya kujikimu na familia yake. Alijikuta tu na shilingi hamsini na tano alizogawiwa na Shaib ingawa hazinunui hata kijiko cha bizari. Hapa utu wa Shaib unajitokeza anapomsaidia rafikiye na hela baada ya kukosa hela.

Ni jambo zuri kuwasaidia wenzako iwapo wanakosa kitu fulani. Kwa kawaida, binadamu huishi kwa kutegemeana na wenzake. Hata kwenye bibilia tunahimizwa kuwa wakarimu kwa wenzetu. Yohana akiwahutubia watu anawaeleza kuwa aliye na nguo mbili apeane moja kwa aliyekosa, na yule anaye chakula kingi, naye asaidiane kwa wale waliokosa .

Mwenzako anapohitaji kitu fulani, ni jambo jema kumsaidia. Bi Muse katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), anamsaidia Ndi, hii inajitokeza hivi;

Mimi ni Muse, alipokwishaaniketisha aliniambia kwa sauti ya kike, sauti tamu ajabu. Unatoka wapi? Nilimwuliza. Kwa asili hasa, Ugiriki- lakini siku hizi naishi popote. Mara nyingine hujificha katika vina virefu vya ardhi kabla sijachomoza kumzuru niliyemchagua. Na leo nimekuchagua wewe. Kwa hivyo nimechomezekea chini ya mnazi palipofukiwa kitovu chako, baada ya kupiga mbizi Bahari ya Hindi kuja kuingia kichwani mwako. (Uk 61).

Bi Muse, humzuru binadamu anayemchagua yeye mwenyewe. Ni kiumbe ambaye hujifichua tu iwapo anahitajiwa kwa mapenzi ya dhati au kwa kutoa msaada. Hivi tunaona upendo wake kwa

mwanadamu. Hapendi binadamu akiteseka na ndio maana huzuru anayehitaji usaidizi wake. Ni kiumbe mwenye mapenzi ya dhati. Amekuja kumsaidia Ndi katika utunzi wake.

Ndi anataka kujua iwapo Bi Muse alimjia yeye na hivyo kumhoji. Hapa pia panatokea suala la msaada alilokuja kufanikisha. Alikuwa kumsaidia Ndi Kufanikisha kazi yake ya utunzi.

Umekuja kufanya nini? Nilitaka kusadikisha kwamba kanijia mimi.

Kama nilivyokuambia, leo nimekuja kukuonyesha njia mpya za kupita kufikia kulekule unakotaka kwenda na katika kufanya hivyo, kukuganga au kukuzidisha wazimu uliopewa na watu wako.

Nimekwama vipi? Wapi?

Kisanaa. Kwenye uhalisia mkavu. Nimekuja kukutambulisha Sanaa ni mbegu yenye korani, haimeji popote ila penye mbolea inayotaka. (Uk 71).

Kutokana na maelezo, Bi Muse alikuja kumpa Ndi msaada wa kisanaa. Msaada katika uandishi wake. Anaona kama Ndi ni mwenye uwezo mkubwa kisanaa na hivyo anataka kuendelea kumkuza kisanaa. Hivi, anamlinganisha na mbegu inayomea kwenye mbolea.

Katika harakati za pita pita pale mjini, katika miji mbalimbali, unaweza kukutana na wale ambao wanaomba msaada wa pesa na chakula kwenye miji hiyo. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), ukarimu wa Faisal unajitokeza anapomsaidia Kibobi. Kibobi anapatikana kando ya barabara akiomba msaada kwa watu wanaopita. Mwandishi anaeleza kuwa;

Kibobi. Alimkamata bega.

Wewe ndiye yule malaika tuliyeambiwa tutateremshiwa?

Malaika? Nimeteremshwa? Lini nimeteremshwa? Mimi malaika? Alijiuliza mtafiti wetu. Kama wewe malaika wa heri tuliyeleremshiwa, hebu niruzuku shilingi elfu moja. Alisema hivyo baada ya kitambo cha kumtolea Faisal macho.

Kufumba na kufumbua Faisal alitoa noti ya shilingi elfu tano akampa Kibobi (Uk 10).

Kibobi, bwana mmoja mchafu, mkofu, mbovu na aliyevaa raru la kanzu, anakutana na Faisal. Faisal na Kibobi ni majirani, walikwenda chuoni pamoja na kucheza pamoja. Hata hivyo, Kibobi amekuwa wehu na hawezi kumtambua Faisal hata Faisal akijaribu kumkumbusha. Hivyo, anapomwona Faisal, anamwona kama malaika aliyetumwa kwake kumrehemu.

Faisal anaonyesha ukarimu wake anapomsaidia Kibobi na shilingi elfu tano. Kibobi yuko pale hajiwezi, hawezi kujikimu kimaisha na hivyo kuishia kuwa omba omba. Kwa sababu hii amemwona Faisal kama malaika. Tukio hili linathibitisha ukweli wa yale asemayo (Samkange

1980) kuwa falsafa ya Ubuntu inaeleza kuwa, mtu huweza tu kuongeza mibaraka yake kwa kusaidia wenzake katika jamii na hivyo hata kuinua hadhi miongoni mwa jamaa, Samkange anaendelea kusema kuwa, matendo ya Ubuntu hujitokeza kama vile kuenda kuwaona wagonjwa ambao hata si jamaa yako, kutuma rambirambi kwa waliofiwa, kupeana chakula kwa wasioweza kupata, kuwasaidia wazee na hata kusalimia watu kwa njia ya upole.

4.2.11 Motisha

Mtu hupewa motisha unapompa hamu ya kufanya jambo fulani. Binadamu huhitaji motisha. Hii ni kwa sababu huwa na hulka ya kuchoka kufanya jambo na kukata tamaa. Kupeana motisha kwa mwenzako ni jambo muhimu sana. Wakati mwingine mtu hutaka kukata tamaa kwa jambo nzuri linaloweza kusaidia sana. Kwa mfano kumpa motisha mwanafunzi aweze kusoma kwa bidii kwa manufaa yake ya baadae. Motisha humhimiza mtu afanye kazi au shughuli zozote kwa bidii katika jamii. Wazazi na walezi hutumia lugha ya kumtia mtoto motisha wanapogundua kuwa alikuwa na udhaifu fulani wa kutekeleza kazi alizoagizwa kufanya. Aidha, humhimiza mtoto kubadilisha tabia yake. Vilevile, mtu aliyepitia changamoto mbalimbali za maisha kama vile magonjwa na mateso katika jamii uhimizwa. Utafiti huu ulibainisha kuwa kumpa mtu motisha humwezesha kufanya kazi kwa bidii, kuwa na tabia nzuri na mgonjwa kupokea nafuu.

Wakati mwingine, mtu huhitaji motisha kutoka kwa wenzake ili kuweza kufaulu kufanya jambo fulani. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Shaib ana mpa motisha Ndi kwa kujadiliana naye kimawazo kuhusu uandishi wake wa riwaya. Shaib anamuuliza;

Umemaliza kusoma The Aristos kwa mara nyingine? Shaib huyo
Ndiyo
Mara ngapi?
Hata sijui... labda milioni moja.
Kinaya!
Sijui mara ngapi nimekisoma.
Unafikiri kitakusaidia katika riwaya yako ya Dunia Yao?
Intertextuality... mchanganyondimi unakusudia? Nilicheka. Naye akacheka. Tukacheka pamoja (Uk 42).

Shaib pia anaonekana akimjali kwa kutaka kujua amefikisha wapi usomaji wake wa riwaya zingine ambazo atatumia kujenga riwaya yake. Kwa kumpa motisha, anamjali na anadhihirisha utu.

Marafiki wa kufaana hujipa motisha wakati wowote wakiwa na masuala fulani ya kushughulikia. Hili humwezesha mtu kujikaza kutimiza malengo fulani aliyokuwa nayo.

Bi Muse anamhamasisha Ndi. Anamwonya kutokana na haraka ya utunzi. Anamweleza kuwa kazi ya utunzi huhitaji utaratibu na wala si pupa. Amemtembeza Ndi katika bustani ya mazingaombwe. Amefanya hivi ili kukuza ubunifu wake wa kuandika vitabu vya kisasa vyenye mfumo wa kimazingaombwe. Katika bustani lile anamfunza, anamfunza ya sasa na ya kale. Anajua kulinganisha vizuri anajua kuendeleza na kusimulia kimantiki. Ndi anampa sifa za ‘Malkia wa Sanaa’.

Ni bustani ya mazingaombwe, Bi Muse alinieleza bila ya kumwuliza. “Inaweza kuchangia Sanaa yenye kuvutia ajabu. Itazame sana. Inaweza kukuchukua na kutajirisha sana usanii wako katika ukweli na uchawi na uchakaramu wake. Ila nataka kukuonya. Ukitaka kufaidika nayo usikubali kuuona upande wake mmoja tu. Uchanganue utata wake kifikra, changanua dialectics zake zinazotangamana na kufarakana. Ziangaze mbinu zake za kisuriamana na mkengeuko... Fumbua macho yako katika leo si katika jana. Katika hiki kipindi cha mpito. Katika vuguvugu la mabadiliko. Katika jiwanga la ukale na usasa unaopamba moto... (Uk 67).

Katika uandishi na usomi panatakikana utaratibu. Mambo haya hayana pupa. Hata Bi Muse anamwelekeza Ndi kuhusu haya. Anampanua mawazo kwa kumwambia kuwa kama mwandishi anapaswa kuwa na mtazamo wa pande zote, asiwe tu na mtazamo hasi kwa kitu fulani.

Kuna watu ambao huwa na woga wa kuwasilisha tungo fulani mbele ya hadhira. Watu hawa huwa wanahitaji kuhimizwa kutokuwa na woga. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana ana woga kuimba mbele ya hadhira. Marehemu mamake naye anampa motisha. Nana anaeleza kuwa;

Katika upeo huu nilishutukia wasifu wa mamangu umekuja kunisimamia mbele ya macho yangu. Kisha kivuli chake hai kikaketi juu ya kiti cha enzi. Kavaa gauni jeupe pana la arusi. Na taji la maua kichwani. Muda si muda, akaanza kunipigia makofi, na mara watu wakayapokea makofi kwa mizani ya kichawi. Uwanja mzima ukanguruma makofi kabla hata sijaanza kuimba. Hatimaye nikafumbua mdomo. Nikaanza kuimba wimbo nilioutunga mimi mwenyewe huku nikiikogesha furaha yangu machozi (Uk 54).

Nana ana woga kuimba mbele ya hadhira. Hajawai fanya lolote mbele ya umati kama ule. Ni siku yake ya sherehe. Babake amewaalika watu wengi nyumbani kwao. Nana amesuburiwa kutoa hotuba. Mpango wake ni tofauti kwa kuwa yeye anataka kuimba. Mpiga gita amekwishamwambia kuwa yu tayari kuanza kazi ya kupiga gita. Nana anapiga gilasi na umati unageuka kwa kimya

ukimwungalia. Mpiga gita anampa motisha. Anamweleza asihofu wala asiogope kwa kuwa ameshampika akapikika katika uga wa muziki. Anapojitayarisha kuimba, kivuli cha marehemu mamake kinajitokeza na kuanza kumpigia makofi. Umati unaingilia kupiga makofi pia. Nana anaanza kuimbia umati. Anaimba kwa furaha.

Marehemu mamake anakuja kumpa motisha wakati ambapo ana woga wa kuimba. Kule kumwona kunamfanya kuanza kuimba na watu wanachangamka.

Kiumbe huyu anajitokeza kwake kumkumbusha Nana kuwa alitoka kuja kumtafuta mamake na kumkomboa mwanamke wa kitaarab, ilhali yeye yumo pale chumbani amekaa tu. Kiumbe kile kimekuja kumpa motisha ya kutimiza alichokuja kutafuta. Anamhoji na kumshurutisha awache kuwa mwoga na aondoke afuate kilichomleta pale.

We Nana! Ile ndoto yangu iliyopigisha rangi iliniita. Kwa sababu sikuitika, ilitoka kichwani kuja kuning'inia juu ya dari chumbani mwangu. Ilipoona nimeipuuza, ilichukua umbo la kiumbe cha ajabu ambacho sijapata kukiona. Kiumbe aliyechanganya rangi za ukole... 'We Nana!' Kiliita tena hicho kiumbe cha ajabu. Si umeapa kwamba utajiacha usukumwe mbele na wakati? Mbona sasa unasitasita? Mbona unajivunja moyo? Sasa mbona unarudi nyuma?

Si umeshachukua hatua? Hapo ulipo si umeshakuwa mwimbaji wa kujisomesha badala ya kuimba kwa kokotezo za kimaumbile tu? ... Watunga-muziki, watunga-mashairi, wapiga-ala, waitikaji, wayumbaji, wachezaji wote umewachungua... Sasa unataka nini tena? Unangojea nini? (Uk 135).

Kiumbe huyu anamwuuliza maswali Nana ya kumkumbusha ahadi zake alizojitolea kwake. Ila sasa ni kama amekata tamaa kuyatimiza. Nana anamwelezea kuwa maneno yale yalikuwa rahisi kusema na yamekuwa magumu kuyatimiza kwa kuwa amekosa fedha na kila kitu kinahitaji fedha. Kiumbe huyu anamhimiza kuwa fedha si kila kitu kwa kuwa yeye tayari ni msomi na amejifunza kuimba kimaumbile tu. Nana anafikiri kuwa ili kupata kazi lazima ahitaji fedha.

Vile vile, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Marehemu mamake Nana bado huja kumzuru kumpa motisha. Anamwambia;

Nina fahari kwako Nana. Mama alimwambia binti yake alipomaliza kumnyonyesha. Umemudu kufanya yale ambayo mimi siku zote nilitaka kufanya katika uhai wangu nikashindwa. ... Lazima lakini uende mbele ya hapo ulipofika. Aliendelea mama mtu. Lazima upige hatua Zaidi kwa hali yoyote utakayochagua, mjane au umeolewa. Haki yako ya uana jike itumie kwa busara, lakini dhuluma juu ya uke wako usiikubali. Wewe umerithi

kilakitu chake ila umekosa tu bahati yangu. Na hilo ni jambo la heri kwako, maana bahati yangu mimi ilikuwa mbaya tangu mwanzo hadi mwisho. (Uk 285).

Nana alipokuwa kachoka na maisha na anahisi anapaswa kuingia kwa dunia ya kiza, yaani dunia ya wafu, mamake alimzuru na kumtia moyo kuhusu maisha. Wakati huu amechoka na kuishi kitandani sana hadi wenzake pale nyumbani wakawa na hofu kuwa angekufa hivi karibuni.

Katika sehemu hii suala la jinsi viumbe wa kiuhalisiajabu wanavyodhihirisha utu umeshughulikiwa. Viumbe hawa wameonekana wakionyesha sifa mbalimbali za utu kwa binadamu. Sifa hizi za utu zilivyojitokeza ni kama; upendo, heshima, usaidizi, uwajibikaji, msamaha na mengineyo. Sifa hizi haswa zilijitokeza viumbe hawa walipokuwa wakitangamana na binadamu. Viumbe hawa wa kiuhalisiajabu walijitolea kuwasaidia binadamu kwa njia mbali mbali. Sehemu hii basi imedhihirisha kuwa hata viumbe wa kiuhalisiajabu wana utu, sifa ambayo imekuwa ikihusishwa na binadamu.

4.3 Athari ya Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu

Kazi ya fasihi ya Uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida. Matokeo haya huweza kushangaza, kuduwaza na kuogofya. Katika sehemu iliyotangulia, viumbe wa kiuhalisiajabu wamedhihirishwa wakionyesha utu. Utu wa viumbe hao huwa na athari kwa binadamu. Aidha, binadamu akiwa amepokea tendo fulani huathirika kwa njia tofauti. Athari huweza kuwa chanya ama hasi. Hali hii hujitokeza kulingana na tendo alilopokea mtu au kitu. Tendo la utu linapojitokeza binadamu huwa na uwiano na watu wakaelewana, pia huleta furaha, mtu hupata nguvu, na hata kutoa shukrani. Sehemu hii basi imeshughulikia athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed na zimejadiliwa ifuatavyo;

4.3.1 Ushirikiano

Ushirikiano hudhihirika baina ya watu wanaoelewana kuhusu jambo fulani. Watu wanaoelewana, hupatana. Penye ugomvi hapana ushirikiano wowote. Ushirikiano ni sifa mojawapo muhimu katika maisha ya binadamu. Ni vizuri kuwa na ushirikiano kati yako na watu walio kwenye mazingira yako ndiposa unaweza kusaidiwa kwa mambo kadhaa. Bila ushirikiano na wenzako,

huwezi kupata msaada wowote unapohitajika. Hii ni kwa sababu kila ukitaka usaidizi watu watakuwa wakikukimbia kutokana na tabia zako mbaya zinazokutenganisha na watu.

Utu ni kuonyesha upendo na huruma haswa kwa kiumbe. Utu ni muhimu katika maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu ni jambo linalo endeleza upendo na utangamano baina ya watu. Bila utu, panaweza kuwepo na vita, watu kuteswa, uongozi mbaya miongoni mwa mengine. Kwa mujibu wa (Gilbert, 2010) binadamu wana mahusiano kupitia kuishi kwao, kifo chao na hisia zao. Anaendelea kusema kuwa utu hupatikana tu kwa binadamu kwa sababu za tofauti za hisia zao na zile za wanyama. Watunzi mbalimbali wa kazi za kifasihi wameendeleza maudhui haya ya utu hususan: Walibora (2002), Kithaka wa Mbeeria (2002) na wengineo. Gilbert anataja kuwa athari ya utu huwa utangamano. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi anaeleza kuwa alichelewa sana kufika nyumbani baada ya kupata hela alizopewa na Shaib. Pia kukaa kwake na Shaib wakizungumza kunamsaidia kupanua mawazo yake.

Leo nilichelewa kurudi, Zaidi kwa sababu baada ya kupata zile fedha, niliketi barazani mimi na Shaib tukawa tunasimuliana hadithi ya ukata, ukapa na upweke uliomzunguka Clegg na Miranda katika riwaya ya Fowles, *The Collector*. Ilinifungua mawazo mapya kuhusu ulimwengu wetu ulivyogawika (Uk 20).

Ndi na Shaib ni marafiki ambao wanapendana, wanasikilizana, na wanasaidiana. Wanapatana kwa vyovyote vile na kila mmoja anamwelewa mwenzake licha ya Shaib kumsaidia katika kupanua mawazo ya uandishi. Pia tunamwona hata akimsaidia na hela ya kujikimu. Utu humsukuma mtu kumsaidia mwenzake mwenye maumivu ya kimwili, kifikra na hata ya kiakili. Athari ya usaidizi unaotolewa na Shaib kwa Ndi ni ushirikiano ambao unabainika wakati wanapopata nafasi ya kusimuliana hadithi. Kwa mujibu wa Gilbert (2010) utu una sifa za upole, unyenyekevu, maarifa na uvumilivu hivi kwamba, mtu aliye na sifa hizi ni rahisi awe na utu kwa wenzake. Sahib anaonekana na sifa hizi na anamsaidia Ndi kwa njia kadhaa.

K, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), anapopelekwa kwa dunia ya mzuka, iliyo tofauti na dunia yake, anaanza kuelewa anachoambiwa na mzuka. Hii ni baada ya mzuka kumfafanulia jinsi wanavyoepukana na binadamu wenzao kwa kuwa wao ni tajiri na wengine ni maskini. Mzuka anamweleza utengano uliopo baina ya matajiri na maskini. Anamweleza kuwa hiyo ni hatari wanayojilimbikizia. Anajaribu kumweleza kuwa si vizuri kutengana na binadamu mwenzako kwa sababu ya mali.

Nani basi atakuja kumwambia kwamba zamani hakukuwa na kudhulumiana? Kwa upande mwingine lakini ilimjia wazi picha ya usamehevu iliyokuweco wakati ule ambayo leo katika wakati wao anajua wazi haipo. Na kwa msingi huu, babu yake mzuka alikuwa akisema kweli (Uk 101).

K alipuuza sana kauli hiyo. Ghafla lakini, kama kupwesa, jambo la ajabu lilimzuka. Macho yake haraka yalikuja kuripuka mripuko mkali; kama ule unaometa katika kiini cha juakali. Ndani ya kichwa chake mkafwatia mripuko wa radi iliyofuatia huo mweso. Alipeleka vidole vyake machoni akayafikicha, na alipoviondoa vidole, alianza kuhisi anafahamu yote aliyokuwa akiambiwa na mzuka sasa. Kwa mara nyingine tena K anapata kufahamu ya kuwa asemayo mzuka ni kweli. Si kwamba hakuyafahamu tokea mwanzo, lakini sasa alihisi hana hiyari kukiri ukweli wa mambo. Yaani hakuwa na kizuwizi ndani ya nafsi yake. Kama vile kulikuja fagio lililosafisha ukaidi wake ndani kwa ndani. Kule kuona kwamba kila alichokuwa akisema na kukifanya mzuka sasa kilikuwa sahihi. Pamoja na hayo hakutaka kujionyesha kwamba anamfahamu. K anakubali kushirikiana na mzuka, vile vile anakubaliana na wazo la Mzuka kuwa matajiri wanadhulumu wasiojiweza.

Kwenye jamii ni vyema kuwa na utu wema na uhusiano mzuri. Tabia ya kuishi katika jamii na kushirikiana katika mambo, mepesi na magumu, ni wajibu wa kila mwanajamii. Kupitia uwiano wanajamii wanadhihirisha ukweli kuwa wanajamii wanahitajiana. Hata kama mtu ni tajiri anayeabudu uwezo wake mkubwa wa hali na mali, bado kuna wakati, atakuwa na mahitaji kutoka kwa wale wenye uwezo mdogo. Kichanga na maiti tu, ndio hufanyiwa kila kitu, mtu pekee hajitoshi, maisha ni kutegemeana na kufanyiana. Iko siku, mama tajiri, ataomba chumvi kwa jirani.

4.3.2 Furaha

Kufurahia ni hali ya uchangamfu, kuridhika au kustarehe. Mtu haswa hufurahia tu jambo zuri linapotokea. Mtu huweza kufurahia kwa sababu ya mambo mengi. Unapofaulu mtihani, wewe hufurahia, unapopona kutokana na magonjwa fulani pia hufurahia. Sababu za kufurahia huwa nyingi maishani mwa binadamu.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi amefurahia sana usaidizi wa Bi Muse, baada ya kumtembeza katika bustani ya kimazingaombwe na kumwelimisha kuhusu masuala ibuka yanayohusiana na utunzi upya wa kisanaa wa kimazingaombwe. Ndi anaeleza kuwa;

Naam, nilikiri. Hii ndiyo itakuwa simulizi yangu mpya katika mchanganyondimi. Kipande hapa...kipande pale. Vipande vya 'allegory'. Vipandevipande vya ngano mpya. Ngano ya

tafrani- za kileo katika usogori mpya. Aaaaa, ikiwa zamani sikukujua Bi Muse, sasa nakuhitaji mara milioni moja. Nataka niwe nawe pachapacha. Nikukumbatie unikumbatie, unikoleze ilhamu, nilimwambia. Nikamsikia akicheka (Uk 68).

Kutokana na dondoo, Ndi ana furaha tele. Furaha hii imetokana na usaidizi alioupata kutoka kwa Bi Muse. Ameona umuhimu wa Bi Muse kwake. Anasema kuwa sasa anamhitaji mara nyingi, awe karibu naye ndiposa aweze kuendelea kumsaidia katika uandishi wake. Katika wanda la uandishi na elimu kwa jumla, mtu huhitaji usaidizi wa wenzake ili kukwea kufikia kiwango alichofikia. Watu wenye tajriba aghalabu huwasaidia wale wanaochipuka katika mawanda mbalimbali.

Vile vile, Nana anafurahia kuvunja ungo. Hii ni katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010). Alikuwa msichana wa miaka ishirini na moja ilhali hakuwa amevunja ungo. Hakuwa ameingia miezini. Anafurahia kwa kusema;

Nimeingia miezini... Nimeingia miezini! Baada ya miaka ishirini na moja nimezaliwa upya! ... Nimezaliwa upya! ... Nimezaliwa upya... Sasa nimeshakuwa mwanamke kamili... Nimeshakuwa mtu mzima! (Uk 29).

Nana alikuwa anajihisi mpweke. Alikuwa hana furaha kwa kuwa hakuwa amevunja ungo kama wasichana wenzake pale shuleni. Alikuwa chumbani pake na akimfikiria mamake akilini mwake. Hakutaka kumsikia mamake wa kambo na babake. Akiwa chumbani anahisi tu kuongozwa kwa lile apaswalo kufanya. Anafanya kila kitu anavyoelekezwa. Anapomaliza na marehemu mamake anavunja ungo na anaingia mwezini. Anfurahia na kuanza kusherehekea. Kuingia kwake mwezini kulitokana na usaidizi wa marehemu mamake. Suala ambalo linamfanya afurahie kupindukia.

Nana anapata motisha wa kuimba kutoka kwa kivuli cha marehemu mamake. Anapoanza kuimba anaimba kwa furaha hadi akatoa machozi ya furaha. Anasimulia kuwa;

Katika upeo huu nilishutukia wasifu wa mamangu umekuja kunisimamia mbele ya macho yangu. Kisha kivuli chake hai kikaketi juu ya kiti cha enzi. Kavaa gauni jeupe pana la arusi. Na taji la maua kichwani. Muda si muda, akaanza kunipigia makofi, na mara watu wakayapokea makofi kwa mizani ya kichawi. Uwanja mzima ukanguruma makofi kabla hata sijaanza kuimba. Hatimaye nikafumbua mdomo. Nikaanza kuimba wimbo nilioutunga mimi mwenyewe huku nikiikogesha furaha yangu machozi (Uk 54).

Marehemu mamake Nana anawasisimua wasikilizaji kwenye uwanja kuanza kupiga makofi kabla hata Nana aanze kuimba. Nana alikuwa mwoga na kutokana na tendo hili anapata nguvu ya kuanza

kuimba. Anafurahia kupita kiasi. Furaha yake inatokana na usaidizi wa mamake kuwasisimua wasikilizaji.

Sauti ya mamake Nana inapomkumbusha kuhusu lile begi aliloachiwa, Nana tena anakitafuta alipokiweka na kukifungua ndani. Anapata bahasha ya pili. Bahasha ya kwanza alikwisha soma barua yake alipokuwa kwao. Siku ambayo kupitia usaidizi wa marehemu mamake, kupitia maelezo ya barua, aliweza kuvunja ungo baada ya miaka ishirini na moja. Leo hii anafungua bahasha ya pili na kupata pesa kadhaa na kitabu cha benki.

Nimeamka tajiri,” alijibu Nana huku akicheka kicheko kipana na kinene kilichoibuka nyuma ya machozi. Alicheka mpaka kuta zikacheka naye. Faisal naye akaambukizwa kicheko. Wakacheka wote wawili huku wamekamatana mabega na kutazamana migongo. Hapo tena Nana akamwonyesha Faisal ile hundi ya shilingi milioni tisini na kibarua kidogo kilichokuwa kimefungamanishwa na hundi hiyo na kitabu cha benki kwenye bahasha maalum (Uk 171).

Nana ana furaha kupita kiasi. Anafurahia kwa kuwa alikuwa na shida ya pesa ambayo alitaka kuanzishia bendi yake ya taarab. Alishatembea kutafuta kazi ili aweze kupata pesa, alikopata, hakupata pesa ya kutosha. Anapopata hizi pesa, anaona uwezo wa kutimiza ndoto zake zote. Usaidizi huu anaopata kutoka kwa marehemu mamake unamfurahisha kupita kiasi.

4.3.3 Shukurani

Binadamu hushukuru anaporidhika baada ya kutendewa tendo fulani. Mara nyingi hushukuru tu anaporidhika na tendo jema analotendewa. Shukurani ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Ni ishara nzuri kwa anayekutendea jambo. Humfanya mtu kuwa na ari ya kukusaidia tena kwa wakati mwingine. Watu hushukuru kwa njia mbalimbali. Huweza kushukuru kwa neno tu “Asante/Shukurani”. Wakati mwingine huweza kushukuru kwa kukupa kitu Fulani au kwa kukutendea jambo fulani kuonyesha ishara ya shukurani.

Nana hushukuru katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), baada ya ishara anazopewa na marehemu mamake kumsaidia. Nana anasema hivi;

Baadhi ya siku unapotaka kunikumbusha kitu, wewe huangusha kifaa chochote kwa kishindo: kikombe, kisahani, bilauri, bakuli, kitabu, kichupa, kioo, hata saa ya mezani. Nami hutambua ni wewe unayenikumbusha. Mara nyingine wewe huja ghafla kuniguta kwa jambo la hatari ninalolikabili- nami hukushukuru (Uk 18).

Mara nyingi, marehemu mamake hujitokeza kwake Nana kumkumbusha kuwa anapaswa kufanya kitu fulani na hata humguta kwa jambo la hatari linalomkabili. Baada ya usaidizi wote hu, Nana hushukuru.

Kutoa shukrani ni jambo muhimu sana maishani mwetu. Ikiwa utapata usaidizi wowote kutoka popote, ni vyema umshukuru aliyekusaidia. Hivi atakuwa na azma ya kukusaidia wakati mwingine tena ukihitaji msaada.

4.3.4 Nguvu

Nguvu ni kuwa na uwezo wa kufanya jambo au msukumo mkali unaotokana na nishati (TUKI, 2010). Binadamu wakati mwingine hufa moyo kutokana na mambo fulani. Jambo zuri nalo ni kuwa, wakati mwingine hupata nguvu au msukumo wa maisha kutokana na hali fulani. Kwa mfano katika maisha ya binadamu, ambaye huwa mzazi, huweza kukata tamaa kuishi kwa sababu ya mizozo itokanayo na ndoa, ila tu anapoona watoto wake hujitia nguvu ya kuendelea na ndoa ile na hata kuendelea kutafuta hela ili aweze kujikimu na watoto wake.

Mbiti (1980) anaeleza kuwa; Waafrika wanaamini kuna nguvu za ajabu ambazo hutoka kwa kiumbe wa ajabu mwenye nguvu na uwezo zaidi. Kiumbe huyu tena husambaza nguvu zake kwa viumbe wengine au kwa vifaa.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana baada ya mamake kumzuru alipokuwa mchovu wa maisha na jamaa zake wakadhani kaelekea kufa, alipata nguvu tena baada ya masimulizi ya mamake kwake. Mamake alimzuru kumwonya kuhusu ndoa na akamzuru tena kumshukuru kwa jitihada zake kama mwanamke. Mwandishi anaeleza kuwa;

Simulizi ya Bi Mkubwa ilipofika hapo, Nana alijiona anapasua ule ungozi uliokuwa ukimzuia kuingia chumbani mwake. Alipotazama vizuri aliona yuko juu ya kitanda chake, amezungukwa na kila mtu aliyeshahiki kumzunguka: Amour, Faisal, Bi Chuma, bibiake, Bi Mau mama wa bibiake Bi Chuma na wenzi wengine waliokuwa wakiishi humo. Wote walikuwa wamechanua furaha kwa vile amemudu kuja juu kutoka chini kwenye sakafu ya dunia (Uk 292).

Nana amejigaragara sakafuni na kila mtu akawa na hofu pale nyumbani. Baada ya marehemu mamake kumzuru, ananyanyuka kutoka pale chini kwenye sakafu. Kila mtu pale nyumbani anafurahia. Nana amepata nguvu tena.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Kuwepo kwa Bi Muse karibu na Ndi unampa jazba ya uandishi. Ndi anajisemesha, anasema:

... Je, huu mkabala wangu na Bi Muse ni muhimu? Nani Bi Muse? Kiumbe gani huyu hasa? Ndiyo, jina lake nimekuwa nikilisikia na kulisoma siku nyingi. Kama alivyosema mwenyewe, si kiumbe wa sasambura turore. Hujifichua anapohitajiwa kwa mapenzi ya dhati au kwa kutoa msaada. Na mimi, nimefika baleghe ya kusalitika naye. Nina haja naye. Ninamhitaji. Ninataka anisaidie. Anisaidie kuwasaidia wengine ikiwezekana. Anisaidie kuukata ugumba wa utunzi. Nina hamu kurutubisha na kutia mbolea pahala fulani. Nipate kizazi kipya cha sanaa katika ukame wa ubunifu. Nipate kurutubisha kizazi kipya cha utu katika ukame usio na utu. Ninahitaji mtekenyo wake unipe jazba (Uk 62).

Ndi anahitaji jazba katika utunzi wake. Ndi anataka kujua kutunga kazi zake kwa mfumo mpya na kwa ubunifu wa hali ya juu, na ni Bi Muse tu ndiye anayeweza kumsaidia. Ndi anahitaji mtekenyo wa Bi Muse umpe jazba ya uandishi. Anataka Bi Muse awepo ampe moyo wa uandishi wa kizazi kipya. Bi Muse alikuja kwake kumsaidia katika sanaa yake ya uandishi. Kupitia kwake Bi Muse anaweza kutenda mengi katika sanaa ya uandishi. Ndi basi amepata nguvu mpya katika uandishi wake.

4.3.5. Hamaki

Hamaki ni kuwa na hasira au kughadhabika kwa sababu ya tendo fulani. Mtu huweza kughadhabika iwapo ameuhiwa na tendo fulani. Matendo ya kuudhi tu ndio huleta hamaki miongoni mwa watu. Mtu aliye na hamaki huonyesha hisia hii kwa njia mbalimbali. Wengine watanuna tu bila kuzungumza, wengine watapiga kelele na hata wengine kutumia nguvu kuonyesha hasira yao, kwa mfano kuchapa mtu kofi.

Utu wa babu kwa waliokosa chakula kunamsababisha K kuwa na hamaki katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001). Hii inadhihirika baada ya haya kutendeka;

K aliposikia jibwa lake Doggy likinung'unika njaa, alipandwa na hamaki. Mara hii nani tena? Nani anamcheza shere? Mwezi mzima kwa hakika kazi ni hiyo hiyo. Weka sahani za vyakula, sahani toweka...weka sahani, sahani ondoka...Nani angeshukiwa kama watumishi? Kwa hivyo, fukuza mtumishi mmoja, ingiza mwingine- mlolongo mrefu us'o kikomo! Watumishi nd'o wanaozing'wapura sahani za vyakula. Vipi? Hata haijulikani. Sahani hutoweka tu kimazingaombwe. Mbele ya mtu. Eti ndivyo watumishi walivyoungama... (Uk 3).

Kutokana na utu wa babu kwa waliokosa chakula, anachukua chakula cha jibwa wa K na kuwapa wale. Anajaribu kumkumbusha K, kilembwekeza chake kuwa, wakati wao, mbwa walipewa

chakula baada ya watu kushiba. Hivyo kila mara sahani ya jibwa likiwekewa jibwa chakula ale, babu huichukua. Jibwa la K hubakia kupiga kelele kwa njaa. Jambo hili humfanya K kukasirika kwa kiasi cha kuzozana na wafanyikazi wake n ahata kuwafuta wengine kazi. Kila wakati Babu alipomtokea K, alijitokeza kwa mazuri li kumsaidia K ingawa K alikuwa na hamaki nyingi. Utu wa babu wa kuwapa chakula wale ambao hawajiwezi, ulimfanya K kukasirika kila wakati.

Vile vile katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2010), babu hataki hali ya K ya kiafya izarote kwa kutumia vyakula vyenye utamaduni wa kigeni. Hii inadhihirisha utu wake kwa K. K anaposhauriwa kuachana na vyakula vyenye utamaduni wa kigeni vilivyo na athari kwa afya na vinavyotozwa pesa nyingi, anakasirika.

K alikasirika. “Unajua nini wewe!” alibwata kwa kejeli huku akitazama juu kwa hasira (Uk 39).

Kuna baadhi ya vyakula ambavyo vinadhuru afya ya watu. Miongoni mwao ni sukari, maziwa, sehemu nyingi za mkate kama vile gluteni na vinywaji vyenye pombe pia huwa na shida. Shida hizi hujitokeza kwa sehemu nyingi za mwili kama vile ngozi, uso, na sehemu nyinginezo za mwili. Ni muhimu kufikiria kuhusu vyakula tunavyokula ili kukimu afya njema.

4.3.6. Mshangao

Mtu anaposhangaa huonyesha hisia kutokana na kitu fulani. Kushangaa ni hali ya kustaajabu na kutojua la kufanya kutokana na jambo lililotokea. Watu hushangaa kwa njia tofauti, huweza kumaka kwa sauti au hata kutumia tu ishara za uso. Pia hushangazwa kutokana na matendo fulani yanayomtendelea. Matendo ya utu wanayopata wahusika mbalimbali yanawaacha kinywa wazi.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi anashangazwa sana na Bori. Anashangazwa na uwezo wa Bori kuzungumza namna ile.

Niliemezwa kwamba Bori aliweza kusema namna hii. Ilikuwa kama miaka yote hii akienda macho wazi kuduhushi kila alama ya falsafa ya elimu na kuifundika kwenye bindo la unyamavu wake. Na sasa bindo hilo limejaa na kufufurika (Uk 114).

Anashangaa kwa kuwa Bori alichukuliwa tu kama mtoto ambaye alipenda kufanya vitu vya mkono kuliko kuongea. Kila wakati alipatikana akiwa ameketi akitengeneza vifaa kwa vyombo vya kuokotwa. Alisikika akiongea kwa nadra.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana anahadithiwa maisha ya mamake anashangaa. Utu wa mamake mzazi unadhihirika wazi anapojitokeza kumkanya kutokana na kuolewa. Linalomshangaza ni uhusiano wake na babake. Anamwelezea ya kuwa

Licha kuolewa na Bwana Hila kwa nguvu za utajiri na mali yake, bwana huyo alidhani tu maisha ya mwanamke ni kustareheshwa. Kwa hali hii aliudhika. Alinigeuza mtawa nyumbani kwa kufanyiwa kila kitu na watumishi. Nilichukua vigae na kusaga na kumtilia kwenye chakula. Babako basi akanifukuza. (Uk 289)

Aliendelea kuishi maisha ya mateso hadi akawa na kiwewe. Alichukuliwa na kupelekwa kwenye hospitali ya wendawazimu kwa miaka. Hatari yake ilipopungua, alitolewa kwenda kuishi maisha ya kawaida. Nana anashangazwa kuwa babake ndiye aliyekuwa sababu ya mamake kuwa mwendawazimu. Anashangaa kwa kugundua kuwa kumbe Faisal ndiye aliyempenda mamake kwa dhati.

Kushangazwa kwa Nana kumetokana na maelezo ya mamake kuhusu ndoa. Marehemu mamake nana anampenda mwanake na hivyo kumtahadharisha kuhusu maisha mbaya ya ndoa. Hamtakii mabaya kama alivyopitia. Suala hili la kumtahadharisha linaonyesha utu alio nao.

4.3.7 Ufarakano

Ufarakano ni kutopatana kimawazo baina ya watu wawili, vikundi viwili au zaidi. Binadamu huwa na mawazo tofauti tofauti kuhusu dhana mbalimbali. Wakati mwingine, hukubaliana kuhusu mawazo haya na wakati mwingine huwa hawakubaliani na mawazo haya. Iwapo hakuna kukubaliana kuhusu jambo fulani, basi huleta kutoelewana kati ya watu.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Kutokana na matendo ya utu yanayodhihirika kwa Nana, kupitia ishara za marehemu mamake, anakataa kuamini wasemavyo watu kuwa mamake kesha aga dunia. Hawaelewani kuhusu suala hili la mamake kuwa hai ama mfu.

Mara nyingi hukumbuka pale unapofurutu ada. Pale unapokuja kuninyukua au kunizaba kibao ili kunizindua na hatari inayonikabili. Nami hujua ni wewe kwani hapana mwingine ambaye angethubutu kunikamata mkono kunivusha barabara ya hatari. Na ingawa hulalama na kulaani huku nasugua mchonoto pajani au shavuni, hujikuta hatimaye nimeonyeka. Nimenusurika. Nimeepuka hatari. Kwa nini basi niwasikilize wao? Kwa nini niamini kuwa wewe haupo? Kwa nini nikubali umeshatoweka? Kwa nini nifanye hivyo wakati najua upo na mi' karibu au mbali? (Uk 19).

Nana anakataa kuamini kuwa mamake hayupo. Hii ni kwa sababu kila wakati anahisi kuwa yupo karibu naye kutokana na zile ishara. Nana anashuku kuwa mamake yu hai na wala sio mfu. Hii ni kwa sababu kila anapohitaji msaada hupata na ni marehemu mamake ndiye humpa msaada.

Sehemu hii imeshughulikia athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa binadamu. Imedhihirika wazi kuwa binadamu ameathirika kwa njia mbali mbali, hasi na chanya. Binadamu alipopokea matendo ya utu kutoka kwa viumbe hawa, aliweza; kufurahia, kutoa shukrani, kukasirika, kupata jazba ya kutenda mambo fulani, kutoelewana na wenzake kuhusu mambo fulani na hata kushirikiana pamoja na viumbe wa kiuhalisiajabu.

4.4 Hitimisho

Sura hii umebainisha uchambuzi wa data. Imebainika kwamba viumbe wa kiuhalisiajabu wamechukua maumbo kama vile: ishara, sauti, mzuka, maumbo yasodhihirika, jinni miongoni mwa mengine wanapodhihirisha utu. Aidha hubainisha utu kwa njia kama vile: kuonyesha upendo, kutahadharisha binadamu, kuongoza binadamu, kuwapa motisha, kuonyesha ukarimu na mengineo. Utu wao umeonyeshwa kuathiri binadamu kwa hali kama vile: binadamu kufurahi, kushangaa, kutoa shukurani, kutoelewana na mengineo. Vilevile imedhihirika kuwa utu ni sifa mojawapo aliyonayo binadamu na viumbe wa kiuhalisiajabu pia wameionyesha. Viumbe hawa wa kiuhalisiajabu wameweza kusheheni tu sifa hii wakiwa katika maumb tofauti. Hali kadhalika, binadamu wameweza kuathirika kwa njia tofauti kutokana na utu waliopata kutoka kwa viumbe wa kiuhalisiajabu. Athari hizi zimekuwa hasi na chanya. Muhtasari wa data umedokezwa katika sura inayofuata. Vilevile, mapendekezo ya utafiti yameweza kudokezwa. Mwandishi pia amezungumzia changamoto za utafiti na hatimaye Mchango wa utafiti.

SURA YA TANO: MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti umejishughulisha na muhtasari wa matokeo ya utafiti mintarafu ya malengo ya utafiti na misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu kama yalivyoibuka kutokana na uchanganuzi wa Riwaya za: *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (2010)*. Vile vile, inatoa hitimisho na mapendekezo ya utafiti. Pia, imeangazia manufaa ya utafiti huu na hali kadhalika, matatizo yaliyokumba utafiti huu. Kwa kutamatisha, mtafiti amependekeza tafiti zingine zinazoweza kufanywa kuhusiana na utafiti huu.

5.1 Muhtasari

Sehemu hii inawasilisha muhtasari wa utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Inaanza kuwasilisha muhtasari wa tasnifu kabla ya kuainisha muhtasari wa matokeo ya utafiti.

5.1.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano.

Katika sura ya kwanza masuala ya kimsingi katika utafiti kama: usuli wa utafiti ambapo umuhimu wa utafiti umeelezwa huku mianya ikidhihirishwa, suala la utafiti ambalo limeshughulikia kichochezi cha kuchagua mada, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada lililotumika kueleza sababu kuu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti inayoonyesha vitabu vilivyoshughulikiwa na misingi ya kinadharia kilichoeleza kwa kina kuhusu nadharia yameshughulikiwa.

Katika sura ya pili, mapitio ya maandishi kuhusu suala la uhalisiajabu, wahusika na uhusika na utu limeshughulikiwa. Sehemu hii ni muhimu sana kwa utafiti kwa kuwa unamwelekeza mtafiti kuhusu yale ambayo yamezungumziwa kuhusu mada. Humsaidia mtafiti kujua masuala yaliyoshughulikiwa na yasiyoshughulikiwa na katika kiwango kipi. Hivi humsaidia kujenga maudhui mazuri ya kazi yake.

Katika sura ya tatu imefafanua namna utafiti ulivyofanyiwa. Sehemu zilizoshughulikiwa ni muundo wa utafiti ambao umeonyesha muundo uliotumika katika uhakiki wa riwaya, eneo la utafiti iliyosheheni mahali pa kufanya utafiti na vitabu vilivyotumika, usampuli na usampulishaji ulioeleza jinsi mtafiti aliweza kuteua riwaya zile teule, ukusanyaji data iliyoshughulikia jinsi

aliweza kupata data kutoka kwenye riwaya teule, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data umeshughulikiwa. Pia sehemu ya utegemezi na uaminifu katika data ya utafiti ipo ili idhihirike wazi kwa nini data iliyopatikana ni ya kweli. Hatimaye sehemu ya maadili ya utafiti ipo kuonyesha kuwa mtafiti alipata idhini kutoka afisi tofauti tofauti ili kuweza kufanya utafiti wake.

Katika sura ya nne matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti yameelezwa kwa upana na kina. Utafiti umewasilisha viumbe wa kiuhalisiajabu wanavyodhihirisha utu, maumbo tofauti wanayojitokeza wanapoonyesha utu na hatimaye athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa binadamu.

Hatimaye, sura ya tano imetoa muhtasari wa utafiti mzima, matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu, mapendekezo yaliyotolewa kuhusu namna binadamu anafaa kupata ujumbe kuhusu umuhimu wa utu na maoni ya mtafiti kuhusu tafiti ambazo zinafaa kufanywa baadaye.

5.1.2. Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza “Utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Lengo kuu la utafiti ilikuwa ni kuonyesha utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu unavyosawiriwa katika riwaya teule za Said A. Mohamed: *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Utafiti huu ulilenga kubainisha jinsi viumbe wa kiuhalisiajabu wanavyodhihirisha utu, umbo lao wanapodhihirisha utu na athari ya utu huu kwa viumbe binadamu. Aidha, upungufu wa utafiti wa kina kuhusu usawiri wa utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu ulichangia kufanywa utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisiajabu na mihimili minne ya nadharia ilitumika kuelekeza utafiti huu.

5.1.1.1 Umbo la Viumbe wa Kiuhalisiajabu

Viumbe mbalimbali wameweza kudhihirisha utu kupitia maumbo tofauti. Mara nyingi, viumbe hawa wamekuwa wakijitokeza kwa wapendwa wao kupitia maumbo mbalimbali. Wamejitokeza kutumia maumbo kama vile kama vile mizuka, sauti za wafu, vivuli vya wafu, picha kutoka kwenye albamu, malaika, nyuso bila miili na hata maumbo mengine yasiyoweza kudhihirika. Mzuka katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) anamtokezea kilembwe wake K. K alikuwa mtoto wa mjukuu wake, ambaye alimpenda na kumuenzi. Anaona K akipotoka kwa kuanza kuishi maisha mbovu, ambayo hakupaswa kuishi haswa kutokana na malezi waliyoipata watu wa ukoo

wake. K anaishi maisha ya kifahari ya kuharibu mali na pesa anayopata kwa njia mbaya ya kuwakandamiza wananchi wenzake. K anampa mbwa wake Doggy kipaumbele ilhali kuna watu ambao hata chakula hicho anachowapa mbwa hawawezi kukipata. Babu anamtokezea K kila mara kumwonya na kumwongoza anavyoweza kuishi maisha mema. Hata anamtolea hukumu kwa kuamini kuwa atabadilika. Mabadiliko ya K hayadhihiriki wazi kwa kuwa anapotoka katika dunia ya wafu na kurudi katika dunia yake, anapata mali yake yameharibika. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), marehemu mamake Nana alikuwa akimtokezea Nana nyakati nyingi. Alikuwa kumuonya, kumsaidia alipokuwa mashakani, kumpa motisha katika hali ngumu za maisha na hata kumuelekeza. Nana alikuwa mwanawe ambaye hakuweza kumlea kama mzazi kwa kukosa fursa kutokana na kifo. Hivyo alijitokeza kwa Nana ili kupata nafasi ya kuwa naye na kumpa malezi ambayo hakumpa.

5.1.1.2 Udhihirikaji wa Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu

Utafiti huu umebainisha kuwa utu ni mojawapo wa sifa muhimu katika maisha ya binadamu. Utu kwa kawaida huhusishwa na binadamu ila imefahamika kuwa hata viumbe wengine huweza kudhihirisha utu. Mwandishi Said A. Mohamed ameweza kudhihirisha wazo hili kupitia usawiri wa viumbe wa kihalisiajbu katika riwaya teule zilizoongoza utafiti huu. Mohamed ameweza kukosoa fikira za watu haswa waafrika ambao kupitia imani na mila zao wanaamini kuwa uhalisiajabu uhusishwa na nguvu za giza ambazo matokeo yake huwa hasi haswa kwa binadamu (Mbiti, 1980).

Kupitia kwa riwaya teule za Said A. Mohamed, utu ulijitokeza kwa namna nyingi. Aghalabu kila riwaya imedhihirisha utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa njia tofauti. Kwa mfano waliwaonya kutokana na hatari iliyowakabili, waliwaonyesha mambo yalivyopaswa kufanywa, waliwatuliza katika nyakati ngumu, waliwapa motisha walipokaribia kukata tamaa maishani, waliwazuru wapendwa wao walipokuwa wapweke, waliwahamasisha kutokana na mambo yanayotokea katika jamii, waliwazindua walipoona wana mitazamo finyu na mengineyo. Kama msomaji wa kazi hizi za waandishi tunaweza kujifunza mengi. Tunaweza kujifunza jinsi sisi binadamu tunapaswa kuishi na binadamu wenzetu. Binadamu siku hizi wamegeuka kuwa wanyama. Maisha ya binadamu yamejaa uovu wa kila aina. Kila uchao tunasikia habari za vifo vya watu vinavyotokea kwa sababu ya uhasama wa binadamu. Binadamu wameishi kujitegemea tu kivyao bila hata kujali jirani yao. Binadamu wamejipenda kiasi cha kupata mtu akijitajirisha kwa kuwaathiri wenzake. Binadamu

wameacha kuwajali wenzao. Viongozi wakatemia mamlaka yao vibaya kuwanyanyasa wananchi ka kuwa wakwasi kwa niaba yao. Kupitia riwaya hizi, tunapata umuhimu wa utu. Umuhimu wa kupendana mtu na mwingine. Umuhimu wa kuelewana, umuhimu wa kusaidiana na hatimaye umuhimu wa upendo kwa jumla. Inajitokeza wazi kwamba, ili mtu aweze kufikia kiwango cha maisha alipo, humhitaji mwenzake. Bi. Mize katika *Dunia Yao* (2006) amemsaidia mwandishi Ndi kukwea kutoka katika uandishi wa uhalisia hadi kufikia uandishi wa kiuhalisiajabu. Huenda mwandishi, kupitia hadithi ya Ndi, anatusimulia kuhusu maisha yake ya uandishi. Tunajifunza pia kuwa, pana umuhimu wa shukrani katika maisha yetu kwa wanao tusaidea.

5.1.1.3 Athari ya Utu wa Viumbe wa Kiuhalisiajabu kwa Binadamu

Athari zilizojitokeza kutokana na utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa binadamu zimebainishwa. Imebainika kwamba athari hizi hazijitokezi tu iwapo viumbe hawa wametuonyesha utu, bali pia hujitokeza binadamu wenzetu wanapotuonyesha utu. Matokeo haya ya utu hupokelewa kwa njia tofauti tofauti, chanya au pia hasi. Ila kwa wakati mwingi, utu hudhihirisha matokeo chanya. Kutokana na tendo hilo la utu, walioonyesha utu kwa wenzao walipata matokeo chanya kama vile: aliyepokea tendo kama ya kuonywa kutokana na kitu kutii. Baadhi walitii walipoonywa na kule kutii kwa kukawasaidia. Wahusika wengine waliweza kutoa shukrani kwa wale viumbe, kwa sababu ya kuwaonyesha utu. Hivyo, viumbe wale hawakukoma kurudi kuwasaidia walipokuwa na tatizo. Wahusika wengine waliweza kufaulu na kuishi maisha mema maishani kutokana na msaada waliopata kutoka kwa viumbe hawa. Mkondo wao wa maisha uliweza kubadilika baada ya wao kufuata kila agizo walichopewa na kiumbe. Pia waliweza kuepuka hatari zozote zilizowakabili baada ya kuonywa na viumbe hawa. Kutokana na utu ulioonyeshwa na viumbe hawa kwa wapendwa wao, uliweza pia kuathiri waliokuwa karibu nao. Hivyo utu ulipojitokeza, aliyetokezewa alifaidika pamoja na wenzake. Kuna waliopokea tendo la utu na ikawaathiri kwa njia hasi pia. Mzozo wakati mwingine ulijitokeza kati ya kiumbe na binadamu aliyekuwa akipokea tendo la utu. Wakati mwingine, alipolemewa binadamu, alimalizia tu kwa kukimya kama aliyekuwa hasikilizi chochote.

5.2 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, hitimisho ulifikwa kwa msingi wa maswali na madhumuni ya utafiti. Suala la umbo la viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed

limejitokeza. Viumbe hawa wameonekana wakijitokeza katika maumbo mbalimbali wanapodhihirisha utu. Wamejitokeza kama; mzuka, kivuli, sauti, malaika, jini, binadamu halisi na hata kwa umbo ambalo haliwezi kuelezwa bayana. Maumbo haya wakati mwingine yanaonekana yakiwashtua binadamu. Hata hivyo, walitekeleza majukumu yao katika yale maumbo. Ni suala la ajabu kwa viumbe wa kiuhalisiajabu kudhihirisha utu. Utu ni sifa ambayo huhusishwa na binadamu. Hata hivyo, sifa ya utu ulijitokeza katika viumbe hawa. Viumbe hawa wa kiuhalisiajabu walijitolea kuwasaidia binadamu kwa njia mbali mbali. Viumbe hawa wameonekana wakionyesha sifa mbalimbali za utu kwa binadamu. Sifa hizi za utu zilivyojitokeza ni kama; upendo, heshima, kutoa msaada, kuwajibika, kusamehe na mengineyo. Sifa hizi haswa zilijitokeza viumbe hawa walipokuwa wakitangamana na binadamu. Ni jambo la kawaida kwa mtu kuathirika kwa njia mbalimbali anapolipokea tendo fulani kutoka kwa mwenzake. Imedhihirika wazi kuwa binadamu ameathirika kwa njia mbali mbali, hasi na chanya kutokana na matendo ya utu waliyoyapokea kutoka kwenye viumbe wa kiuhalisiajabu. Binadamu alipopokea matendo ya utu kutoka kwa viumbe wa kiuhalisiajabu, aliweza; kufurahia, kutoa shukrani, kukasirika, kupata jazba ya kutenda mambo fulani, kutoelewana na wenzake kuhusu mambo fulani na hata kushirikiana pamoja na viumbe wa kiuhalisiajabu kutekeleza mambo fulani.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia kipengele cha utu wa wahusika wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Aidha ulishughulikia utu wa viumbe hawa unavyodhihirika, umbo lao wanapojitokeza kuonyesha utu na athari ya utu wa viumbe hawa wa kiuhalisiajabu kwa binadamu. Hivyo kutokana na utafiti huu, mtafiti anapendekeza suala la utu lipewe kipau mbele katika jamii. Kutokana na utu maisha huwa yenye upendo na Amani. Hivyo, nyenzo tofauti kama vile ufundishaji wa fasihi andishi na fasihi simulizi zitumiwe kujulisha watu kuwa sifa ya utu ni sifa muhimu katika maisha ya binadamu. Mtafiti anapendekeza pia kuwa suala la uhusika liwe suala la kushughulikiwa vilivyo katika fasihi za Kiswahili. Hii ni kwa sababu katika maisha yetu binadamu na viumbe wengine kwa wakati fulani huhusishwa na fasihi na huwa wahusika. Utafiti huu uwe kichocheo kwa watafiti wengine kushughulikia suala la utu na uhusika katika jamii.

5.4 Mapendekezo kwa ajili ya Tafiti Zaidi

Kuna mapendekezo anuwai yanayoweza kuzingatiwa na watafiti wengine katika tafiti zaidi za baadaye, hii ni kwa kuwa hakuna utafiti unaoweza kukamilisha kila jambo. Masuala mengine

yanayoweza kushughulikiwa ni kama vile; Kushughulikia jinsi mtindo wa uandishi wa kiuhalisiajabu umechangia katika kukua kwa fasihi ya Kiswahili.

Pia utafiti unaweza kufanywa kuhusu uhalisiajabu katika vipera vingine vya fasihi andishi kama vile tamthilia, hadithi fupi na hata ushairi.

Mbinu tofauti za uandishi zinajitokeza haswa na suala la uhalisiajabu, mbinu hizi zitambulishwe na zishughulikiwe katika maandishi tofauti ya uhalisiajabu.

Utafiti wa kina unaweza kufanywa kuhusu vipengele vingine vya uhusika wa viumbe wa kiuhalisiajabu na hata utafiti linganishi kuhusu suala la utu wa binadamu na viumbe wengine wasio binadamu.

5.5 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikabiliwa na matatizo. Miongoni mwa matatizo ni changamoto ya tafsiri ya baadhi ya mapitio ya maandishi kwa sababu yalikuwa katika lugha ya Kingereza. Maneno mengine yalikosa visawe vya Kiswahili ikabidi mtafiti kutoa maelezo marefu ili kueleweka. Licha ya hayo, kwa neema ya Mwenyezi Mungu, mtafiti alitia juhudi kubwa ili kufanikisha utafiti huu ambao unalenga kwa kiasi kikubwa kuchangia katika kufanikisha usomaji na ufundishaji wa somo la fasihi kwa mazingatio ya kuelimisha watu kuhusu umuhimu wa utu.

5.6 Mchango wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomi na hata waandishi wa fasihi. Umedhamiria kuwaandaa binadamu kuelewa maana ya utu, na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Aidha umeonyesha kuwa utu haujitokezi tu kwa kiumbe binadamu bali hata kwa viumbe wengine. Imebainika kuwa, utu kwa kiasi kikubwa kina athari chanya katika maisha ya binadamu. Binadamu wanafaa kuwa wenye utu kwa wenzao na hata kwa wanyama.

Utafiti huu umeweza kubainisha jinsi utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu unavyosawiriwa katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Isitoshe, umefungua ukurasa mpya wa kuchunguza, kutathmini na kujadili kwa makini matumizi ya riwaya za Kiswahili. Imebainisha kwamba kazi ya sanaa ni njia bora zaidi ya kuelimisha jamii kuhusu suala lolote katika jamii. Fauka ya hayo, utafiti huu umeweka wazi utu unavyodhihirika katika jamii na kuwapa moyo waandishi wa riwaya hizi waendeleo kuandika. Hivyo basi, riwaya hizi teule zimedhihirika kuwa gurudumu la kuburudisha, kuhamasisha, kuelimisha jamii na hivyo kuongeza dhima ya fasihi andishi kwa jumla.

MAREJELEO

- Alexander, M. (1990). *Flights from Realism*. London: Edward Anold.
- Alomo , S. O. (2016). Uwakilishaji wa Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili iliyoandikwa na Said A. Mohamed na Wadi K. Wamitila.” (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Egerton
- Assumpta, K. (2014). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publishers
- Augustin (1955). ‘*Essays in philosophical theology*’ Reff.in Encyclopedia of philosophy vol.3:138 [www.str.org/articles retrieved on 9/8/2019](http://www.str.org/articles/retrieved%20on%209/8/2019)
- Awdhesh, S. (2014). Good and Evil. Ajjahabad; Aatmic Science Publication (A Division of Aatmic Science Publication.)
- Baldic, M. (1997). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (2nd edition). Toronto: University of Toronto Press.
- Battle, M (2009). Ubuntu: I in You and You in Me. Church Publishing Inc.
- Bertoncini, E. Z. (1989). *Outline of Swahili literature*. Leiden: E. J. Brill.
- Chanady, A. B. (1985). *Magical Realism and the Fantastic*. New York: Garland Publishing Inc.
- Chepkoech, T. (2018) “Usawiri wa maudhui yenye kufunza wanafunzi wa vyuo maadili mema: Tathmini ya Alidhani Kapata na Damu Nyeusi.” (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Fiction*. New York: Routledge.
- Crysal, L. (1987) “Humanity; A bridge between nature and the Supernatural”- Unpublished Literary review.
- Danow, K. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grotesque*. Kentucky University of Kentucky Press.
- Faris, W. B. (2004) Ordinary Enchantments: Magical Realism and Remystification of Narrative. Nashville: Vanderbilt University Press.
- Gade, C.B. (2011) The Historical Development of Written Discourses on Ubuntu. *South African Journal of Philosophy*, 30 (3), 303-329
- Gilbert, E. (2010). Magical Realism and Visionary Materialism in Okri and Blake. *Dreams of Freedom*, 15 (1), 18-32.
- Gromov, M. D. (2002). Nagona and Mzingile Novels, Tale or Parable. Swahili ForumVAAP No. 55.
- Hailey, J. (2008). *Ubuntu: a literature review document*. London: Tutu Foundation.
- Hart, S. M. (2003). *Magical Realism in the Americas: Politicized Ghosts in One*.

- Hill, J.S (1977). *The Romantic Imagination*. London: Macmillan Press Ltd.
- Jackson, T. (2010) Tim Jackson's Economic Reality Check. Speech. <https://doi.org/10.4324/9781849774338> Retrieved 19/10/2021.
- Kezilahabi, E. (1976) Ushairi wa Shaaban Robert. Nairobi: KLB.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Khamis, S. A. M. (2005). "Vionjo Vya Riwaya Mpya ya Kiswahili." Research in African Literatures 36/1: 92-108. Bayreuth: Bayreuth University.
- Khoza, R. J. (2006). *Ubuntu, botho, vhuntu, African Humanism*. Johannesburg: African Morning Star Publishers.
- Kimani, C. (2003). "Swala La Dhuluma Dhidi ya Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)
- Kimeu, N. A. (2016) "Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti." Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)
- King'ei, K. G. (2002). "Fantasy and Realism in the Modern Kiswahili Novel: A Critical look at *Babu Alipofufuka* by S. A. Mohamed."- Unpublished literary review.
- Kithaka, W. M. (2002). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications.
- Lamont, F. C. (1997). *The philosophy of humanism*. New York: Amherst.
- Lutz, D. W. (2009). African urban philosophy and global management. *Journal of Ethics*, 84(3), 313-328
- Lynch, P. A. na Roberts, J. (2010). African Mythology A to Z (second edition). <https://img.fireden.net/tg/image/1454/78/1454787608049.pdf>
- Madumulla J. S (2009). *Riwaya ya Kiswahili. Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Phoenix Publishers Nairobi.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.
- Maganju, J. (2004). 'Uhakiki wa Uhalisiajabu katika Bin-Adamu (2002) na Babu Alipofufuka (2004). Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Mandela, N. (1994). *A Long walk to freedom*. Boston, Little Brown.
- Masatu, F. J. (2019). Uhusika wa sauti kama mhusika katika uteuzi na ujenzi wa dhamira katika tamthilia ya kiswahili: Mfano wa tamthilia ya usiniue (2019) ya Eric F. Ndumbaro na Maria N. Isaya. *International Academic Journal of Social Sciences and Education*, 1, 39-58

- Mazrui, A.M & Syambo, B .K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi* .Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbatia, M. (2002). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks.
- Mbigi, L. (1997). *Ubuntu: The African dream in management*. Pretoria: Sigma.
- Mbiti, J. S. (1980) *The Encounter of Christian Faith and African Religion*. At www.christiancentury.org Retrieved 25/08/2019 On-line version published by Religion Online.
- Mbiti, J. S. (1991). *African Religion and Philosophy*. Nairobi. Heinemann.
- Mbote, P. K. (1995) *The Law of Succession in Kenya: Gender Perspectives in property Control and Management*. Nairobi www.ielrc.org retrieved on 22/4/2021
- Mgeni, A. (1982). *The Elements of Mystery in novels of Mohamed Said Abdalla. Jarida la Kiswahili, 2.*
- Miruka, O. (1994). *Encounters with Oral Literature*. Nairobi. East African Publishers.
- Murithi, J. (2018) “Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.” *Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta* (Haijachapishwa)
- Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mokgoro, Y. (1997). *Ubuntu and the law in South Africa*. Johannesburg: In Seminar Report Constitution and the Law.
- Msila, B. (2015) *Ubuntu and its potential impact on the international social work profession*. *International Social Work*. 64 (5), 649-662. doi: 10.1177/00208728211022787.
ISSN 0020-8728
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mturo, N.G., Omboga, Z., and Wamutiso, K. (2018). *Uhalisiamazingaombwe katika Muktadha wa Ubaadaukoloni: Mchango wa Vita vya Mapenzi ya Maundu Mwingizi*,. Vol. 3, No. 1, Pages 22 - 31, ISSN 2520-0577
- Mugumbate, J. Nyanguru. A. (2013) *Exploring African Philosophy: The value of Ubuntu in Social Work*. 3 (1), 82-100.
- Mugwika, F. (2012). *Dhana ya Uchichimizi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kimajaribio ya Mafamba*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi. (Haijachapishwa).

- Mwachofi, A. K. (1987). *Mama ee*. East African Educational Publishers. Nairobi.
- Mwangi, J. (2013). Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya Mpya. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa)
- Ndanu, A. (2018). Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Fasihi. Rock Island, Augustana College.
- Nyambuga, V. A. (2005). "Uhakiki wa Bina-Adamu! (2002) na Musa leo (2004) na Wamitila K. W. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Okri, B. (1992). *The Famished Road*. New York: N. A. Talese.
- Olali, T. (2010). *Structure and Anti-Structure of a Swahili New Novel: A stylistic Analysis Babu Alipofufuka*.
- Onchwati, J. S. (2016). Uhalisiajabu Unavyojitokeza katika Ukawafi wa Miiraji na Utenzi wa Fumo Liyongo. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi. <http://hdl.handle.net/11295/100224>
- Oruka H.O. (1990). *Ethics*, Nairobi: Nairobi University.
- Palmer, F. (1992). *Literature and Moral Understanding*. Oxford: Clarendon Press.
- Pietersen, H. J. (2005). Western Humanism, African Humanism and Work Organization. *SA Journal of Industrial Psychology*, 31(3), 54-61.
- Rio, F. (2002). Magical Realism Definitions. Unpublished.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Shen, F. (2006). "Narrative Strategies in Robert Cormier's Young Adult Novels." PhD Dissertation, Ohio State University.
- Samba, R. (2018) "Uhusika katika mashairi ya Kiswahili: Malenga wa Vumba, Kichomi na Utenzi wa Fumo Liyongo." (Tasnifu ya Uzamili) Chuo Kikuu cha Maseno, Kisumu.
- Samkange, S.J.W.T. and Samkange, S. (1980) *Humanism or Ubuntuism: A Zimbabwe Indegenous Political Philosophy*. Harare: Graham Publishing
- Syambo, K. Mazrui (1992) Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi: EastAfrica Education Publishers
- Tebbe, N. (2008). Inheritance and Disinheritance: African Customary Law and Constitutional Rights. *The Journal of Religion* 88(4), 466-496, doi: 10.1086/589947 Retrieved on 22/4/2021

- Thomas, H. K. (2004) “Training Strategies for Improving Humanity.” (Doctoral Dissertation). University of Colorado, Boulder.
- TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Tutu, D. (2000). *No future without forgiveness: A Personal Overview of South Africa’s Truth and Reconciliation Commission*. London: Rider Random House.
- Tutu, D. (2004). *God has a Dream: A Vision of Hope for Our Time*: New York Doubleday.
- UK. (November 2018). *Humanity Is The Only Religion Theology Religion Essay*. At <https://www.ukessays.com/essays/theology/humanity-is-the-only-religion-theology-religion-essay.php?vref=1> Retrieved on 30/9/2019
- Vutagwa (2013). “Sifa za uhalisiajabu katika Utenzi wa Mwana Fatuma.” (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Venter, M. (2004). May the Real Ubuntu Please Stand Up? *Journal of Media Ethics*. 30 (2), 125-147. doi: 10.1080/23736992.2004.1020380
- Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2010). “Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao na The Tin Drum*.” *SWAHILI FORUM* 17. Uk 143-157. Mainz: Johannes Gutenberg University.
- Wamitila, K.W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi* (chapa ya tano). Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wanjiru, M. J. (2013). Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya za Babu Alipofufuka na Watu wa Gehhena. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Wichtner-Zoia, Y. (2012). Could the philosophy of ubuntu support community connections, development and economic prosperity in your community? At http://msue.anr.msu.edu/news/ubuntu_is_powerful_thinking Retrieved 21/05/2021
- Zamora, L. P. & Wendy, B.S. (1995). *Magical Realism Theory, History, Community*. London: Duke University Press.

KIAMBATISHO 1: IDHINI YA CHUO YA KUFANYA UTAFTI

KIAMBATISHO 2: IDHINI YA ERC CHUO KIKUU CHA JOOUST

KIAMBATISHO 3: KIBALI CHA NACOSTI